

**Uchunguzi  
Wa  
Agano  
Jipyä**

**Na Robert Stapleton**

## UCHUNGUZI WA AGANO JIPYA

| <u><b>Yaliyomo</b></u>   | <u><b>Ukarasa</b></u> |
|--|-----------------------|
| 1. Kitabu Cha Pumzi Ya Mungu   | 3                     |
| 2. Utollewaji Kwa Uwezo Uhifadhi                                     | 5                     |
| 3. Mazingira Ya Kihistoria Ya Agano Jiypa                            | 8                     |
| 4. Mathayo – Mfalme Na Ufalme Wake                                   | 11                    |
| 5. Marko – Mtumishi wa Yehova  | 15                    |
| 6. Luka – Yesu Mtu Mkamilifu   | 18                    |
| 7. Yohana – Yesu Mtu wa Wote   | 22                    |
| 8. Matendo ya Mitume – Kufahamika Ukombozi                           | 26                    |
| 9. Warumi – Utii Wa Imani  | 29                    |
| 10. 1 Wakorintho – Matatizo Ya Kanisa Lilipo                         | 32                    |
| 11. 2 Wakorintho – Kujitetea Kwa Paulo Kuhusu Utume Wake             | 35                    |
| 12. Wagalatia – Ukweli wa Injili                                     | 39                    |
| 13. Waefeso – Utukufu kwa Kristo                                     | 42                    |
| 14. Wafilipi – Mawazo ya Kristo                                      | 45                    |
| 15. Wakolosai – Ubora Mkuu Wa Kristo                                 | 49                    |
| 16. 1 Wathesalonike – Ujio Wa Pili Wa Kristo                         | 52                    |
| 17. 2 Wathesalonike – Matukio Yanayotangulia Siku ya Bwana           | 55                    |
| 18. 1 Timotheo – Misingi Ya Vitendo Kwa Wahubiri                     | 58                    |
| 19. 2 Timotheo – Waraka Wa Mwisho wa Paulo                           | 61                    |
| 20. Tito – Kuliweka Kanisa Katika Utaratibu                          | 63                    |
| 21. Filemon – Barua Ya Kibinafsi Toka Kwa Mtume                      | 66                    |
| 22. Waebrania – Neno La Mwisho La Mungu                              | 69                    |
| 23. Yakobo – Waraka Wa Kutumia Akili Ya Kawaida                      | 73                    |
| 24. 1 Petro – Wito Kutumika KatiKati Ya Mateso                       | 76                    |
| 25. 2 Petro – Wito Kwenye Ufahahmu Katikati ya Mafundisho ya Upotofu | 78                    |
| 26. 1 Yohana – Waraka Wa Upendo Toka Kwa Mtume Wa Upendo             | 82                    |
| 27. 2 Yohana – Barau Kwa Mkristo Mwanamke                            | 85                    |
| 28. 3 Yohana – Viongozi Watatu Katika Kanisal la Awali               | 87                    |
| 29. Yuda – Kuishindania Imani  | 89                    |
| 30. Ufunuo – Msiba Na Shangwe  | 92                    |

## **UCHUNGUZI WA AGANO JIPYA**

### **SOMO LA I - KITABU CHA PUMZI YA MUNGU**

#### **UTANGULIZI:**

1. Kama Biblia sio mkusanyiko wa maandiko yaliyovuviwa , basi haiwezi kuathiri tunavyoishi, kuamini au kuabudu.
2. Biblia ni kitabu cha ajabu kupita vyote ulimwenguni.
  - A. Kimojawapo cha vitabu vya zamani kupita vyote duniani.
  - B. Kilichotafsiriwa mara nyingi zaidi duniani.
  - C. Kipendwacho zaidi na kuchukiwa zaidi ya vyote duniani.
  - D. Kilichosomwa zaidi na kupuuzwa zaidi ya vyote duniani.

#### **MJADALA:**

1. Madai Kwamba Ni Neno La Uvuvio Wa Mungu.
  - A. Je, Biblia inaweza kutumika kujithibitisha yenewe kuhusu kwamba ni **uvuvio**?
    1. Shahidi huruhusiwa mahakamani kujitetea mwenyewe.
    2. Thamani ya machimbo hujulikana kutokana na madini ndani yake yaliyopatikana.
    3. Biblia ina kila sababu ya kutumika kama ni shahidi ya yenewe.
  - B. Madai ya Agano la Kale kuvuviwa.
    1. Zaidi ya semi 3800 za A.K. katika, “Hivyo asema Bwana”.
    2. Daudi alidai uvuvio katika maneno ya 2 Sam. 23:2
  - C. Madai Ya Uvuvio Wa Agano Jipy.
    1. 1 Kor. 14:37
    2. 1 Thes. 2:13
    3. Paulo alinukuu toka A.K. na A.J. katika 1 Tim. 5:18.
      - A. Kumb. 25:4; Lk. 10:7.
    4. Maandishi ya Paulo yalitajwa na Petro kuwa ni Maandiko 2 Pet. 3:15, 16.
2. Uvuvio Ni Nini?
  - A. Latokana na neno la Kiingereza ambalo nalo latokana na neno la Kilatini la “Kutoa pumzi”.
    1. 2 Tim. 3:16, kama maneno yasemavyo, Pumzi ya Mungu.
  - B. Mawazo mbali mbali kuhusu uvuvio:
    1. “Genius View”
      - A. Hayo hujumuisha yale ya wasanii wa uchoraji, muziki na waandishi.
        1. Hupingana na Mt. 4:4.
    2. “PARTIAL view”.
      - A. Hayo hudai kuwa Biblia imevuviwa katika maeneo ya mafundisho, lakini sivyo katika Historia, Jiografia au Sayansi.
        1. Mtazamo umeingia ndani ya makanisa ya madhehebu, shule na seminari.
        - B. Hupingana na 2 Tim. 3:16 - Kila andiko lenye pumzi ya Mungu....”
    3. “Neo - Orthodox View”
      - A. Maoni ni kwamba Biblia ina asili ya kibinadamu (katika mawazo yake) na ndani yake mna makosa, lakini Mungu aliitumia pamoja na makosa hayo.
      - B. Kama Biblia ina makosa tutazitambuaje sehemu zenye makosa na zile zisizo na makosa?

1. Je, Mpango wa wokovu ni kama vile ulivyo tajwa katika Agano Jipy? Na je, ni sahihi?
    - A. Kama Biblia ina makosa tunajua ni wapi?
  2. Je, mambo mengine - 2 Pet. 1:3?
  4. "Mechanical or Dictation View".
    - A. Isingeruhusiwa taratibu za uandishi wa kibinafsi tuuonao ndani ya Biblia leo.
    - B. Utaratibu huo Mungu aliutumia mara chache sana - Mdo. 2:39; Hes. 22:22-35.
  5. "Thought View".
    - A. Maoni kwamba Mungu alitoa mawazo lakini akamwachia mwandishi kuchagua maneno ya kutumia.
    - B. Vipi kama mwandishi alichagua maneno yasiyo sahihi?
      1. Biblia hudai uvuvio wa neno - Yer. 1:9.
  6. "Verbal Plenary View"
    - A. Biblia kudai imevuviwa kwa njia hii 2 Sam. 23:2, Yer. 1:9, 1 Kor. 2:9-13.
    - B. Aina hii ya mawazo husisitiza ukamilifu wa uvuvio.
3. Biblia Kudai Uvuvio Kamili
- A. Agano la Kale hudai uvuvio wa maagizo ya mdomo - 2 Sam. 23:2; Yer. 1:9.
  - B. Agano Jipy hudai uvuvio - 1 Kor. 2:9 - 13.
    1. Roho Mtakatifu alifunua mawazo ya Mungu kuitia watu wa Mungu - 2 Pet. 1:20,21.

### **MWISHO:**

1. Biblia yote imevuviwa
  - A. Ifahamike pia nyakati zingine uvuvio unapatikana katika neno lililorekodiwa kuliko tukio halisi au maneno halisi - Mwa. 3:4, 5, n.k.
2. Kwa sababu Biblia ni uvuvio, haina makosa likiwa ni neno la Mungu, mwanadamu hulikataa kwa kujihtarisha ye ye mwenyewe milele - Yn. 12:48.

## **SOMO LA II - UTOLEWAJI KWA UWEZA UHIFADHI**

### **UTANGULIZI:**

1. Biblia imetolewa kwa maelezo ya uvuvio ya mdomo.
2. Mwanafunzi wa Biblia anahitaji kujifunza uhifadhi wa Biblia hadi leo.

### **MJADALA:**

#### **1. VYANZO MBALIMBALI VYA SOMO.**

- A. Baadhi ya maneno yanahitaji kuainishwa katika mjadala
  1. CANON - asili yake ni Kiyunani na humaanisha kifaa/fimbo (kinachoongoza na kimenyooka). Hii inakusudia kwamba vitabu vihusika vyakubalika kama Maandiko Matakatifu.
  2. AUTOGRAPH - asili yake kuonyesha kumbukumbu iliandikwa na mvuviwa.
  3. Apocrypha - asili yake ni baadhi ya vitabu kushirikishwa (kuingizwa) mara nyingi katika Biblia, lakini havitazamwi kama vya uvuvio.
    - A. Hivi viko katika Biblia ya Katoliki.
    - B. Maandiko ya Agano la Kale.
      1. Agano la Kale liliandikwa na waandishi kiasi cha thelathini - na - wawili, kuanzia Musa (1500 K.K.) hadi Malaki (400 K.K.).
        - A. Kumb. 31:36 - Kitabu cha sheria kiliwekwa ndani ya sanduku la Agano.
        - B. Danieli 9:10-13 - Sheria ya Musa imetajwa na Danieli.
        - C. Isaya 34:16 Kitabu cha Bwana kumetajwa na Isaya.
        - D. 2 Fal. 22:8 - Kitabu cha sheria kilipatikana wakati wa Yosia.
      2. Katika mapokeo ya Kiyahudi Ezra anasifiwa kwa kukusanya vitabu vya Agano kuwa kitabu kimoja.
      3. Josephus aliandika kwamba kuanzia kifo cha Artashasta (424 K.K.) hakuna kilichoongezwa katika A.K. au kufanya mabadiliko yo yote katika maelezo.
- C. Maandiko ya Agano Jipy.
  1. Vitabu vya Agano Jipy, yalichukuliwa kuwa Maandiko ya Mungu tangu wakati yalipoandikwa.
    - A. 1 Kor. 14:37; 1 Thes. 2:13; 1 Tim. 5:18; 2 Pet. 3:15,16.
  2. Vitabu vya Agano Jipy vilisambazwa punde baada ya kuandikwa Kol. 4:16.
  3. Wakati wa karne ya kwanza na mapema karne ya pili, vitabu vya Agano Jipy vilinukuliwa kama Neno la Mungu.
    - A. Clementi (95 B.K.) aliandika barua mbili kwenda Korintho akinukuu kutoka Waraka wa 1 na 2 kwa Wakorintho.
    - B. Papias, mwanafunzi wa Polycarp aliyejewa mwanafunzi wa mtume Yohana alihusisha vitabu vya Mathayo na Marko kama vitabu viwili vya kwanza katika Agano Jipy.
    - C. Kufikia karne ya nne vitabu vyote vya A.J. vilikuwa vimekusanya katika kikundi cha mkusanyo mmoja wa maandiko.

#### **2. KUHIFADHI MAELEZO YA MAFUNDISHO:**

- A. Kunusurika kwa Biblia katika miaka mingi kumetumika kuonesha uvuvio wake.
- B. Maandiko ya Agano la Kale yalikusanya kutunza usahihi.
  1. Waandishi walinukuu maelezo kwa mkono.
  2. Walioga kabla ya kufanya nukuu.

3. Kila herufi katika kila ukurasa ilihesabiwa.
  4. Kama kulifanyika makosa, kalamu ilivunjwa na ukurasa kurudiwa.
- C. Vyanzo vikuu vitatu vya Agano la Kale
1. Maandiko ya Kiyunani (Septuagint) katika mji wa Alexandria, Misri, katika Karne ya 3 K.K.
    - A. Yalisaidia maandalizi ya kuja kwa Kristo.
    - B. Yalitumika kama "Biblia" ya Kristo kwa mitume na Wakristo wa awali.
  2. Maandiko ya Wayahudi (Masoretic) katika karne ya 9 A.D.
  3. Maandiko yaitwayo: Dead Sea Scroll yaliyopatikana mwaka 1947.
    - A. Kila kitabu cha A.K. kimewakilishwa (kimeandikwa), isipokuwa kitabu cha Esta.
    - B. Tarehe kuanzia nyuma kiasi cha 200 B.C.
    - C. Huafikiana vema kabisa kama yale ya Masoretic.
    - D. Vitabu vya Agano Jipy a vina ushuhuda mkubwa zaidi kuliko maandiko yale yanayopokelewa bila mashaka.
      1. Maandiko mengi ya asili yana Maandiko ya awali sehemu 5 au 6 tu.
      2. Karibu maandiko ya awali 3000 na maelezo ya Agano Jipy hurudi nyuma kiasi cha karne ya kwanza (uzamani wake).
  - E. Vyanzo vikuu vitatu vya A.J.
    1. Maandiko ya awali ya mkono.
    2. Tafsiri
    3. Dondoo toka kwa mababa (wakati wa mitume).
- F. Maandiko ya awali ya Agano Jipy.
1. Codex Vaticanus - Karne ya nne A.D.
    - A. Yamo ndani ya Maktaba ya Vatican tangu 1481.
    - B. Zimo kurasa 759 kati ya 820 za awali.
    - C. Yalilindwa na Kanisa Katoliki na hayakuwa yakipatikana hadi mwaka 1889 - 90.
  2. Codex Sinaiticus - Karne ya nne A.D.
    - A. Yalipatikana katika Jumuia ya kitawa ya Russian Orthodox kwenye mlima Sinai, aliye yapata alii twa Tishendorf (msomi wa Kijerumani).
    - B. Yalikabidhiwa kwa Czar wa Russia mwaka 1859.
    - C. Yalinunuliwa na British Museum katika mwaka 1933 kwa (100,000 pounds).
    - D. Yanajumuisha maandiko yote ya Agano Jipy na sehemu kubwa zaidi ya A.K.
  3. Codex Alexandrius - karne ya 5.
    - A. Katika jumba la Makumbusho la Uingereza lililoko London.
    - B. Yamekosekana mistari michache tu ya Agano La Kale Na Agano Jipy.
  4. Codex Ephraemi - karne ya 5.
    - A. Katika jumba la makumbusho ya Masomo ya Biblia Ufaransa, Katika mji wa Paris.
    - B. Maandiko katika ngozi ya ndama ya Biblia ya Kiyunani ambayo yalirudiwa na mwandishi katika karne ya 14.
    - C. Maandiko hayo huhusisha sehemu za Agano la Kale na kila sehemu ya Agano Jipy isipokuwa 2 Wathesalonike na 2 Yohana.
  5. Maandiko yaitwayo Papyri.
    - A. Maandiko yaitwayo Chester Beatty Papyri yana sehemu za Biblia ya Kiyunani kuanzia karne ya 2 hadi karne ya 4.
    - B. Maandiko The Rylands Papyrus 457 katika Maktaba ya John Rylands Manchester, England.
      1. Zimo sehemu zilizodumu kwa umri mrefu sana kutoka Yohana 18:18-31, 37, 38.
- G. Tafsiri za mwanzo.
1. Tarehe zake ni za zamani kuliko maandiko ya zamani yaliyoandikwa kwa mkono.
  2. Tafsiri ya OLD SYRIAC iliyofanyika karibu na mwisho wa karne ya kwanza (B.K.)

3. Tafsiri ya OLD LATIN iliyofanyika mapema mnamo karne ya pili. (B.K.)
  4. Tafsiri ya Peshita (SYRIAC PESHITTA) ilifanyika mnamo mwaka 425. Tafsiri hiyo ilitokana na kumbukumbu za Byzantine text, ambazo zimeitwa Textus Receptus, ambazo ndizo tafsiri ya KJV ilikotoka.
  5. Tafsiri ya COPTIC iliyofanyika Misri mapema mnamo 200 B.K.
  6. Tafsiri ya LATIN VULGATE iliyofanyika mwaka 384 (Agano Jipy) na 404 (A. la Kale) Hiyo ilifanywa na JEROME.
- H. Maandiko ya “Mababa wa kanisa”
1. Tarehe zake ni za zamani mpaka nyakati za uhai wa mitume.
  2. Kuna nukulu nyingi za maandiko matakatifu.
  3. Maandiko hayo ni ya zamani kuliko maandiko ya zamani yaliyofanywa kwa mkono.
  4. Agano Jipy lote laweza kutolewa toka katika maandiko hayo.

### **3. JE, TUNA BIBLIA YA UVUVIO LEO?**

- A. Hatuna maelezo ya awali ya vitabu vya Agano Jipy.
  1. Badala yake tuna nakala za nakala za nakala.
  2. Kama kumbukumbu halisi ya maandiko hayo imetunzwa, wanadamu wangezifanya sanamu (ya kuabudiwa ) - 2 Fal. 18:4.
  3. Waandishi wa Agano Jipy waliandika kwa pumzi ya Mungu, bali wafasiri hawakuwa hivyo.
- B. Tafsiri sahihi ina uvuvio kama ulivyo uvuvio wenywewe.
  1. Kama lugha ya tafsiri ni kweli kufuatana na lugha iliyotumiwa kutafsiri Biblia, basi lugha hiyo ya tafsiri ni uvuvio kama ile ya uvuvio.
  2. Yesu na mitume walidondoa kutoka tafsiri ya SEPTUAGINT (tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale toka Kiebrania ), na kuliita “neno la Mungu” au “Maandiko”.
  3. Kama leo hakuna tafsiri ya usahihi kama ule uvuvio, basi hatuna Neno la Mungu.

## **SOMO LA III - MAZINGIRA YA KIHISTORIA YA AGANO JIPYA.**

### **UTANGULIZI:**

1. Mungu aliwaandaa watu kwa ujio wa Mwanawe.
  - A. Alikuja ulipowadia “utimilifu wa wakati” - Gal. 4:4, 5.

### **MJADALA:**

1. **YESU ALIKUJA WAKATI WA UTAWALA WA KIRUMI - Dan. 2:31-45.**
  - A. Rumi ulianzishwa mwaka 753 K.K. kama jimbo la mji (lenye serikali).
    1. Kufikia mwaka 265 K.K. Rumi ilikuwa imeishinda Italia.
    2. Carthage ilishindwa mwaka 146 K.K. na kumaliza ugomvi wa miaka 200.
    3. Kisha Rumi iliangusha himaya ya Iskanda Mkuu (Alexander the Great)
    4. Palestina ilishindwa kwa Pompey kwa ajili ya Rumi mwaka 63 K.K.
    5. Uingereza na Gauli (Gaul) zilishindwa kwa Julius Caesar.
    6. Kufikia karne ya kwanza Rumi ilikuwa ikitawala sehemu kubwa ya ulimwengu wa Mashariki.
  - B. Historia ya mwanzo wa kanisa ilihamasishwa na utawala wa Kirumi - Dan. 4:17.
    1. Chini ya Julius Caesar, Rumi ilibadilika toka Jamhuri na kuwa ya Kiimra
    2. Alipouawa huyo Kaisari (Caesar) vita vya wenyewe kwa wenyewe vilizuka.
    3. Octavius - binamu wa Kaisari na mrithi (aliyeshinda katika vita), alitawala kuanzia 27 K.K. hadi 14 B.K. – Kama Augusto - Lk. 2:1.
    4. Huduma ya Yesu na kuzaliwa kwa kanisa kulikuwa chini ya Tiberio, aliyetawala tangu 14 B.K. hadi 37 B.K. - Lk. 3:1.
    5. Kaligula (Caligula) alitawala toka 37 - 41 B.K.
      - A. Hakuwa na akili nzuri, na alitaka aabudiwe kama Mungu.
      - B. Alikufa kabla hajatekeleza azma hiyo.
    6. Klaudio alitawala kuanzia 41 - 54 B.K.
      - A. Mwanahistoria mashuhuri, Suetonius, aliandika kwamba Klaudio aliwafukuza Wayahudi kutoka Rumi kwa sababu ya “fujo zilizoanzishwa na Christus”. - Mdo. 18:1, 2.
    7. Nero alitawala toka 54 - 68 B.K.
      - A. Aliwalaumu Wakristo kwa kuunguzwa Rumi mwaka 64 B.K.
      - B. Alimlaani (shutumu) Paulo.
      - C. Alijua, na vita vya wenyewe kwa wenyewe vikazuka baadaye.
    8. Rumi ilitawaliwa kwa muda mfupi na GALBA, OTHO na VITELLIUS kwa muda wa jumla mwaka 1.
    9. Vespasian alitawala kuanzia 69 - 79 B.K.
    10. Titus, aliyeushinda Yerusalem mwaka 70 B.K. alitawala kama mfalme (emperor) kuanzia 79 hadi 81 B.K.
    11. Domitian alitawala kuanzia 81 - 96 B.K.
      - A. Alijitangaza kuwa yeze ni mungu na akadai watu wamwabudu kama jaribio la kuona wanaitii kiasi gani Himaya ya Kirumi.
  2. **ISRAELI ILITUMIKA KAMA SEHEMU MUHIMU YA MPANGO WA MUNGU.**
    - A. Mstari wa uzao wa Kristo - Adamu, Seth, Nuhu, Shemu, Ibrahimu, Isaka, Yuda, Yesu, Yakobo, Daudi, Kristo - Mwa. 12:1-3; Mt. 1:1-17, Lk. 3:23 - 38.

- B. Nchi na sheria ilitolewa kwa Israeli na mtoaji akiwa Mungu - Mwa. 17:1 - 8; Kut. 20 - 31; Yoshua 21:43 - 45.
1. Sheria ilifanya kazi kama kiongozi kutuleta kwa Kristo - Gal. 3:23 - 25.
  2. Israeli iliogozwa na waamuzi - Mdo. 13:20.
  3. Ufalme uliouunganika ulidumu kwa miaka 120, Mdo. 13:21; 1 Fal. 2:11; 11:42.
    - A. Uligawanyika alipofariki Sulemani 1 Fal. 12:1-33.
    - B. Israeli ikaenda Ashuru (Assyria) utumwani mwaka 721 K.K., 2 Fal. 17:6 - 23.
    - C. Yuda ikaenda Babeli (Babylon) utumwani mwaka 586 K.K. - 2 Fal. 25:1 - 21.
  4. Wayahudi waliruhusiwa kurudi wakati wa utawala wa Koreshi - 536 K.K. - Ezra 1:1 - 8.
  5. Walitawaliwa na Waajemi na Wayunani.
  6. Walikuwa huru na kuongozwa na Makabayo (Maccabees) kwa kipindi cha miaka 100.
  7. Walipigana upande wa Pompey chini ya utawala wa Kirumi mwaka 63. K.K.
- C. Familia ya Herode ilikuwa imepewa cheo cha ufalme (kiini macho) kwa ajili ya Israeli katika kipindi cha Agano Jipy.
1. Wakati wa utawala wa Wamakabayo, Waedom walishirikishwa katika Yuda na kujulikana kama Idumea.
  2. Mtu mmoja wa Idumea aliyejulikana kama Antipater alichaguliwa kiongozi wa Yuda - Warumi walimpa uongozi huo.
  3. Herode Mkuu, mwana wa Antipater aliongoza kati ya 37 K.K. na 4 K.K.
    - A. Alikuwa na maadui wengi pamoja na mionganoni mwa familia - walimwua.
    - B. Aliliongeza na kulipamba zaidi hekalu, Yn. 2:19,20; Mt. 24:1.
    - C. Aliamuru watoto wachanga wakiume wauawe kule Bethlehemu kwa sababu aliogopa kutokea mshindani - Mt. 2:16.
  4. Maherode wengine walijotajwa katika Agano Jipy.
    - A. Arkelao - mwana wa Herode Mkuu alitawala baada ya kifo cha babaye - Mt. 2:22.
    - B. Filipo - mwana wa Herode Mkuu, alijenga Kaisaria Filipi - Lk. 3:1; Mt. 16:13.
    - C. Herode (wa eneo la nne), pia aliitwa Antipa, aliamuru Yohana auwe - Mt. 14:1-12; Lk. 13:31,32; 23:6-12.
    - D. Herode Agripa I, mjukuu wa Herode Mkuu, aliamuru Yakobo auwe - Mdo. 12:1 - 3, 20 - 23.
    - E. Herode Agripa II, alijitokeza mbele ya Paulo - Mdo. 25:13 - 26:32.

### 3. KRISTO ALIKUJA UKAMILIFU WA WAKATI ULIPOFIKA.

- A. Nyakati za siasa zilikuwa sahihi.
1. Sehemu kubwa ya dunia ilikuwa chini ya serikali moja
  2. Usafiri ulikuwa rahisi na salama kuliko kipindi cho chote kabla yake.
  3. Sarafu ya aina moja ilitumika.
  4. Kwa muda karibu miaka 100 amani ilitawala.
- B. Utamaduni na lugha vilielekeana.
1. Lugha ya Kiyunani ilikuwa ni lugha ya himaya ya Kirumi.
  2. Agano la Kale lilikuwa limetafsiriwa katika lugha ya Kiyunani mjini Alexandria Misri katika karne ya tatu kabla ya Kristo (K.K.)
- C. Masuala ya jamii na maadili yalikuwa mabaya mno kiasi ambacho haja ya kutafuta jambo lingine jema ilitafutwa sana.
1. Makahaba walitumika kama makuhani katika mahekalu ya wapagani.
  2. Kutoa mimba na vitendo vya ulawiti vilikubaliwa kama kawaida - Rum. 1:18 - 32.
  3. Talaka ilikuwa ni jambo la kawaida.
    - A. Seneca aliandika kwamba baadhi ya wanawake walihesabu umri wao kwa idadi ya wanaume waliowahi kuwa nao.

- D. Maisha ya mwanadamu yaliwekwa katika hali ya chini.
  - 1. Kutoa mimba na kutelekez a watoto wachanga vilifanyika kama kawaida.
  - 2. Kujiua kulihesabiwa kuwa haki ya watu .
  - 3. Shughuli za michezo zilikuwa za kikatili za umwagaji damu na vurumai.
  - 4. Uuaji ulijulikana kama Euthanasia vilionekana ni jambo la kawaida.
  - 5. Utumwa ulikuwa wa kawaida kiasi kwamba mara nyingi watumwa walikuwa wengi zaidi kuliko waungwana.
- E. Dini za wote Warumi na Wayunani zilipoteza mvuto wake.
  - 1. Utupu uliachwa mionganoni mwa waumini.
- F. Uyahudi ulifanya mengi yaliyotayarisha ujio wa Kristo.
  - 1. Wayahudi walitawanyika duniani kote.
  - 2. Palipokuwa na Wayahudi kumi wanaume palikuwa na Sinagogi.
  - 3. Mungu mmoja na wa kweli alikwisha hubiriwa na watu walimtzamia Masihi.
  - 4. Dini ya Kiyahudi ilisitisiza viwango vya juu vya maadili.
  - 5. Watu wengi wa Mataifa (Gentiles) wakawa Wacha Mungu (Jewish Proselytes) - Mdo. 10:2.
  - 6. Sinagogi palikuwa ni mahali palipotayarisha chanzo cha uinjilisti. Mdo 13:5,14; 14:1; 17:1 - 4,10,17; 18:4.

**MWISHO:**

- 1. Ulimwengu ilitayarishwa na Mungu kwa ajili ya kuja Mwana wake - Gal. 4:4,5.
- 2. Hali ilikuwa mwafaka kwa uenezaji wa injili.

## **SOMO LA IV - MATHAYO - MFALME NA UFALME WAKE.**

### **UTANGULIZI:**

1. Mathayo ni katibu cha kwanza katika Agano Jipyा.
  - A. Kina sura 28.
  - B. Kina jumuisha maisha ya Kristo kuanzia kuzaliwa kwake hadi wakati wa kutoa Ujumbe Mkuu.
2. Kitabu kinachosomwa mara nyingi zaidi ya vitabu vingine vya Biblia.
3. Huunganisha pengo kati ya A.K. na A.J.
  - A. Mtu hawesi kulielewa Agano Jipyा kama hajui Agano la Kale.
    1. Wala mtu hawesi kulielewa Agano la Kale kama halijui Agano Jipyা.
  - B. Augustine alisema, “Agano la Kale ni Agano Jipyा katika kificho, Agano Jipyा ni Agano la Kale katika Kifunuo”.
  - C. Kati ya kipindi cha kumalizika kuandikwa kitabu cha Malaki na kipindi cha matukio ya Mathayo, kifunuo (ufunuo wa Neno) kilikuwa kimya kwa muda wa zaidi ya miaka 400.
  - D. Kitabu cha Mathayo kilielekezwa kwa Wayahudi.
  - E. Kinanukuu kiasi cha mara 65 kutoka katika Agano la Kale.
  - F. Kinaonyesha kwamba Yesu ni Masihi wa unabii katika Agano la Kale.
  - G. Kinafuatilia ukoo wa Yesu Kristo tangu Ibrahimu Mpaka Daudi.
    1. Kinaonesha Kristo alikuwa Myahudi halisi na Uzao wa ahadi ya Ibrahimu.
    2. Pia kinaonesha Kristo alikuwa mrithi wa kiti cha Israeli na mwana wa Daudi.
4. Katika maelezo ya maisha ya Kristo (katika vitabu vinne), Mathayo ni cha Kiyahudi zaidi ya vyote.
5. Si kitabu cha masimulizi ya hatua za maisha ya mtu tangu kuzaliwa.
  - A. Hakuna maelezo ya maumbile ya Kristo.
  - B. Sehemu kubwa zaidi ya maisha ya Kristo haijaelezwa.
    1. Mkazo Uko katika: kuzaliwa, kubatizwa, mafundisho, huduma, kifo na kufufuka.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIANDIKA KITABU CHA MATHAYO?**

- A. Wasomi wa hivi karibuni hupinga kwamba ndicho cha kwanza kuandikwa.
  1. Huzungumzia tatizo la “SYNOPTIC”.
    - A. SYNOPTIC - Kulitazama jambo kwa ujumla.
    - B. Mathayo, Marko na Luka hutajwa kuwa ni Injili za SYNOPTIC kwa sababu zinanukuu mambo yanayofanana.
  2. Jambo hilo, SYNOPTIC huleta hoja ya maelezo ya sehemu zinazotofautiana na kufanana katika masimulizi hayo.
  3. Nadharia iliyopo toka kwa wenyewe msimamo huria ni kwamba Marko ndicho kilichoandikwa kwanza katika injili.
    - A. Kuna maoni kwamba Marko aliandika kwa kutumia mkusanyiko wa semi za Yesu zilizopewa alama Q (kutokana na neno la Kiyunani Quelle - chanzo).
      1. Imeonekana kwa maoni kuwa Mathayo baadaye aliandika akitumia maandiko ya Marko na Q. Akifuatiwa na Luka, aliyetumia Mathayo, Marko na Q.
    - B. Hata hivyo, hizo semi ziiwazo “Q” hazina nukuu kuonesha kuwako kwake.
      1. Nadharia hiyo inaharibu uvuvio wa maneno ya mdomo ya Mathayo - 2 Tim. 3:16, 17.
    - C. Kufanana kumeelezwa kwa ukweli kwamba waandishi wote watatu waliandika kuhusu mtu mmoja na matukio yaliyoelezwa yalikuwa ya uvuvio wa yule yule Roho Mtakatifu.

- D. Tofauti imeelezwa na ukweli kwamba kila mwandishi aliandika kwa watu tofauti na wale walioandikiwa na mwandishi mwingine. Yakisisitizwa mambo yaliyokuwa muhimu kwa watu hao.
- B. Mathayo alikubaliwa na kanisa la awali kwamba ndiye mwandishi.
1. Irene (Irenaeus) aliyejifunza chini ya Polycarp na aliyemfahamu mtume Yohana alimkubali Mathayo kuwa ndiye mwandishi.
  2. Ingawa Mathayo hatajwi kitabuni kuwa mwandishi, inaonekana kuwa dhahiri ndiye aliyeandika.  
A. Hata hivyo, hata kama hakukiandika, umuhimu wa nani alikiandika si mkubwa.
- C. Mathayo alikuwa mtoza ushuru - Mt. 9:9; Mk. 2:14; Lk. 5:27, 28.
1. Anaweza kuwa alikuwa mionganoni mwa watoza ushuru na watenda dhambi ambao walivutiwa na mafundisho ya Yesu.
  2. Aliacha kila kitu pasipo kusita na kumfuata Yesu katika wito wake - Lk. 5:28, 27.
  3. Yamkini alikuwa na elimu ya kutosha, kwa sababu fani ya kazi yake ingehitaji hivyo.
  4. Pia yawezekana alikuwa mwenye mali nyingi.  
A. Alikuwa mtoza ushuru - Mt. 9:9.  
B. Alikuwa na nyumba - Mt. 9:10 - 13; Mk. 2:14 - 17; Lk. 5:29.  
C. Alikuwa na uwezo kifedha kutengeneza karamu kwa ajili ya Yesu - Lk. 5:29.
  5. Aliishi Kapernaumu Mathayo 9:1, 9; Marko 2:1.
  6. Alikuwa anaitwa Lawi mwana wa Alfayo - Mk. 2:14.
- D. Inafahamika kidogo sana kuhusu maisha yake baada ya Pentekoste.
1. Mara ya mwisho kutajwa katika Agano Jipyä ni Matendo 1:13.
  2. Kufuatana na maelezo ya wengine alihubiri mionganoni mwa Wayahudi kwa muda wa miaka 15 baada ya Pentekoste na kisha aliipeleka Injili Ashuru, Uajemi, Parthia, Mede na Ethiopia (Kushi).
  3. Maelezo ya mapokeo yanatofautiana kuhusu kifo chake.  
A. Wengine hudai alikuwa kwa kifo cha kutetea imani.  
B. Wengine kama Socrates wanadai, Mathayo alifariki akihubiri Ethiopia, kifo cha kawaida.

## 2. LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA?

- A. Mapema (Wakristo wa awali) wanadai Mathayo alikuwa wa kwanza kuandika maisha ya Kristo.
1. Tarehe hutofautiana.
    - A. Wengine husema mapema kiasi cha 37 A.D.
    - B. Irene anadai kitabu cha Mathayo kiliandikwa wakati Petro na Paulo wako Rumi kuhubiri.
      1. Hata hivyo, hakuna ushahidi kwamba Petro aliwhali kuwa Rumi.
    - C. Dhahiri, kiliandikwa kabla ya 70 A.D. kwa sababu kinabashiri kuharibiwa (kuteketezwa) kwa Yerusalemu katika Mathayo 24.
    - D. Ni dhahiri kuna ushahidi wa milele kuhusu muda kupita kati ya wakati wa tukio lenyewe na wakati wa kurekodi tukio hilo - Mt. 27:8; 28:15.
- B. Baadhi ya waandishi wa kale wamesema kwamba Mathayo kiliandikwa kwanza katika Kiebrania na akakitafsiri katika Kiyunani.
1. Hata hivyo, ndani ya kitabu hakuna ushahidi unaoonesha ukweli huo.
    - A. Lughya ya Kiyunani ilikuwa imeenea Palestina.
    - B. Hakuna nakala za kumbukumbu za Kiebrania katika Mathayo zilizowahi kupatikana.
    - C. Hilo linaleta hoja nyingine ya kwa nini Mathayo angehitaji kutafsiri semi fulani za Kiebrania kama kitabu kizima ni tafsiri ya kutoka Kiebrania kuwa katika Kiyunani.
      1. Taz. Mat. 1:23; 27:33; 27:46.
      2. Kwa sababu yaonekana kitabu kiliandikwa kwa lengo la kueneza habari kwa sehemu kubwa, uwezekano ni mkubwa kwamba kiliandikwa katika lugha ya Kiyunani cha kawaida.
- C. Mahali kilipoandikwa hapajajulikana

1. Labda Yerusalem au Uyahudi.

### 3. KWA NINI KITABU CHA MATHAYO KILIANDIKWA?

- A. Ni ujumbe wa Mfalme na Ufalme wake.
  - 1. Usemi - “Ufalme wa mbinguni” hupatikana mara 33.
  - 2. “Ufalme wa Mungu” mara nne.
  - 3. Yesu kutajwa kama mwana wa Daudi mara 9.
- B. Yesu amejulikana na kuoneshwa kuwa utimilifu wa unabii wa A.K. wa Masihi.
  - 1. Usemi wa “ili litimie” hutokea mara nyingi Mt. 1:27; 2:23; 4:14; 8:17; 12:17; 13:35; 21:4; 27:9.
  - 2. Kinarekodi kukiri kwa Petro Mt. 16:16.
- C. Haja ya ushuhuda wa uvuvio wenyewe nguvu wa maisha ya Kristo kutimizwa.
  - 1. Ukristo ulikuwa unaenea kwa kasi.
  - 2. Wale waliomwona Yesu walikuwa wanapita.
  - 3. Hadithi nyingi zilizo za kweli zilikuwa zinaenezwa Lk. 1:1.

### 4. KITABU ALIANDIKIWA NANI?

- A. Kila maelezo ya kila kitabu cha Injili yaliandi kwa kwa watu tofauti:
  - 1. Mathayo - kwa Wayahudi.
  - 2. Marko - Warumi.
  - 3. Luka - kwa Wayunani (Wamataifa).
  - 4. Yohana - kwa Wote.

### 5. MUHTASARI WA MATHAYO

- A. Kimeandikwa kwa mfuatano wa wakati na mada.
  - 1. Sura 1 - 4 ni mfuatano wa wakati.
    - A. Kuzaliwa
    - B. Safari Misri
    - C. Huduma ya Yohana.
    - D. Ubatizo wa Yesu.
    - E. Majaribu ya Yesu.
    - F. Mwanzo wa huduma ya Yesu.
  - 2. Sura ya 20 hadi 28 ni mfuatano wa wakati.
- B. Mpangilio wa mada katika sehemu za Mathayo.
  - 1. Maelezo sita ya kumbukumbu za Yesu:
    - A. Mahubiri ya mlimani - sura ya 5 - 7.
    - B. Miujiza - sura ya 8 na 9.
    - C. Ujumbe (Maagizo) sehemu maalum - sura ya 10.
    - D. Mifano kuhusu ufalme - sura ya 13.
    - E. Maelekezo kuhusu unyenyekevu na msamaha - sura ya 18.
    - F. Shutuma dhidi ya Waandishi na Mafarisayo - sura ya 23.
    - G. Maelekezo kwenye mlima wa mizeituni - sura ya 24 na 25.

### MWISHO:

1. Ukweli unaovuta (unaohamasisha):
  - A. Mathayo maana yake “zawadi ya Mungu”

- B. Kufuatana na maelezo ya Eusebius kitabu cha Mathayo, kilijuli kana India katika karne ya pili.
- C. Neno “kanisa” limetumika mara tatu.
- D. Mifano kumi - na - tano inapatikana katika kitabu cha Mathayo.
  - 1. Kumi kati ya ke haipatikani po pote penginepo katika Agano Jipy.
- E. Miujiza ishirini inapatikana katika Mathayo.
  - 1. Mitatu kati yake haipatikani penginepo katika Agano Jipy.

## **SOMO LA V - MARKO MTUMISHI WA YEHOVA.**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu cha pili cha A.J. ni Marko, maelezo ya maisha ya Kristo.
  - A. Kina sura 16.
  - B. Kifupi kuliko vyote katika maelezo ya injili.
2. Marko ni maelezo yenye mwendo wa kasi katika kuonesha huduma ya Yesu.
  - A. Hutumia maneno: “mara (moja)” “mara”, “kwa kasi” mara 41.
  - B. Htuonesha jinsi Kristo alivyokuwa na shughuli nyingi katika huduma yake.
3. Inaaminiwa kwamba Marko aliandika maelezo ya maisha ya Kristo aliposikia yakielezwa katika Mahubiri ya Petro.
  - A. Jina lake kamili ni Yohana Marko - Mdo. 12:12.
  - B. Alikuwa mfuasi wa Petro katika miaka ya baadaye ya Petro. - 1 Pet. 5:13.
  - C. Papias, Mkristo, aliandika mapema katika karne ya 2, “Marko alipokuwa mkalimani wa Petro, aliandika kwa usahihii kila kitu alichokumbuka ingawa sio katika mpangilio wa kile alichokisema au kufanya Yesu Kristo....”.
  - D. Irene (Irenaeus) alisema katika sehemu ya mwisho ya karne ya pili,..... Marko, mkalimani na mwanafunzi wa Petro, aliweza kutupatia katika maandishi kile kilichohubiriwa na Petro.

### **MJADALA:**

1. **NI NANI ALIANDIKA KITABU CHA MARKO?**
  - A. Waandishi wa mwanzo kwa pamoja wanamkulali Marko kama ndiye mwandishi.
    1. Papias, Justin Martyr, Tertullian na Irene wa karne ya pili.
    2. Origen wa karne ya tatu.
    3. Eusebius katika karne ya nne.
  - B. Marko aliкуwa na sifa kamili kuandika juu ya maisha ya Kristo.
    1. Alikuwa ni mwana wa Mariamu ambaye nyumba yake palikuwa mahali pa kukutania kanisa la awali - Mdo 12:12.
      - A. Inaaminiwa kwamba chumba cha juu ambako Yesu alikula chakula cha mwisho na ambacho wanafunzi walikutana baada ya Yesu kupaa, kilikuwa nyumbani mwa Mariamu - Marko 14:12 - 26; Mdo. 1:13.
      - B. Ni Marko pekee anayeandika kuhusu kijana aliyemfata Yesu alipokamatwa Mk. 14:51, 52.
        1. Wengi wanaamini huyo kijana alikuwa Marko.
    2. Marko aliкуwa ama binamu au mpwa wake Barnaba Kol. 4:10.
    3. Angeweza kuwafahamu mitume wote kwa sababu ya kukutania nyumbani mwa mamaye.
    4. Aliongozana na Paulo na Barnaba katika safari yao ya kwanza ya umisionari - Mdo. 13:4 - 13.
      - A. Hakuimaliza safari, bali alirudi walipofika Pamfilia.
      - B. Paulo alikataa kumchukua Marko katika safari ya pili ya umisionari - Mdo. 15:36 - 41.
        1. Hilo lilipelekea utengano kati ya Paulo na Barnaba.
          - A. Paulo alimchukua Sila na kwenda Ashuru (Syria) na Kilikia.
          - B. Barnaba akamchukua Marko na kwenda Kipro.
          - C. Baadaye Paulo alimtaja Marko katika hali ya uzuri, hiyo ikioneshwa kwamba walisuluhishana baadaye. 2 Tim. 4:11.

5. Marko alisafiri na Petro aliyejkuwa “baba” yake katika imani - 1 Pet. 5:13.

## 2. LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA?

- A. Dhahiri kiliandikwa kabla ya 70 A.D. kwa sababu ya utabiri wake wa maangamizi ya Yerusalem - Mk. 13.
  - 1. Wasomi wenyewe msimamo wa kushikilia taratibu hutaja tarehe za kitabu kati ya 56 A.D. NA 66 B.K.
- B. Mapokeo hudai huenda kiliandikwa Rumi, nchini Italia.
  - 1. Marko alikuwa Rumi wakati wa ufungwa wa Paulo wa mara ya Kwanza - Kol. 4:10.
  - 2. Baadaye aliiwa Rumi kwa Paulo wakati wa ufungwa wa Paulo wa mara ya pili - 2 Tim. 4:11.

## 3. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA NA KWA NANI?

- A. Mathayo alisisitiza alichofundisha Yesu, wakati Marko alisisitiza alichokifanya Yesu.
- B. Marko aliandika akiwa na taswira ya Warumi mawazoni.
- C. Kitabu chake hutofautiana na kile cha Mathayo na Luka.
  - 1. Marko ameruka maelezo ya ukoo wa Yesu.
  - 2. Hajataja kuzaliwa na maisha ya utoto wa Yesu.
  - 3. Ghafula anaanza na huduma ya Yohana Mbatizaji.
  - 4. Haandiki baadhi ya masimulizi makuu ya Yesu kama Mahubiri ya Mlimani, shutuma dhidi ya waandishi na Mafarisayo na mifano ya ujio wa mara ya pili kama ionekanavyo Mt. 25.
  - 5. Anatoa nafasi ndogo kwa mifano na kuweka nafasi kubwa kwa Miujiza.
  - 6. Anamweka Yesu katika hali ya mtumishi wa Yehova, ambapo Mathayo anamweka Yesu katika nafasi ya Masihi na Mfalme wa Wayahudi.

## 4. MUHTASARI WA MARKO.

- A. Matukio yanayojifungua katika maisha ya Yesu hadharani - 1:1 - 13.
- B. Utumishi wa Yesu kule Galilaya - 1:14 - 9:50.
- C. Safari ya Yesu Yerusalem - 10:1 - 52.
- D. Juma la mwisho la Yesu - 11:1 - 15:47.
- E. Ufufuo na kutolewa kwa Agizo kuu - 16:1 - 20.

## 5. JE, MARKO 16:9 - 20 NI SEHEMU YA NENO LA UVUVIO?

- A. Wenyewe msimamo huria hudai sehemu hiyo ya maandiko ingefaa iondolewe.
  - 1. Tafsiri zote za kisasa za Kiingereza huiruka sehemu hiyo, isipokuwa New King James Version. Hata hivyo, huyaweka maandiko hayo kwenye kumbukumbu za chini ya ukurasa.
  - 2. Sio suala la mafundisho, bali suala ni maelezo hayo yaliandikwa na Marko au mtu mwengine aliongeza baadaye.
  - 3. Maelezo hayo hayapatikani katika sehemu ndogo ya Maandiko ya mkono ya awali.
    - A. Hayapatikani kutoka yale ya Sinai na Maandiko ya Vatican (ya mkono).
    - B. Jerome na wengineo wa karne ya nne huonesha maandiko hayo hawakuwa nayo katika baadhi ya Maandiko hayo ya awali ya mkono wakati wao.
- B. Hata hivyo, ushahidi ni mkubwa kuwa maelezo hayo yanastahili kuwa sehemu ya maelekezo matakatifu (Canon).
  - 1. Yapo katika maandiko mengi pamoja na yale ya Alexandria.
  - 2. Yalinukuliwa wakati wa waandishi wa karne ya 2 na ya 3 hali inayoonesha yalikuwa sehemu ya

Agano Jipyka kabla ya nyakati za yale ya Sinai na Maandiko ya awali ya mkono ya Vatikani (Vatican Manuscripts).

- A. Irene alinukuu Marko 16:19 katika karne ya 2.
- C. Maandiko ya tafsiri za zamani yaliyofanywa kutoka maandiko ya awali ya mkono ya kabla ya yale ya Sinai na Vatican, yalikuwa na maelezo hayo.

#### **MWISHO:**

1. Kitabu cha Marko ki wazi zaidi kuliko vitabu vingine vya waandishi wa injili.
  - A. Katika Marko 1:12,13, anafafanua zaidi kuliko wengine.
  - B. Katika Marko 6:39 ni mwandishi huyo tu anayeonesha kukaa alikoagiza Yesu penye “majani mabichi”.
2. Marko ananukuu toka Agano la Kale mara moja tu.
  - A. Ananukuu mara 19 kwamba Yesu alinukuu toka Agano la Kale.
3. Eusebius alisema kwamba Marko alianzisha kanisa Alexandria, Misri.
4. Marko aliandika kuthibitisha kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na Mwokozi wa mwanadamu.

## **SOMO LA VI - LUKA - YESU MTU MKAMILIFU.**

### **UTANGULIZI:**

1. Cha tatu katika vitabu vya Agano Jipyä ni maelezo ya Luka kwa ajili ya maisha ya Kristo.
  - A. Kina sura 24.
  - B. Ndicho kirefu zaidi katika maelezo ya vitabu vya injili, na cha pili kwa urefu katika Agano Jipyä.
2. Kimetajwa kuwa ni kitabu kilichoandikwa katika hali inayopendeza zaidi ya vitabu vingine viliviyowahi kuandikwa.
  - A. Kufuatana na wasomi wa Kiyunani Luka na Matendo ni vitabu vilivyoandikwa katika Kiyunani kinachopendeza zaidi ya vingine vyote katika Agano Jipyä.
3. Ni cha kawanza katika viwili vya Kristo na Kanisa lake vilivyoandikwa na Luka.
  - A. Kitabu cha pili ni Matendo, Mdo. 1:1.
  - B. Matendo ni maendelezo ya yale aliyoyatenda Yesu na kufundisha kwa njia ya wawakilishi wavuviwa duniani.

### **MJADALA:**

#### **1. NI NANI ALIYEKIANDIKA KITABU?**

- A. Kitabu hakitaji aliyekiyeandika.
- B. Ushuhuda wa wote wa kanisa la awali ni kwamba Luka alikuwa ndiye mwandishi.
  1. Clement wa Rumi alinukulu kutoka Luka mnamo 95 B. K.
  2. Agano la Mababa Kumi - na - wawili lililoandikwa kati ya 100 - 120 B. K. lilinukulu kiasi kikubwa kutoka Luka.
  3. Mnamo katikati ya karne ya pili Heracleon aliandika muhtasari kuhusu kitabu cha Luka.
  4. Katikati ya karne ya pili Justin Martyr alinukuu kutoka kitabu cha Luka kiasi cha mara 70.
  5. “Injili ya Luka inasimama katika nafasi ya tatu ikiwa imeandikwa na Luka, tabibu, mfuasi wa Paulo, ambaye, akiwa si shahidi wa kuona, alitumia masimulizi yake kutokana na habari alizozipata kuanzia kuzaliwa kwa Yohana”.
  6. Mnamo 180 A.D. Irene (Irenaeus) aliandi ka kwamba Luka, “Alinukuu katika kitabu Injili iliyohubiriwa na Paulo”.
  7. Mwishoni mwa karne ya pili na mapema katika karne ya tatu, Clement wa Alexandria na Tertullian walinukuu kutoka kitabu cha Luka na kuonesha uthibitisho wa uandishi wa Luka.
- C. Kwa jina Luka anatajwa mara tatu tu katika Agano Jipyä.
  1. Kolosai 4:14.
    - A. Luka anapambanuliwa nje ya wengine, “waliokuwa watohara”.
    1. Inaonesha Luka hakuwa Myahudi.
    - B. Luka alikuwa Rumi wakati wa kifungo cha kwanza cha Paulo.
    - C. Luka alikuwa mganga (tabibu).
  2. Filemoni 2:4
    - A. Wakati wa kifungo cha pili cha Paulo.
    - B. Paulo yawezekana aliuawa mara baada ya wakati huo - 2 Tim. 4:6-8.
- D. Luka aliandika kitabu cha Luka na cha Matendo.
  1. Vyote vimeandikwa kwa mtu mmoja - Thiofilo - Lk. 1:3; Mdo. 1:1.
  2. Matendo sura ya kwanza kinaanza pale Luka sura ya 24 kinapokomea.
  3. Vitabu vyote viwili vina mtindo mmoja wa Kiyunani.

4. Vyote viwili vina msamiati wa kiganga.
- E. Luka alikuwa na nafasi nzuri kuandika maisha ya Kristo.
1. Alisafiri na Paulo katika safari yake ya pili na ya tatu ya umisionari.
    - A. Alikutana na msafara wa Paulo kule Troa, Mdo. 16:10.
    - B. Alikwenda na Paulo Filipi, Mdo. 16:40.
      1. Yaelekea Luka alibaki Filipi wakati wengine waliendelea.
    - C. Aliunganika na kundi la Paulo katika safari yake (Paulo) ya tatu ya umisionari - Mdo. 20:5.
    - D. Katika sehemu za maandiko ya Matendo katika nafsi ya kwanza uwingi ("sisi"..... "tu") zaonesha kuwako kwa Luka.
  2. Alikuwa na Paulo wakati Paulo anafungwa Kaisaria.
    - A. Yawezekana aliitumia miaka hiyo miwili kuweza kuwazoea mama na ndugu wa Yesu na mashahidi wengine walioona kwa macho maisha ya Kristo.
    - B. Aliongozana na Paulo kwenda Rumi - Mdo. 21:1 - 28:16.
- F. Luka alikuwa ni mwana - historia wa kwanza wa kanisa.
1. Ni mwandishi pekee wa Agano Jipy aayewataja wafalme na maafisa wengine wa Kirumi kwa majina.
  2. Anataja matukio mengi ambayo yanaweza kuthibitika kihistoria.
  3. Watu wa msimamo huria hudai kuwa kuna masuala aliyokosea katika ukweli wa jambo.
    - A. Wanadai kuwa Augusto hakuitisha kufanyika hesabu ya watu kama ilivyosemwa katika Lk. 2:1.
      1. Sasa inafahamika kuwa hesabu hiyo ilifanyika kila miaka 14 ipitapo.
    - B. Wanapinga kuwa Kirenio alikuwa liwali wa Shamu alipozaliwa Yesu.
      1. Sasa imejulikana alitumikia awamu mbili.
- G. Kweli zinazohamasisha kuhusu Luka
1. Eusebius anadai Luka alikuwa mwenyeji wa Antiokia ya Shamu.
  2. Anaweza kuwa alipata elimu yake ya uganga kwenye chuo cha Uganga cha Antiokia ya Shamu - Mdo. 11:13.
  3. Ndiye pekee ambaye hakuwa Myahudi aliyeandika kitabu cha Biblia.

## 2. KILIANDIKWA LINI NA WAPI?

- A. Vyote viwili vimeandikwa kwa Thiofilo.
1. Thiofilo maana yake MPENDA MUNGU.
  2. Yawezekana lilikuwa jina halisi la mtu.
  3. Yawezekana lilikuwa ni jina lililowakil isha wampendao Mungu wote.
- B. Dhahiri kiliandikwa kabla Matendo hakijaandikwa.
1. Matendo yawezekana kiliandikwa Rumi wakati Paulo akiwa kifungoni.
  2. Hiyo ingemaanisha kuwa Mnamo 63 B.K.
  3. Yawezekana kitabu hicho kiliandikwa wakati Paulo akiwa kifungoni Kaisaria mnamo 61 B.K.

## 3. KWA NINI KILIANDIKWA NA KWA NANI?

- A. Kila mwandishi aliandika kwa watu maalum.
1. Mathayo - Wayahudi.
  2. Marko - Warumi.
  3. Luka - Wayunani.
  4. Yohana - Kwa wote.
- B. Wayunani walitafuta kumpata mtu mkamilifu.
1. Luka anaandika kuonesha kuwa mtu huyo ni Kristo.

2. Wayahudi na Warumi walikuwa na mtazamo wa kipekee, ambapo Wayunani walikuwa na mtazamo wa kiujuimla.
3. Luka anamweka Kristo kama mtu wa Wote wa Wayunani.
  - A. Mathayo anamweka Kristo kama Masihi wa Kiyahudi.
  - B. Marko anamweka Kristo kama Mtu wa Matendo.
- C. Msisitizo umewekwa kwamba Kristo ni Mwokozi wa ulmwengu wote, sio wa Wayahudi.
  1. Simoni alisema, "Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa" - Lk. 2:32.
  2. Luka anafuatilia ukoo kurudi kwa Adamu - Lk. 3:38.
  3. Mwandishi pekee aliyemtaja mjane Sarepta na Naamani wa Shamu - Lk. 4:25 - 27.
  4. Ni mwandishi pekee anayenkuu mfano wa Msamaria mwema - Lk. 10:25 - 37.
  5. Ni mwandishi pekee anayenkuu kuhusu Msamaria aliyerudi kutoa shukurani kwa kuponywa Lk. 17:12 - 17.
  6. Ni mwandishi pekee anayenkuu yaliyosemwa katika Isa. 40:5 "Wenye mwili wote watauona wokovu wa Mungu" Lk. 3:6.
- D. Mkazo wake Upendo wa Kristo kwa waliopotea
  1. Nyumbani mwa Zakayo - Lk. 19:1 - 10.
  2. Mifano ambayo Luka peke yake ndiye anayenkuu:
    - A. Kondoo aliyepotea - Lk. 15:1 - 7.
    - B. Shilingi iliyopotea - Lk. 15:8 - 10.
    - C. Mwana mpotevu - Lk. 15:11 - 24.
    - D. Ndugu aliye mkubwa aliyepotea - Lk. 15:25 - 32.

#### 4. MUHTASARI WA LUKA:

- A. Utangulizi - 1:1 - 4.
- B. Utoto uchanga na utoto wa Yohana na Yesu - 1:5 - 2:52.
- C. Kuanza kwa utumishi wa Kristo - 3:1 - 4: 13
- D. Mafundisho ya Galilaya - 4:14 - 9:6.
- E. Kujitenga toka Galilaya - 9:7 - 50.
- F. Mafundisho ya baadaye ya Uyahudi na Perea - 9:51 - 19:28.
- G. Kufungwa kwa huduma ya hadhara Yerusalem - 19:29 - 21:38.
- H. Mateso na kifo cha Yesu - 22, 23.

#### 5. MASOMO KUTOKA LUKA KWA AJILI YETU KUJIFUNZA

- A. Maisha huanza wakati uzao unapoanzishwa.
  1. Roho Mtakatifu alimjaa Yohana tangu tumboni mwa mamaye - Lk. 1:15.
  2. Tumboni mwa Elizabeth, katika mwezi wa 6 wa ujauzito wake, Yohana "Aliruka kwa furaha" - Lk. 1:26, 41, 44.
- B. Hupinga utaratibu wa kanisa la Katoliki wa kumwabudu Mariamu.
  1. Wakatoliki wanamwita Mariamu "Mama wa Mungu" na mpatanishi.
  2. Yesu alifundisha kwamba ye yote asikiaye na kutimiza mapenzi yake ana haki ile ile kama aliyonayo Mariamu mbele ya Yeye - Lk. 8:18 - 21;11:27,28.
    - A. Kumbuka pia 1 Tim. 2:5 uone nani mpatanishi wetu.
- C. Maelezo ya Luka yanawapa wanawake sifa kwa kutimiza yale waliyokabidhiwa na Mungu.
  1. Elizabeth - mama wa mtayarishaji mapito ya Yesu - Lk. 1:5 - 25.
  2. Mariamu - akawa mama wa Mwana wa Mungu - Lk. 1:26 - 38.
  3. Ana - alizungumza kuhusu Yesu - Lk. 2:36 - 38.

4. Mariamu Magdalene, Yoana na Susana walimfuata Yesu na kumsaidia katika huduma kimahitaji Lk. 8:3.
  5. Mariamu na Martha walimwonyeshea Yesu ukarimu nyumbani mwao - Lk. 10:38 - 42.
  6. Wanawake walikuwepo kwenye kifo na mazishi ya Yesu - Lk. 23:49, 55.
  7. Wanawake walikuwa wa kwanza kumwona yesu baada ya kufufuka kwake - Lk. 24:1 - 10.
- D. Anahimiza umuhimu wa sala.
1. Hunukulu mafundisho mengi ya Yesu juu ya sala ambayo hayajarekodiwa penginepo.
  2. Huonesha Yesu aliomba (-sali) pia nyakati ngumu katika maisha yake:
    - A. Ubatizo wake - 3:21.
    - B. Kabla ya kuwachagua mitume - 6:12 - 16.
    - C. Kiri kuu - 9:18 - 20.
    - D. Kugeuka kwa sura ya uso wa Yesu - Lk. 9:28 - 36.
  3. Ni mwandishi pekee aliyenukuu sala ya Yesu ya kuwaombea wauaji (waliomwua) wake - Lk. 23:34.
- E. Anasisitiza umuhimu wa toba.
1. Anatumia neno “tubu” na yale yahusianayo na neno hilo mara 15 - 13:1; 15:7,10,17 - 20; 19:1 - 9; 23:39 - 43.

### **MWISHO:**

1. Kitabu kina habari nyingi ambayo haipatikani katika Mathayo, Marko au Yohana.
  - A. Kuzaliwa kwa Yesu.
  - B. Ziara ya Yesu hekaluni akiwa na umri wa miaka 12.
  - C. Mifano ya Msamaria Mwema, Mwana Mpotevu na wengineo.
  - D. Maelezo ya tajiri na Lazaro na mwizi msalabani.

## **SOMO LA VII - YOHANA - YESU MTU WA WOTE.**

### **UTANGULIZI**

1. Katika vitabu vinne vinavyoolezea kwa nyakati maisha ya Kristo, imesemwa kwamba:
  - A. Mathayo kiliandikwa kwa Wayahudi na kumwonesha Mfalme na Ufalme wake.
  - B. Marko kiliandikwa kwa Warumi na kumwonesha Yesu kama mtumishi wa Yehova, mtu wa vitendo.
  - C. Luka kiliandikwa kwa Wayunan i na kumwonesha Yesu kama Mtu aliye mkamilifu.
  - D. Yohana kiliandikwa kwa watu wote na kumwonesha Kristo kama Mungu aliyekuwa katika mwili aliye wa wote.
2. Kitabu cha Yohana kinatofautiana kiasi kikubwa na vile vitabu vingine vitatu.
  - A. Vingine viko katika uelezeaji wa maisha ya mtu zaidi.
  - B. Yohana anaonesha silika ya Kristo.
  - C. Kitabu cha Yohana kiliandikwa miaka mingi baadaye kuliko vingine.
    1. Kusingekuwa na haja kwa Yeye kuandika kitabu wakati huo wa baadaye kama ambalo angefanya ni kurudia walichosema wenzake.
  - D. Anaacha maelezo mengi yanayopatikana katika vitabu vingine vitatu:
    1. Ukoo, kuzaliwa, utoto, ubatizo, majoribu, Mahubiri ya mlimani n.k.
  - E. Anaingiza mengi ambayo katika vitabu vingine vitatu hayamo.
    1. Mujiza wa Kana, habari ya Nikodem, habari ya mwanamke kisimani, mfano wa mchungaji mwema, kumfufua Lazaro, kuosha miguu ya wanafunzi, sala ya Bwana kwa ajili ya umoja, na matukio ya Tomaso.
3. Kitabu hicho kimeitwa, “kitakatifu cha vitakatifu” katika Agano Jipy.

### **MJADALA:**

1. **NI NANI ALIYEANDIKA KITABU?**
  - A. Wapinzani wanajaribu kukipa tarehe za baadaye sana ili kupunguza hadhi ya uandishi wake.
    1. Kama ingeoneshwa kwamba vitabu viliandikwa karne ya pili, au baadaye, ingeondoa uwandishi wa watu wa awali na kushusha hadhi ya Agano Jipy lote.
    2. Sasa tunazo sehemu za kitabu cha Yohana ambazo tarehe zake zinakuwa katika miaka 25 ya maisha yake, ikipingana na madai ya wapinzani.
  - B. Ushahidi wa ndani unatetea uandishi wa Yohana.
    1. Mwandishi alikuwa na uzoefu wa watu, mahali na desturi za Palestina, hali iliyoonesha kwamba lazima atakuwa alikuwa Myahudi aliyeishi kule.
    2. Dondoo nyingi zaidi kutoka Agano la Kale, zinatoka katika Kiebrania, ambacho ni Mpalestina wa Kiyahudi (Myahudi wa Palestina), kama Yohana, ambaye angeweza kufanya hivyo.
    3. Maelezo ya binafsi ya undani na uchambuzi wa karibu unaopatikana katika kitabu hicho unaonesha kiliandikwa na mtu aliyekuwa karibu na Yesu, kama alivyokuwa Yohana.
  - C. Mitume watatu walikuwa karibu sana na Yesu - Petro, Yakobo na Yohana - Mk. 5:35 - 43; Mt. 17:1 - 9; 26:36, 37.
    1. Yakobo aliuawa kwa kukatwa kichwa, siku za kwanza za kanisa, hali ambayo inamwondoa kuwa ndiye mwandishi. Mdo. 12:12.
    2. Kama tulivyoona kitabu cha Marko kinayo mahubiri ya Petro, kwa hiyo hakuna haja ya historia nyingine kutoka katika msimamo wa Petro.
    3. Hiyo inamaanisha Yohana peke yake.
  - D. Ushahidi wa nje unaonesha Yohana ndiye mwandishi.

1. Justin Martyr, karibu 150 A.D. anaonesha Yohana ndiye mwandishi.
2. Muratorian Canon, karibu 170 A.D. pia huthibitisha kwamba Yohana ndiye mwandishi.
3. Irene, karibu na 180, aliandika kwamba Polycarp, aliye kuwa rafiki wa Yohana, humpa sifa Yohana kuwa ndiye mwandishi.
- E. Yohana alikuwa na sifa ya kutosha kuandika maelezo ya maisha ya Kristo.
  1. Alikuwa kaka wa Yakobo mwana wa Zebedayo na Salome - Mt. 4:21; 20:20, 21; 27:56; Mk. 15:40, 41.
  2. Yawezekana alikuwa ni mdogo kwa Yakobo kwa vile daima alitajwa katika nafasi ya pili. Mt. 4:21; 10:2; 17:1; Mk. 1:29; 10:35.
  3. Alikuwa mshiriki katika shughuli za uvuvi na baba yake, ndugu na Petro na Andrea. Lk. 5:10.
  4. Salome anajulikana kuwa alikuwa mmoja wa wanawake waliomfuata Yesu na kumpa msaada ulipohitajika katika kazi yake - Mk. 16:1; Lk. 8:2, 3; 24:10.
  5. Alikuwa ni mmoja wa mitume wa kwanza na alifurahia ukaribu maalumu na Yesu.
    - A. Alikuwa ni "mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda" Yn. 13:23; 19:26; 21:20; Mt. 17:1; Mk. 5:37.
  6. Kabla ya kifo chake Yesu aliamuru Yohana amtunze mamaye (Yesu) - Yn. 9:25 - 27.
  7. Yohana na Petro walifanya kazi kwa ukaribu wa pamoja - Luka 22:8; Yn. 20:2 - 10; Mdo. 4:13 - 22; 8:14.
  8. Alikuwa ni mwanafunzi ambaye Yesu alimwita "mwana wa ngurumo," lakini aligeuka kuwa mtume wa upendo Mk. 3:16, 17; 9:38 - 40; Lk. 9:51 - 56.
  9. Alikuwa mmoja wa viongozi wa Yerusalem - Gal. 2:9.
  10. Historia inaonesha alibaki Yerusalem hadi kifo cha mama wa Yesu.
  11. Historia inasema kwamba alitumia miaka yake iliyobaki Efeso.
    - A. Kufuatia kuharibiwa kwa Yerusalem, Efeso uligeuka kuwa kitovu cha Ukristo.
    - B. Alipelekwa uhamishoni kisiwa cha Patmo wakati wa utawala wa mfalme Domitian - Ufu. 1:9.
    - C. Alikufa wakati wa utawala wa mfalme Trajan mnamo mwaka 100 A.D. na alizikwa Efeso.

## 2. KILIANDIKWA LINI NA WAPI?

- A. Yohana alikuwa mwandishi wa tatu kufuatia Luka na Paulo.
  1. Aliandika nyaraka Yoh. 1,2,3; Yohana na Ufunuo.
- B. Ushahidi unaonesha kitabu cha Yohana inawezekana kiliandikwa Efeso karibu na mwisho wa karne ya 1.
  1. "Mwisho wa yote, akiona kwamba katika Injili mambo yale yalikuwa ameelezewa, yaliyohusu mwili, akishauriwa na marafiki zake na kuvutwa na Roho wa Mungu akaandika Injili ya kiroho" - Clement wa Alexandria aliandika kiasi cha miaka 100 baada ya kifo cha Yohana.
  2. Irene aliandika kwamba Yohana aliandika kuhusu maisha ya Kristo kiasi cha miaka 60 ya kupaa kwa Kristo.
    - A. Pia alitaja kwamba Yohana aliandika baada ya kifo cha Domitian kufuatia kurejea kwake toka Patmo.
    - B. Alihusisha maelezo ya Yohana kama ni maelezo ya mwisho katika awamu nne za maelezo ya maisha ya Kristo.
  3. Kwenda uhamishoni kwa Yohana kuko katika sehemu ya mwisho ya utawala wa Domitian.
    - A. Domitian alikufa mwaka 96 A.D.
    - B. Kitabu cha Yohana kiliandikwa baada ya uhamisho kwenda Patmo.
    - C. Hivyo, hiyo ingekiweka kitabu hicho mnamo 97 na 98 A.D.

## 3. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?

A. Kusisitiza uungu wa Kristo.

1. Miujiza mikubwa minane imenorodheshwa na Yohana kuthibitisha uungu huo.
  - A. Maji kuwa divai - 2:1 - 11.
  - B. Uponyaji wa mbali wa mtoto wa diwani - 4:46 - 54.
  - C. Watu 5000 kulishwa - 6:1 - 13.
  - D. Yesu atembea juu ya maji - 6:16 - 21.
  - E. Mtu aliyezaliwa haoni (kipofu) - aponywa 9:1 - 7.
  - F. Lazaro kufufuliwa toka wafu - 11:1 - 46.
  - G. Kufufuka - 20:30, 31.
  - H. Uvuvi mkuu wa samaki - 21:1 - 8.
- B. Yohana hanukuu cho chote katika miaka 30 ya kwanza ya Yesu Kristo.
- C. Lengo lilikuwa ni kuongezea yale ambayo tayari yalikwisha andikwa na Mathayo, Marko na Luka.

#### 4. MUHTASARI WA YOHANA

- A. Neno ni la milele - 1:1 - 5 Neno ni milele (hapo anahusishwa kuwa neno ni Yesu)
- B. Neno likawa mwili - 1:6 - 18.
- C. Neno lilifunuliwa kwa Israeli - 1:19 - 12:50
- D. Neno lilifunuliwa kwa wanafunzi - 13:1 - 17:26
- E. Neno alisulubiwa kwa ajili ya dhambi za watu - 18:1 - 19:42.
- F. Neno akafufuka kwa wafu - 20:1 - 13.
- G. Neno akathibitishwa kwa wanafunzi baada ya kufufuka - 21:1 - 25.

#### 5. MASOMO KUTOKA YOHANA KWA AJILI YETU LEO.

- A. Kristo ni Mungu mwumbaji, ni mmoja wa nafsi tatu za Uungu - Yn. 1:1 - 3, 14; 20:24 - 28.
  - B. Pamoja na madai ya Wakatoliki, Kristo hakufanya miujiza kabla ya Kana - Yn. 2:11
  - C. Alama ya uwanafunzi (wa Kristo) ni upendo. Yn. 13:34,35.
  - D. Roho Mtakatifu alitumwa ili kuongoza katika kweli yote. Yn. 16:13; 17:17
  - E. Mtume wa upendo hakudharau kuhusu kuwako kwa mafundisho ya uongo - 1 Yoh 2:4.
  - F. Madai ya Yesu Kristo katika sehemu za "Mimi....."
    1. Chakula cha uzima - 6:35.
    2. Nuru ya ulimwengu - 8:12; 9:5.
    3. Mlango wa zizi - 10:7.
    4. Mchungaji mwema - 10:11, 14.
    5. Ufufuo na uzima - 11:25.
    6. Njia, kweli na uzima - 14:6.
    7. Mzabibu wa kweli - 15:1.
  - G. Yesu ndiye "tu Mwana Pekee wa Mungu" - Yn. 1:14, 18; 3:16, 18; 1 Yoh. 4:9.
    1. Wenye msimamo huria wanajaribu kuharibu fundisho kwamba "Yesu ni Kristo Mwana wa Mungu aliye hai", - Mathayo 16:16.
      - A. Wanatafsiri, "Mwana pekee" kama "tu".
      - B. Pia wanabadili "bikira" kuwa "mwanamke kijana".
    2. Njia tatu tu mtu anaweza kuwa mwana wa Mungu:
      - A. Uumbaji - Mwa. 1:27.
      - B. Warithi (kuwa mrithi) - Rum. 8:14 - 17.
      - C. Yesu pekee ndiye "Mwana pekee wa Mungu".
1. Kwamba Mungu alikuwa Baba yake na Mariamu alikuwa mama yake.

**MWISHO:**

1. Neno la ufunguo katika Yohana ni “amini”.  
A. Hutokea mara 100 hivi.
2. Vitabu viliandikwa ili mwanadamu aweze kuamini kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu na awe na uzima wa milele - Yn. 3:16; 20:30, 31.

## **SOMO LA VIII - MATENDO YA MITUME - KUFAHAMIIKA UKOMBOZI**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu cha Matendo mara nyingi kimetajwa kuwa ni “kitovu (kiunganisho) cha Biblia”.
2. Vitabu vinne vya awali vingekuwa havijakamilika pasipo kitabu cha Matendo.
3. Kama tulivyoona, Matendo ni kitabu cha pili kuandikwa na Luka. - Lk. 1:1 - 4; Mdo. 1:1.
4. Hakielezei kazi zote zilizotendwa na mitume, bali zaidi zilizofanywa na wawili:
  - A. Petro - Sura ya 1 - 20.
  - B. Paulo - Sura ya 13 - 28.
5. Matendo ni kitabu cha mianzo:
  - A. Kumhubiri Bwana aliyefufuka - 2:14 - 36.
  - B. Kanisa - 2:41,47; 8:12.
  - C. Utekelezaji wa Agizo Kuu - 1:8.
  - D. Kuabudu (Ibada) - 2:42; 20:7.
  - E. Kuteswa kwa ajili ya imani - 4, 5, 7, 8, 12.
  - F. Wamataifa kuingia katika kanisa - 10, 11.
  - G. Jina jipya kwa watu wa Mungu - 11:26.
  - H. Wazee kwa ajili ya kanisa - 11:30; 14:23; 20:17, 28.
6. Nyaraka za Agano Jipy, hasa zile za Paulo inapasa kuzisoma kukiwa na mawazo ya Matendo ya Mitume akilini.

### **MJADALA (MADA):**

#### **1. NANI ALIKIANDIKA KITABU?**

- A. Sehemu zile zinazotaja majina katika hali ya “sisi” zinaonesha Luka alikuwa mshiriki katika sehemu nyingi za matukio - Mdo. 16:10 - 17; 20:6 - 15; 21:27, 28.
- B. Irene (Ireneaus) alisema kwamba Luka aliandika kitabu cha Matendo.
- C. Luka alikuwa nani?
  1. Labda mwenyeji wa Antiokia ya Shamu.
  2. Tabibu - Kol. 4:14.
  3. Myunani.
  4. Mwana - historia na mwadilifu - mweka historia ya Kanisa wa kwanza.
  5. Mmisionari na mtenda kazi pamoja na Paulo, Sila, Timotheo, Tito n.k.

#### **2. KILIANDIKWA LINI NA WAPI?**

- A. Yawezekana toka Rumi kwani kinaishia na kufungwa kwa Paulo mara ya kwanza kule - Mdo. 28:30, 31.
- B. Historia yaonesha Paulo aliuawa wakati wa mateso ya Nero - 64 - 68 B. K.
- C. Labda mwishoni mwa 62 au mapema 63.

#### **3. KWA NINI KILIANDIKWA?**

- A. Yesu alikufa msalabani, akazikwa kaburini na akafufuka toka kwa watu kufanya wokovu uwezekane - 1 Kor. 15:1 - 4.
  1. Alitoa Agizo Kuu - Mt. 28:19,20; Mk. 16:15,16; Lk. 24:44 - 47.
  2. Matendo ya Mitume kinaonesha lilivyotekelzwa.
- B. Matendo ni kitabu cha kuongoka.

- C. Baadhi waliochaguliwa na Roho Mtakatifu kama kielelezo kwa ajili ya vizazi vijavyo:
1. Wayahudi siku ya Pentekoste - sura ya 2.
  2. Wasamaria - 8:5 - 12.
  3. Simoni mchawi -8:13.
  4. Towashi mtu wa kushi (Ethiopia) - 8:26 - 40.
  5. Sauli - sura ya 9, 22, 26.
  6. Korneli o -sura ya 10, 11.
  7. Lidia - 16:13 - 15.
  8. Mlinzi wa gereza la Filipi - 16:25 - 34.
  9. Wakorintho - 18:1 - 18.
  10. Wanafunzi wa Efeso - 19: 1 - 6.
- D. Hatua za msingi zinazopatikana katika matukio haya ya kuongoka:
1. Injili kuhubiriwa - Marko 16:15; Rum. 10:17.
  2. Wasikiaji kuamini - Marko 16:16; Yn. 8:24.
  3. Kutubu dhambi zilizopita - Lk. 13:3; 24:47
  4. Kumkiri Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu - Rum. 10:8-10.
  5. Kubatizwa kwa ondoleo la dhambi - Mt. 28:19; Marko 16:16; Rum. 6:4; Mdo. 2:38.
  6. Bwana huongeza katika kanisa - Mt. 16:18; Mdo.2:47; 8:12
  7. Anayefanya mambo hayo leo hupokea yale yale, yaliyoelezwa hapo juu.
- E. Matendo ni kitabu cha umisionari - Lk. 24:47; Mdo. 1:8.
1. Injili kuhubiriwa:
    - A. Kule Yerusalem - Sura ya 2-6.
    - B. Kule Uyahudi - Sura ya 2 - 9.
    - C. Kule Samaria - 8:4 - 25.
    - D. Sehemu za mbali duniani - sura ya 10-28.

#### 4. KILIANDIKWA KWA NANI?

- A. Anuani ni kwa Thiofilo - Mdo. 1:1; Lk. 1:1 - 4.
- B. Kukusudiwa kuwa historia ya kuanza na kukua kwa kanisa.

#### 5. MUHTASARI WA MATENDO YA MITUME.

- A. Kugawa kufuatia maeneo na mvuto wako.
  1. Yerusalem - Sura ya 1 - 12.
  2. Antiokia - Sura ya 13 - 28.
- B. Kugawa kufuatia kazi za Petro na Paulo.

#### 6. SOMO TUJIFUNZALO KUTOKA KITABU CHA MATENDO LEO.

- A. Ndimi (Lugha) katika Matendo 2 zilikuwa lugha halisi za watu - Mdo. 2:4 - 8.
- B. Karama za miujiza zilitolewa kwa kuwekewa mikono ya mitume.
  1. Kwa sababu sasa hakuna mitume walio hai, karama hizo hazijakabidhiwa kwa ye yote. Mdo. 8:14 - 18; 19:6.
- C. Mungu si Mungu wa upendeleo - Mdo. 10:34,35.
- D. Kanisa moja tu na wanaokolewa wanaongezwa katika hilo na Bwana - Mdo. 2:41, 47.
- E. Swalii la "Nifanye nini niweze kuokolewa ?" linajibiwa ndani ya kitabu cha Matendo. Mdo. 2:37, 38; 9:6; 16:30 - 34; 22:16.

- F. "Mkristo", ni jina ambalo Mungu amewapa watoto wake waaminifu walitumie Isaya 62:1,2; Mdo. 11:26.
- G. Ubatizo ni lazima kwa wokovu - Mdo. 2:38,41; 8:12,13,26 - 39; 9:18; 10:47, 48; 16:15, 30 - 34; 18:8; 19:1 - 5.
- H. Walimu wapotovu watakuja toka nje na ndani ya kanisa - Mdo. 15:1 - 11; 20:28 - 32.
- I. Kuna muundo maalum wa ibada sahihi ya kanisa - Mdo. 2:42; 20:7.
- J. Kuna muundo maalum wa uongozi wa kanisa - Mdo. 14:23; 20:17, 28.
- K. Kanisa ni lazima lifanye mambo ya hisani - Mdo. 2:44, 45; 4:34 - 37, 6:1 - 6; 11:27 - 30.
- L. Kanisa linaweza kutokewa na mateso - Mdo. 4:21; 5:40; 7:1 - 60; 8:1 - 3; 12:1, 2; 14:22.
- M. Nidhamu inadaiwa na Mungu - Mdo. 5:1-11.
- N. Roho zitaongezwa katika kanisa kila siku kama kila siku mafundisho yatafanywa Mdo. 2:47; 5:42.
- O. Ufalme ulikwishaanzishwa na Kristo anatawala juu yake - Mdo. 2:29 - 36; 8:12; 19:8; 20:25; 28:30, 31.

**MWISHO:**

1. Kitabu cha Matendo kinafunua sheria mbili za msamaha
  - A. Kuamini na kubatizwa - Mdo. 8:12, 13.
  - B. Tubu na kuomba - Mdo. 8:22.
    1. Moja kwa yule ambaye si Mkristo (mdhamini wa nje) na ya pili ni mtoto aliyeanguka toka kwa Mungu.
2. Kitabu cha Matendo kinatumika kama historia ya kwanza ya kanisa.

**MATUKIO YA KUONGOKA KATIKA KITABU CHA MATENDO**

| <b>KUONGOKA</b>                              | <b>-SIKIA</b> | <b>-AMINI</b> | <b>-TUBU</b> | <b>-KIRI</b> | <b>-BATIZWA</b> |
|--|---------------|---------------|--------------|--------------|-----------------|
| Wayahudi siku ya Pentekoste - Mdo. 2:14 - 40 |               |               |              |              |                 |
| Wasamaria - Mdo. 8:5 - 12                    |               |               |              |              |                 |
| Simoni mchawi - Mdo. 8:13                    |               |               |              |              |                 |
| Towashi wa Kushi - Mdo. 8:26 - 40            |               |               |              |              |                 |
| Sauli - Mdo. 9:1 - 9; 22:1 - 16; 26:13 - 18  |               |               |              |              |                 |
| Kornelio - Mdo. 10:1 - 11:18                 |               |               |              |              |                 |
| Lidia - Mdo. 16:13 - 15                      |               |               |              |              |                 |
| Mlinzi wa gereza wa Filipi - Mdo. 16:25 - 34 |               |               |              |              |                 |
| Wakorintho - Mdo. 18:1 - 8                   |               |               |              |              |                 |
| Waefeso - Mdo. 19:1 - 6                      |               |               |              |              |                 |

## **SOMO LA IX - WARUMI - UTII WA IMANI**

### **UTANGULIZI:**

1. Hufikiriwa kuwa ni kimojawapo katika vitabu vigumu kuliko vyote katika Biblia kuvielewa.
2. Pia hufikiriwa kuwa ni kitabu kikuu kuliko vyote katika nyaraka za Paulo.
  - A. Martin Luther alisema Warumi kilibadili msimamo wake wote wa wazo la wokovu.
  - B. Kumbuka, “Maandiko yote yametolewa kwa uvuvio wa Mungu”, na hivyo umuhimu unalingana - 2 Tim. 3:16, 17.
3. Labda ndicho kitabu kichoelewka tofauti mno katika Agano Jipya.
  - A. Luther aliongeza neno “-tu-” katika Rum. 3:28 na kusababisha mamilioni ya watu kuuelewa tofauti mpango wa wokovu.
  - B. Ufunguo wa kukielewa kitabu cha Warumi ni usemi “utii katika imani” ambao hupatikana mwanzoni na mwishoni mwa kitabu - Rum. 1:5 na 16:26.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIANDIKA KITABU HICHO?**

- A. Ushahidi wa ndani unaonesha ni Paulo.
  1. Kitabu kimefanywa na Mkristo wa Kiyahudi ambaye alikuwa na uzoefu wa Agano la Kale la Kiyunani na pia Kiebrania.
  2. Mwandishi anajitaja mwenyewe kama Paulo (1:1) na kujieleza mwenyewe katika hali ambayo Paulo tu anaweza - Rum. 11:13; 15:15 - 20.
- B. Ushahidi wa nje unaonesha ni Paulo.
  1. Marcion, mnamo 140 B.K. alisema Paulo aliandika kitabu cha Warumi.
  2. Ireneaus (Irene) alidai Paulo ndiye aliyeandiaka.
  3. Waandishi wa zamani wote kuanzia Irene huonesha Paulo ndiye aliyeandiaka kitabu hicho.

#### **2. ALIANDIKIWA NANI?**

- A. Mji wa Rumi ulikuwa mji mkubwa kuliko yote ya wakati wake.
  1. Ulianzzishwa mwaka 753 K.K.
  2. Ulitawala ulimwengu.
  3. Njia zote zilielekea Rumi.
- B. Wayahudi wengi walifanya Rumi makazi yao.
  1. Wayahudi kutoka Rumi walikuwepo siku ya Pentekoste (Mdo. 2:10).
  2. Makazi ya jumuia za Kiyahudi yamekuwepo tangu karne ya pili K.K.
    - A. Hata hivyo, yaliongezeka zaidi baada ya Pompey kuishinda na kuiunganisha Uyahudi mwaka 63 K.K.
  3. Cicero alitaja mvuto mkubwa wa Jumuia za Kiyahudi huko Rumi mwaka 59 K.K.
  4. Mfalme Tiberio aliwfukuz a Wayahudi Rumi mwaka 19 B. K.
    - A. Wengi walirudi ruhusa ya kurudi Rumi ilipotolewa.
  5. Pia walifukuzwa wakati wa utawala wa Klaudio aliyetawala kuanzia 41 - 54 B.K.
    - A. Prisila na Akila walitakiwa waondoke Mdo. 18:2.
- C. Ni nani alianzisha kanisa Rumi?
  1. Haiwezekani awe ni Paulo kwa sababu lilikuwa huko kanisa kabla hajaenda Paulo huko (Rumi) - Rum. 1:10 - 13.

2. Haiwezekani iwe ni Petro, kwa sababu hakuna rekodi za kuwepo kwa Petro huko Rumi wakati wo wote wa uhai wake.
3. Kuna uwezekano mkubwa kwamba Injili ilipelekwa Rumi na Wayahudi wa Rumi wakati walipoongoka siku ya Pentekoste - Mdo. 2:10.
4. Ilikuwa ni vyepesi kwa Injili kufika Rumi kwa sabbu kulikuwa ni kitovu kikuu cha biashara.
5. Kanisa lilikuwa limejiimarisha vya kutosha wakati Paulo anaandika - Rum. 1:8.

## 2. KITABU KILIANDIKWA LINI NA WAPI?

- A. Wayahudi walifukuzwa na Klaudio 52 B. K. kwa amri yake.
  1. Prisila na Akila tayari walikuwa Korintho alipokuja Paulo.
  2. Paulo alikaa Korintho kwa muda wa miezi kumi na nane Mdo. 18:11.
  3. Kisha alisafiri kutoka Kenkrea hadi Antiokia ya Shamu, akisimama Efeso na Kenkrea akiwa njiani - Mdo. 18:18 - 22.
  4. Alianza safari yake ya umisionari kutoka Antiokia mnamo 55 B.K.
    - A. Akapita Galatia na Fligia - Mdo. 18:23; 19:1 -4.
    - B. Kisha akafika Efeso alikokaa miaka miwili na miezi mitatu - Mdo. 19:8, 10, 21, 22; 20:31.
  5. Hivyo tarehe haiwezi kuwa kabla ya 56 B. K. wala baada ya 58 B. K.
- B. Kitabu kiliandikwa kutoka Korintho wakati wa miezi yake mitatu ya kukaa Uyunani - Mdo. 20:2, 3.
  1. Alikaa ndani ya nyumba ya Gayo - Rum. 16:23.
  2. Gayo alibatizwa na Paulo Korintho - 1 Kor. 1:14.

## 3. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?

- A. Paulo alikuwa ametaka kulitembelea kanisa Rumi, lakini alishindwa kufanya hivyo - Rum. 1:10 - 13.
- B. Paulo alitaka atoe karama za kiroho na kuweza kupata matunda mionganii mwao - Rum. 1:11 - 13.
- C. Alijisikia kuwiwa kuhubiri injili kwa watu wote pamoja na wale waliokuwako - Rum. 1:14, 15.
- D. Alitumaini kanisa la kule Rumi lingesaidia kazi yake aliyoipanga ifanyike Uhispania (Spain) - Rum. 15:23, 24.
- E. Alijibu swalii la "Vipi mtu anaweza kuwa mwenye haki mbele za Mungu?

## 4. MUHTASARI WA KITABU CHA WARUMI (WARAKA WA PAULO).

- A. Utangulizi - 1:1 - 15.
- B. Somo la kitabu - Injili ya Kristo 1:16, 17.
- C. Uhitaji wa Injili kwa Wamataifa 1:18 - 32.
- D. Uhitaji wa Injili kwa Wayahudi - 2:1- 3:8.
- E. Wote wamepotea pasipo injili - 3:9 - 20.
- F. Yesu ndiye njia pekee ya wokovu - 3:21 - 31.
- G. Kuhesabiwa haki kwa Ibrahimu ni kwa njia ya imani - 4:1 - 25.
- H. Matokeo ya kuhesabiwa haki - 5:1 - 11.
- I. Injili inafika hatua ya kuokoa, kama dhambi inavyomfikisha mtu kwenye hukumu - 5:12-21.
- J. Wokovu kwa njia ya neema hakumvutii mtu kutenda dhambi - 6:1-23.
- K. Mzigo wa, na mapungufu ya kuokolewa kwa sheria ya Musa - 7:1-25.
- L. Uhuru uko kwa Yesu Kristo - 8:1-39.
- M. Mahali pa Wayahudi katika mpango wa Mungu wa ukombozi - 9:1 - 11:36.
- N. Maonyo ya vitendo kwa ajili ya maisha ya kikristo - 12:1 - 13:14.
- O. Mambo ya imani na mambo ya hiari - 14:1 - 15:7.
- P. Paulo kama mtume kwa Mataifa - 15:8 - 33.

Q. Maonyo ya kibinagsi na salaam - 16:1 - 27.

**MWISHO:**

1. Ukweli wenge mvuto maalum:
  - A. Cha sita katika mpangilio wa vitabu nya A.J., lakini ni cha kwanza katika nyaraka kwa sababu ya umuhimu wa mafundisho yake.
  - B. Kanisa la Rumi lilijumuisha wote wawili Wayahudi na Mataifa.
  - C. Vitabu nya Wagalatia na Waebrania pamoja na 2 Korintho 3 visomwe kwa kuhusisha Warumi.
  - D. Neno haki katika Warumi humaanisha maana ile ile ya kisheria kuhalalishwa na linahusisha kitendo cha kuondolewa katika hatia.
  - E. Warumi ni waraka uliopelekwa kwa mkono wa Fibi aliyetoka kanisa lililokuwa Kenkrea - Rum. 16:1.
2. Wokovu katika Waraka wa Warumi (kwa mtazamo wa kitabu hicho).
  - A. Huokolewa kwa utii katika imani - Rum. 1:5.
  - B. Mtu anapaswa atii namna ya mafundisho - Rum. 6:17.
  - C. Utii huo huhitaji:
    1. Imani katika Yesu Kristo - Rum. 1:16, 17.
    2. Kutubu dhambi zilizofanywa nyuma - Rum. 2:4.
    3. Kukiri imani katika Yesu Kristo - Rum. 10:8 - 10.
    4. Kubatizwa kwa kuzikwa katika kifo cha Kristo - Rum. 6:3 - 5.
  - D. Utii huu ndio wenge maana ya “Kuliitia jina la Bwana” - Rum. 10:13; Mdo. 22:16.

## **SOMO LA X - 1 WAKORINTHO - MATATIZO YA KANISA LILIPU**

### **UTANGULIZI:**

1. Kanisa Korintho lilianzishwa na Paulo katika safari yake ya pili ya umisionari - Mdo. 18:1 - 18.
  - A. Kawaida yake ilikuwa ni kuingia maeneo makuu kuhubiri.
  - B. Aliishi na Prisila na Akila, watengenezaji wa hema, ambao walikuwa wamefukuzwa toka Rumi.
    1. Kama walikuwa tayari Wakristo kabla ya Paulo kuishi nao, haifaha miki.
2. Mwanzo alihubiri katika Sinagogi la Wayahudi.
  - A. Baada ya Sila na Timotheo kuungana naye, waliamuriwa kutoka katika Sinagogi.
  - B. Wakaanza kukutana kwenye nyumba ya Tito Yusto.
  - C. Kiongozi wa Sinagogi, Krispo, akawa Mkristo - 1 Kor. 1:14.
  - D. Wengi waliitii injili - Mdo. 18:8.
  - E. Paulo alikwishaambiwa na Bwana kwamba alikuwa na watu wengi Korintho - Mdo. 18:10.
  - F. Paulo alikaa Korintho kwa muda wa mwaka mmoja na nusu - Mdo. 18:11.
3. Shutuma zilizuka dhidi ya Paulo mbele ya liwali Galio zikilet wa na Wayahudi.
  - A. Galio alikataa kushughulikia masuala ya sheria za Kiyahudi.
  - B. Sosthene, mkuu wa sinagogi alipigwa na Wayunani, lakini Galio hakuona kama ni kitu cha kujali.
4. 1 Wakorintho hunukuliwa mara nyingi zaidi ya nyaraka zingine za Paulo.
  - A. Ni Waraka unaoshughulikia matatizo katika kanisa.

### **MJADALA:**

1. **NI NANI ALIANDIKA KITABU?**
  - A. Jina la Paulo na Sosthene yamehusishwa kuwa ni waandishi wa waraka huo - 1 Kor. 1:1.
  - B. Waandishi wa zamani humpa haki Paulo kama ndiye mwandishi wa waraka huo.
    1. Mnamo 95 B. K. Clement wa Rumi aliandika Korintho akihusisha kitabu hicho kwamba “waraka wa mtume Paulo mbarikiwa”.
    2. Mwanzioni mwa karne ya pili Polycarp alinukulu 1 Kor. 6:2 kwa kumpa haki ya uandishi wa sehemu hiyo Paulo.
    3. Mnamo 150 B.K. Justin Martyr alinukulu 1 Kor. 11:19 kama sehemu iliyoandikwa na Paulo.
    4. Mwishoni mwa karne ya pili Irene alinukuu 1 Wakorintho kiasi cha mara 60.
2. **KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**
  - A. Kwa Kanisa la Korintho - 1 Kor. 1:2
  - B. Mji wa Korintho ulikuwa ni wa kale.
    1. Ulikuwepo miaka 1000 kabla ya Kristo.
    2. Ulijumlishwa katika utawala wa Filipo (Philip) wa Makedonia mwaka 338 K.K.
    3. Ukawa na hadhi ya kujitawala mwaka 196 K.K.
    4. Ukakamatwa chini ya Rumi mwaka 146 K.K.
      - A. Mji ukasambaratishwa, wanaume wote wakauawa, wanawake na watoto kuuzwa utumwani.
      - B. Mji uliteketezwa kabisa na kuchomwa wote.
      - C. Miaka 100 baadaye mji ulijengwa upya na Julius Kaisari (Caesar) kama koloni la Kirumi.
    5. Kufikia wakati wa Paulo watu 600,000 wenye utaifa wa Kiyahudi, Kiyunani na Kirumi walikuwa wanaishi mjini humo.
  - C. Mji huo ulikuwa katika ukanda wa nchi inayotenganisha kati ya bahari ya Aegean na Ionian.
    1. Njia ya Biashara kutoka Kaskazini kwenda Kusini mwa Uyunani ilidhibitiwa na mji wa Korintho.

2. Meli zilikuwa zinakokotwa kwenye ardhi inayozitenganisha bahari hizo.
  3. Mfereji ulianzishwa na Nero, lakini haukukamilishwa hadi mwaka 1893.
  4. Mji ulijengwa kwenye mwamba ambao ndio juu yake mwinuko ulioitwa Acrocorinthus, wenyewe kimo cha ft. 2,000, unaanzi a (mwinuko mrefu kupita yote Korintho).
- D. Hekalu la Venus (Aphrodite) likikuwa upande wa kaskazini mwa Acrocorinthus.
1. Malaya wa hekalu 1,000 waliendesha shughuli zao huko.
  2. Maovu ya Korintho yalijulikana ulimwengu mzima.
    - A. Kufanya Ukorintho (Corinthianize) kulimaanisha kufanya uovu wa kijinsia unaozidi kipimo cha ufuksa.
    - B. Kumtaja mtu kuwa ni Mkorintho likikuwa ni tusi.
    - C. Paulo aliandika juu ya hali hii dhalili katika Rum. 1:18 - 32.
- E. Mji ulijulikana katika masuala ya utamaduni.
1. Ustadi wa ujenzi ulijulikana na kupendwa kwingi.
  2. Watu wa Korintho walipenda umahiri wa usemi na mdahalo wa kifilosofia.
  3. Michezo ya Isthmian, iliyofanana na ile ya Olympic, lifanyika kila mwaka huko Korintho.

### **3. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Baada ya Paulo kuondoka Korintho alijulishwa matatizo yaliyolisumbua kanisa
1. Habari za matatizo hayo zililetwa na jamaa wa nyumbani mwa Kloe. 1:11.
  2. Timotheo alitumwa na Paulo kuwasaidia - 1 Kor. 4:17; 17:10.
  3. Barua iliandikwa kwa kanisa, ambayo haikuhifadhiwa - 1 Kor. 5:9.
  4. Apolo alikuwa amekwisha rejea Efeso baada ya kuhubiri Korintho - 1 Kor. 16:12
  5. Stefana, Fotunato na Akaiko walikuja kwa Paulo yamkini kuleta msaada kutoka Kanisa lililokuwa Korintho - 1 Kor. 16:17, 18.
  6. Kanisa likikuwa limemwandikia Paulo likiulizia juu ya mambo kadhaa - 1 Kor. 7:1, 25; 8:1; 12:1; 16:12.
- B. Masuala yalliyolikumba kanisa la Korintho:
1. Faraka kuhusiana na wahubiri - sura 1 - 4.
  2. Kushindwa kutekeleza vema mambo ya nidhamu - sura ya 5.
  3. Kushitakiana kati ya Wakristo mbele ya mabaraza ya wapagani - sura ya 6.
  4. Masuala ya ndoa - sura ya 7.
  5. Matatizo ya kula vyakula na mambo ya uhuru - sura ya 8 - 10.
  6. Matatizo yahusuyo wajibu wa wanawake na tabia - sura ya 11:1 - 16.
  7. Matatizo ya Chakula cha Bwana - sura ya 11:17 - 34.
  8. Matatizo ya matumizi ya karama za kiroho - sura ya 12 - 14.
  9. Kukana ufufuo wa mwili - sura ya 15.
  10. Matatizo yahusuyo changizo - sura ya 16.

### **4. KITABU HICHO KILIANDIKWA LINI NA WAPI?**

- A. Kufuatana na maelezo yaliyopatikana Delphi, Galio alikuwa liwali Korintho mwaka 51 A.D.
- B. Kama Paulo aliletwa mbele ya Galio karibu na mwisho wa kukaa kwake kwa miezi 18, ingeonekana ni mwaka 52 A.D.
1. Punde baada ya hapo Paulo aliondoka Korintho.
  2. Kufuatia ziara yake ya Antiokia, alirudi Efeso ambako alikaa miaka kati ya miwili na mitatu - Mdo. 19:1-20; 20:31.
  3. Ni wakati huo ndipo Paulo alipoandika 1 Wakorintho.
  4. Hiyo ingeweka kuandikwa kwa kitabu hicho kusiwe kabla ya 55 A.D. na sio baada ya 57 au 58 B. K.

## 5. MUHTASARI WA I KORINTHO

A. Kitabu kinaweza kutengenezewa muhtasari kulingana na masuala yaliyolikumba kanisa (Yale yote ya 3B):

1. Faraka kuhusiana na wahubiri - sura 1 - 4.
2. Kushindwa kutekeleza vema mambo ya nidhamu - sura ya 5.
3. Kushitakiana kati ya Wakristo mbele ya mabaraza ya wapagani - sura ya 6.
4. Masuala ya ndoa - sura ya 7.
5. Matatizo ya kula vyakula na mambo ya uhuru - sura ya 8 - 10.
6. Matatizo yahusuyo wajibu wa wanawake na tabia - sura ya 11:1 - 16.
7. Matatizo ya Chakula cha Bwana - sura ya 11:17 - 34.
8. Matatizo ya matumizi ya karama za kiroho - sura ya 12 - 14.
9. Kukana ufuluo wa mwili - sura ya 15.
10. Matatizo yahusuyo changizo - sura ya 16.

### MWISHO:

1. Kanisa leo linakumbwa na matatizo mengi ya aina ile ile kama yaliyolikumba kanisa la Korintho.

## **SOMO LA XI - 2 WAKORINTHO - KUJITETEA KWA PAULO KUHUSU UTUME WAKE.**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu hiki yawezekana husomwa mara chache na kisichojulikana kuliko vitabu vya nyaraka zote za Paulo.
  - A. Hakiko katika mpangilio mzuri kama barua zake zingine.
  - B. Labda yatokana na shauku kubwa iliyooneshwa na Paulo anapotetea mamlaka yake ya kitume kwenye kusanyiko alilolianzisha.
2. Kitabu hiki ndicho kinachoelezea maisha ya Paulo zaidi kuliko nyaraka zake zote zingine.
  - A. Mengi yanafahamika humo ndani kuhusu kusumbuka kwake, mateso na sadaka yake, ambayo hayamo katika nukulu za maandiko yake mengine.
  - B. Tunafahamishwa moyo wa mtu huyu ambaye anatafuta kujitetea dhidi ya wale ambao wanetaka kuharibu ushawishi wake.
3. Kitabu hicho chapaswa kisomwe kama mfululizo na 1 Wakorintho.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIANDIKA KITABU HICHO?**

- A. Paulo anajitaja mwenyewe mara mbili kwamba ndiye mwandishi - 2 Kor. 1:1; 10:1.
- B. Kitabu kimekuba liwa kwa pamoja kwamba mwandishi ni Paulo.
  1. Polycarp - 150 B.K.
  2. Irenaeus - 185 B.K.
  3. Clement wa Alexandria - 210 B.K.

#### **2. KILIANDIKWA KWA NANI?**

- A. Kwa kanisa la Korintho - 2 Kor. 1:1.
- B. Kanisa lilianza mwanzoni, mwanzishaji akiwa Paulo, katika safari yake ya pili ya umisionari - Mdo. 18:1-18.
  1. Korintho ulikuwa ni mji wa kale.
    - A. Ulijengwa yapata miaka 1,000 K.K.
    - B. Warumi waliuteketeza kabisa mwaka 146 K.K. na kuujenga wao wenyewe miaka 100 baadaye.
    - C. Kinamna maalum ulikuwa katika makusudi ya kijeshi na kibashara.
    - D. Maadili yake yalikuwa ya chini sana.
- C. Kusumbuka kwa Paulo kulikuwa na mafanikio sana.
  1. Wengi waliitii injili - Mdo. 18:8 - 10.
  2. Paulo alibaki hapo kwa muda wa miezi 18 - Mdo. 18:11.

#### **3. KITABU KILIANDIKWA LINI NA WAPI?**

- A. Kanisa lilianzishwa na Paulo Korintho mwaka 50 - 51 A.D.
  1. Paulo aliletwa mbele ya Galio kwa shutuma toka kwa Wayahudi - Mdo. 18:12
  2. Maelezo yaliyopatikana Delphi yenyе tarehe (mwaka) 51 A.D. yaonesha Galio alikuwa liwali wa Akaya wakati huo.
- B. Paulo baada ya kuondoka Korintho alikwenda Efeso kisha Kaisaria na Antiokia - Mdo. 18:19 - 22.
  1. Paulo alirudi Efeso kwa kupitia Galatia na Frigia - Mdo. 18:23; 19:1.
  2. Alibaki Efeso kwa miaka 2 au mitatu - B. K. 52 - 55. - Mdo. 19:10; 20:31.

3. Aliandika barua Korintho (ya kwanza), ambayo haikutunzwa - 52 - 53 B.K. - 1 Kor. 5:9.
4. Wakorintho walijibu wakimwuliza Paulo maswali - 1 Kor. 7:1; 8:1.
5. Paulo alimtuma Timotheo ili asaidie katika matatizo yao - 1 Kor. 16:10, 11.
  - A. Yawezekana kwamba Paulo aliletewa taarifa ya kukatisha tamaa toka kwa Timotheo, ambaye yamkini alikwenda Korintho akiwa na waraka 1 Wakorintho.
6. Paulo alifanya ziara fupi na ya “Uchungu” Korintho - 2 Kor. 2:1.
7. Kisha Paulo aliondoka Efeso kwenda Troa ili kukutana na Tito - 2 Kor. 2:12, 13.
  - A. Alishindwa katika jitihada yake ya kuonana na Tito.
  - B. Kisha alikwenda Makedonia ambako alikutana na Tito na kupokea ripoti ya kutia moyo - 2 Kor. 7:5-7.
8. Akaandika 2 Wakorintho kutoka Makedonia na yawezekana akautuma Korintho kwa njia ya Tito na ndugu wengine wawili - 2 Kor. 8:16 - 23.
9. Hilo lilitokea wakati fulani kati ya 55 na 57 A.D.
  - A. Labda kiasi cha miezi sita hadi mwaka baada ya kuandika 1 Wakorintho.

#### **4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Taarifa aliyoipokea Paulo toka kwa Tito ilimfariji - 2 Kor. 7:6, 7.
  1. Wengi wao katika ndugu walimjibu na walitubu - 2 Kor. 7:8 - 10.
  2. Yule aliyeishi katika uasherati alikwisha tubu - 1 Kor. 5; 2 Kor. 2:5 - 11.
- B. Paulo aliwapa moyo ili kukumbuka yaliyokuwa yakitendeka na wajitayarische kwayo, katika Wakristo wa Kiyahudi - 2 Kor. 8:9.
- C. Bado kulikuwa na kundi dogo lilolompinga Paulo - 2 Kor. 10 - 12.
  1. Walichochea upinzani dhidi yake.
  2. Walimshutumu katika njia nydingi:
    - A. Alikuwa kigeugeu na asiyeweza kutegemewa - 1:15 - 24.
    - B. Hakuwa na barua za sifa - 3:1 - 3.
    - C. Nyaraka zake zilikuwa na nguvu, lakini maumbile yake yalikuwa dhaifu - 10:8 - 11.
    - D. Hakuwa msemaji hodari - 11:5, 6.
    - E. Alipungu kiwa kujiamini kwa sababu alikataa kusaidiwa kimsaada - 11:7 - 10.
    - F. Hakuwa mtume hasa - 12:11, 12.
    - G. Hakuwa mwaminifu - 12:17, 18.

#### **5. MUHTASARI WA 2 WAKORINTHO:**

- A. Kufurahi kwa sababu Wakorintho walio wengi walitubu - sura 1 - 7.
  1. Sala ya Paulo ya sifa - 1:3 - 7.
  2. Hatari upande wake na kukata tamaa Efeso - 1:8 - 11.
  3. Dhamiri yake ya wazi kwa ajili ya kanisa Korintho - 1:12 - 14.
  4. Ziara yake aliyoipanga kuahirishwa - 1:15 - 2:4.
  5. Ombi lake kwa ajili ya ndugu mwenye toba kurejeshwa - 2:5 - 11.
  6. Wasiwasi wake wa kutoonana na Tito Troa - 2:12 - 17.
  7. Hati zake zilikuwa ni Wakristo wa Korintho - 3:1 - 3.
  8. Alikuwa mhudumu wa Agano Jipy, sio la Kale - 3:4 - 18.
  9. Anawajibu wapinzani wake - 4:1 - 6.
  10. Yeye na mitume wengine walikuwa ni vyombo vya duniani vyenye kuwa ndani yake Neno la Mungu - 4:7-15.
  11. Mtazamo wake wa kuona umilele usioonekana ulivyotofautiana na mwili unaoangamia - 4:16 - 5:5.
  12. Kuwa katika mwili ni kuwa haupo kwa Bwana - 5:6 - 10.

13. Uwazi wake kwa sababu alikuwa wa Kristo - 5:11 - 17.
14. Mwanadamu alipatanishwa na Kristo kwa njia ya msalaba; mitume ni mabalozi wa Kristo - 5:18 - 6:2.
15. Kuteseka kwake kwa sababu ya Kristo zilikuwa ni hati zake - 6:3 - 10.
16. Anaonekan a kwa Wakorintho kama baba kwa watoto wake - 6:11 - 13.
17. Wakristo hawapaswi kuifuata dunia - 6:14 - 7:1.
18. Kusihu kwake kwa ajili ya kukubaliwa kwake - 7:2 - 4.
19. Taarifa ya Tito kule Troa inampendeza Paulo - 7:5 - 7.
20. Furaha yake kwa sababu ya toba ya Wakorintho - 7:8 - 12.
21. Mafanikio ya ziara ya Tito - 7:13 - 16.
- B. Mchango kwa ajili ya wahitaji, sura ya 8 & 9.
  1. Mfano wa watu wa Makedonia na Kristo katika matoleo ya sadaka - sura ya 8:1 - 9.
  2. Maonyo ya kutunza msimamo wao - 8:10 - 15.
  3. Wasaidizi wa Paulo na wawakilishi wa makanisa kukusanya michango, 8:16 - 24.
  4. Ombi lake la kuwataka waishi kama anavyojivunia walivyomsikia - 9:1 - 5.
  5. Motisha (hamasa) kwa ajili ya kutoa - 9:6 - 15.
- C. Kutetea utume wake na kushutumu mitume wapotofu - sura ya 10 - 13.
  1. Nguvu yake na silaha zake kwa ajili ya mambo ya vita ya kiroho - 10:1 - 6.
  2. Yeye si "chui wa karatasi" (Ujasiri wake ni wa vitendo).
  3. Alijisifia kazi yake - walimu wapotofu walipata sifa kwa kazi isiyo yao - 10:12 - 18.
  4. Wasiwasi wake kuwa Wakorintho wangepotoshwa na walimu wa uongo - 11:1 - 6.
  5. Mhimili wake ujitegemeao ulikuwa ni kusaidia, sio kuzuia kwa Wakorintho - 11:7 - 11.
  6. Wapinzani wake walikuwa mitume wapotoshaji - 11:12 - 15.
  7. Wakorintho walikuwa wapumbavu kwa kuwakubali walimu wapotofu na kumkataa Paulo 11:16 - 21.
  8. Paulo aliweza kuoanisha majivuno ya walimu wapotofu kwa sababu ya haki ya kazi yake - 11:22 - 33.
  9. Ziara ya Paulo Paradiso - 12:1 - 6.
  10. Mwiba wa Paulo mwilini kumweka katika hali ya unyenyekevu - 12:7 - 10.
  11. Paulo akiwa mbele zaidi ya washitaki wake - 12:11 - 13.
  12. Paulo alitafuta mema yao, sio shehena yao - 12:14 - 18.
  13. Wasiwasi wa Paulo kwa yale ambayo angeyakuta Korintho - 12:19 - 21.
  14. Onyo toka kwa Paulo - hakuweza kulisitisha wakati wa ziara yake iliyofuata - 13:1 - 4.
  15. Onyo kwa Wakorintho kujiangalia wenyewe - 13:5 - 10.
  16. Kuaga kwake na baraka - 13:11 - 14.

## 6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA 2 WAKORINTHO.

- A. Kuachana katika kushirikiana ni kwa ajili ya kuona kuwa mwenye dhambi anajisahihisha - 2 Kor. 2:6 - 11; Gal. 6:1, 2; Yak. 5:19, 20.
- B. Agano Jipyä lilichukua nafasi ya Agano la Kale kwa sababu lilikuwa bora zaidi - 2 Kor. 3:5 - 18.
- C. Mkristo analo tumaini hata katika kifo - 2 Kor. 4:16 - 5:9.
- D. Wote watahukumiwa siku ijayo - 2 Kor. 5:10.
- E. Toba ya kweli huja kutoka majuto yatokanayo na moyo upendao utauwa - 2 Kor. 7:8 - 12.
- F. Kichocheo (hamasa) cha kutoa hutoka moyoni - 2 Kor. 8:1 - 5, 9, 12; 9:6 - 11.
- G. Mkristo ni lazima atoe kile ambacho ni cha uaminifu mbele za Mungu na mwanadamu - 2 Kor. 8:20 - 23.
- H. Kanisa linapaswa kuwa na ukarimu kwa wote - 2 Kor. 9:13; Gal. 6:10.
- I. Walimu wapotofu ni wadanganyifu na hatari - 2 Kor. 11:13 - 15.

- J. Tunao mfano wa mahangaiko ya kidhabihu na ustahimilivu kwa ajili ya injili - 2 Kor. 11:23 - 33.  
K. Ili mtu awe ni mtume ni lazima awe na hati zihusikazo - 2 Kor. 12:12; 1 Kor. 9:1; Mdo. 1:21, 22:15.

**MWISHO:**

1. Masomo mengi muhimu sana yanapatikana katika kitabu hicho.
2. Tunapata undani wa fikira katika matatizo ambayo kanisa limekumbwa nayo katika karne ya kwanza na kitabu kinatuzatiti kuyashughulikia matatizo ya leo yanayolingana na hayo.

## **SOMO LA XII - WAGALATIA - UKWELI WA INJILI**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu cha Wagalatia kimeitwa “MAGNA CHARTA cha Imani ya Ukristo”.
2. Ni kitabu cha kiaskari kimeandikwa katika roho ya kimapambano.
  - A. Walimu wapotovu kuipotosha injili kwa kuweka sheria juu ya waongofu wa kimataifa kwa mambo ya tohara na Sheria ya Musa.
  - B. Kimsingi ni kuwa waliingiza mambo ya tohara na Sheria kuishika katika mpango wa wokovu.
  - C. Paulo hakuwa tayari kuwapa nafasi walimu hao wapotofu kufundisha hivyo - Gal. 2:5.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIANDIKA HICHO?**

- A. Hakuna kuhoji kwamba alikuwa Paulo.
  1. Ni nadra sana uthabiti wa mwandishi wa nyaraka nne umehojiwa. Nyaraka hizo ni : Warumi, Wagalatia, 1 Wakorintho na 2 Wakorintho.
  2. Luga na mtindo wa nyaraka zingine hupimwa kwa kutumia nyarak a hizo nne kuona kama ni za hakika.
- B. Ushahidi wa nje huonesha kuwa mwandishi ni Paulo.
  1. Clement wa Rumi, Polycarp, Ignatius na Barnaba wanatumia kumbukumbu za Wagalatia.
  2. Marcion, mnamo 140 A.D. ndiye wa kwanza kutaja Wagalatia kwamba mwandishi wake ni Paulo.
  3. Irenaeus, Tertullian na Clement wa Alexandria walidondo mara nyingi Wagalatia na kukihusisha naye katika uandishi.
- C. Ushahidi wa ndani unaonesha kwa Paulo.
  1. Mwandishi hujitaja mwenyewe Paulo mara mbili - 1:1: 5:2.
  2. Msamiati, mtindo na mwelekeo ni dhahiri na ule wa Paulo.
  3. Mengi ya sura ya kwanza na ya pili ni yale yahusuyo maisha ya mtu.

#### **2. KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**

- A. Wagalatia walikuwa ni wale waliotokana na wapiganaji wenye kuzunguka zunguka walioon doka Gaul (Ulaya ya kat) katika karne ya 3 K. K.
  1. Kwanza waliivamia Uyunani na kisha walihamia Asia ndogo.
  2. Wakaanzisha makazi ya kudumu katika Asia Ndogo katikati.
  3. Amyntas, mfalme wa mwisho wa Galatia, alilirithisha eneo lake kwa utawala wa Rumi na likawa ni jimbo la Rumi mwaka 25 K. K.
- B. Kuna mgawanyiko katika wasomi kama Paulo aliandika Wagalatia kwa makanisa ya upande wa Kaskazini au Kusini mwa Galatia.
  1. Katika safari ya kwanza ya Paulo ya umisionari alianzisha makanisa katika Antiokia ya Pisidia, Ikonia, Listra na Derbe - Mdo. 13, 14.
  2. Hakuna taarifa ya kumbukumbu za yeze kuendesha kazi nyingi upande wa Galatia ya Kaskazini.
  3. Yaonekana yafaa zaidi kusema kwamba waraka uliandikwa kwa makanisa ambayo yeze Paulo na Barnaba waliyaanzi sha katika safari ya kwanza ya umisionari.
- C. Makanisa ya Galatia yangewajumuisha wote Wayahudi na Wamataifa, na Wamataifa kuwa wengi zaidi - Mdo. 13:14, 42-48; 14:1, 2.

#### **3. WAPI NA LINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Paulo na Sila waliyatemelea makanisa ya Galatia ambayo yeye na Barnaba waliyaanzisha wakati wa safari yao ya kwanza ya umisionari - Mdo. 16:1 - 6.
  - 1. Timotheo aliungana nao Listra.
  - 2. Kisha wakatoa mwongozo wa mitume na wazee wa Yerusalem - Mdo. 15:23-29; 16:4.
- B. Ilikuwa baada ya hilo walimu wa Kiyahudi walikuja kutoka Palestina kuja Galatia.
  - 1. Walihoji kama Paulo alikuwa mtume.
  - 2. Walifundisha kwamba Wakristo ni lazima wawe Wayahudi ili waweze kuokolewa.
  - 3. Paulo aliweza kufahamu fundisho hilo potofu.
  - 4. Kwa kutopata uwezekano wa kulitembelea kanisa, mara aliwaandikia barua - Gal. 4:20.
- C. Kuna uhaba wa kufahamu kuhusu kipindi cha wakati tangu Paulo alipozuru Galatia hadi hapo walimu wapotoshaji walipoleta mafundisho ya kiyahudi au mapema kiasi gani alivifahamu vitendo vyao.
  - 1. Ilikuwa dhahiri kuwa ni baada ya baraza la Yerusalem kwa sababu suala la tohara lilikuwa limeshughulikiwa - Mdo. 15; Gal. 13 - 16.
- D. Kuhusu tarehe, wasomi wamegawanyika.
  - 1. Wengine maoni yao ni 48 B. K.
    - A. Hilo lingefanya waraka uwe wa mwanzo kabisa katika nyaraka za Paulo.
  - 2. Wengine wameuweka kuwa wa baadaye, kiasi cha 58 B. K..
  - 3. Kwa sababu ya mtindo wa mafundisho kufanana na nyaraka za Warumi, Galatia, I & II Wakorintho, wengi wamehitimisha ni lazima ziwe ziliandikwa nyakati zilizokaribia na.
  - 4. Yawezekana uliandikwa kutoka Makedonia au Akaya mnamo 55 au 56 B.K.

#### **4. KWA NINI KITABU HICHO KILIANDIKWA?**

- A. Injili ilikukwa inapotoshwa na watu wenye mafundisho ya kiyahudi - Gal. 1:6 - 9.
  - 1. Wale waliokuwa wakiwashirikisha watu Sheria ya Musa walikuwa wameanguka toka katika neema - Gal. 5.
- B. Utume wa Paulo ulikuwa unakataliwa na walimu wapotoshaji wa kiyahudi.
  - 1. Kama wangeweza kupinga utume wake wangeweza kupinga mafundisho yake.
  - 2. Paulo anajitetea kwa maelezo mengi:
    - A. Kama ilimpendeza kuwafurahisha watu, asingekuwa mtumishi wa Kristo.
    - B. Injili yake ilimfikia moja kwa moja toka Mbinguni.
    - C. Aliuacha wadhifa wake katika dini ya Kiyahudi ili kumfuata Kristo.
    - D. Aliitwa na Mungu tangu tumboni mwa mamaye.
    - E. Katika ziara zake mbili Yerusalem, mitume na wazee hawakufanya mabadiliko yo yote katika injili, lakini, badala yake wakampa mkono wa ushirikiano.
    - F. Alipingana na mtume mwininge, Petro, uso kwa uso alipokosa.
    - G. Utu wake wa zamani ulisulibiwa na Kristo na sasa anaishi maisha ya huduma kwa Kristo.

#### **5. MUHUTASARI WA WAGALATIA.**

- A. Kujitetea kwa Paulo katika injili aliyoitangaza na utume wake - sura ya 1 na 2.
- B. Kusudi la Sheria ya Musa - sura ya 3.
- C. Hadithi ya mfano wa Sara na Hajiri ilikuwa ni kielelezo kutoka katika Sheria – sura ya 4.
- D. Tofauti kati ya matendo ya mwili na tunda la roho - sura ya 5.
- E. Maonyo ya vitendo - sura ya 6.
  - 1. Kubeba mizigo ya wengine - 6:1-5.
  - 2. Kupanda na kuvuna - 6:6-10.

3. Paulo alijisifia katika Kristo wakati Wenye mafundisho ya Kiyahudi walijisifia katika mwili - 6:11 - 17.
4. Baraka - 6:18.

## 6. MASOMO TUJIFUNZAYO KUTOKA WAGALATIA

- A. Wakristo hawako chini ya Sheria ya Musa - Gal. 3:11, 23 - 25; 4:21-5:4.
  1. Kosa la madhehebu ni kushindwa kwao kulitumia kwa halali neno la kweli.
  2. Masuala ya wokovu, Ibada na maisha ya Kikristo yanaweza kujibiwa kwa usahihi kwa kulitumia kwa halali Neno.
- B. Kusudi la Sheria ya Musa lilikuwa la pande mbili:
  1. Liliongezwa kwa sababu ya makosa ya mwanadamu - Gal. 3:19.
  2. Lilikuwa ni kiongozi kumleta mwanadamu kwa Kristo - Gal. 3:24.
- C. Mwanadamu yupo chini ya sheria leo, japokuwa sio ile ya Musa.
  1. Mwanadamu yupo chini ya sheria ya Roho - Rum. 8:2.
  2. Mwanadamu ni lazima aitimiza sheria ya Kristo - Gal. 6:2; 1 Kor. 9:21.
  3. Mwanadamu anapaswa aendelee katika sheria timilifu ya uhuru - Yak. 1:25.
  4. Kuna amri za Bwana zinazohitaji kutiiwa - 1 Kor. 14:37.
  5. Upendo wa mwanadamu kwa Mungu huoneshwa kwa kushika amri zake - Yn. 4:15.
- D. Inawezekana kwa mtoto wa Mungu kuanguka kutoka katika neema - Gal. 5:4.
- E. Injili iliyopotoshwa haiwezi kuokoa - Gal. 1:6 - 9.
- F. Matendo ya mwili huongoza katika hukumu ya milele - Gal. 5:19 - 21.
- G. Tunda la Roho lionekane katika maisha ya Mkristo - Gal. 5:22 - 25.
- H. Mwanadamu huvuna alichopanda - Gal. 6:6 - 10.
- I. Baraka za kiroho ziko katika Kristo mwanadamu anapobatizwa - Efe. 1:3; Gal. 3:26,27.
- J. Kuna mafundisho ya fungasho moja tu ambayo ni lazima kuyatii - Gal. 2:5, 14, 16; 5:7; 1 Pet. 1:22.
- K. Atwambiaye kweli ni rafiki na sio adui - Gal. 4:16.
- L. Mwanadamu huokolewa kwa imani itendayo kazi ya upendo - Gal. 5:6.
- M. Kuwafadhili wahitaji kuelekezwa kwa wale ambao wako katika uhitaji na kwa kadiri fulsa ipatikanapo - Gal. 1:2; 6:10.
- N. Ni dhambi kufungamanisha ambapo Mungu amefungua na kufungua pale alipofunga - Gal. 5:2 - 4.
- O. Mtoto wa Mungu ni lazima awe tayari kukemea wale wanaofanya makosa - Gal. 2:11 - 14.
- P. Petro alikosea katika masuala ya mafundisho, hangeweza kuwa Papa - Gal. 2:11 - 14.
- Q. Atendacho mmoja chawaathi ri wengine - 2:13.

## MWISHO:

1. Kitabu hiki kinafundisha vema mahali na kusudi la Agano la Kale.
2. Ni kitabu cha Wagalatia kama kuna jitihada ya kuokoa makusanyiko mengi toka upotofu.

## **SOMO LA XIII - EFESO - UTUKUFU KWA KRISTO**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu cha Waefeso ni kimoja kati ya vinne vijulikavyo kama Nyaraka za Paulo kifungoni.
  - A. Ni: - Efeso, -Filipi, -Kolosai na - Filemoni.
  - B. Zote nne ziliandikwa wakati Paulo alikuwa amefungwa kwa mara yake ya kwanza Rumi - Mdo. 28:30, 31.
  - C. Tatu ziliandikwa kwenye makanisa au kwa watu binafsi wa eneo moja.
    1. Efeso na Kolosai zilikuwa Asia.
    2. Filemoni aliiishi Kolosai.
    3. Yawezekana Tikiko alizichukua barua hizo na kuwapelekea wahusikao - Efe. 6:21; Kol. 4:7.
    4. Yaliyomo ndani yanaelekeana.
      - A. Hasa Waefeso na Wakolosai, nyaraka hizo huitwa “Pacha”.
    5. Zote nne zinahusisha Paulo kuwa kifungoni Rumi - Efe. 3:1; 4:1; 6:18 - 20; Flp. 1:12,13; 4:22; Kol. 4:2 - 4; Flm. 1:10, 22, 23.
2. Kitabu cha Waefeso kimehusishwa kwamba ndicho kitabu chenye jumla ya “nasaha kuu kupita zote kuhusu kanisa.....”
  - A. Kristo anasimama kama kichwa cha kanisa katika kitabu cha Wakolosai.
  - B. Kanisa linasimama kama mwili wa Kristo katika kitabu cha Waefeso.

### **MJADALA :**

#### **1. NI NANI ALIYEANDI KA KITABU HICHO?**

- A. Ushahidi wa nje unaomwonesha Paulo kuwa ndiye mwandishi ni mkubwa.
  1. “Kama mbarikiwa Paulo atangazavyo katika waraka wake kwa Waefeso ....” Irene (Ireneaus) 120 – 202.
- B. Ushahidi wa ndani unaonesha kuwa Paulo ndiye mwandishi.
  1. Mwandishi anajitaja mwenyewe kuwa ni Paulo mara mbili Efe. 1:1; 3:1.
  2. Lugha, mtindo na hoja ni vya Paulo.
  3. Kati ya mistari 155 katika Waefeso, 78 hupatikana katika mwelekeo wa usemi katika Wakolosai.
- C. Wapinzani wamepinga uandishi wa Paulo.
  1. Wanadai kuwa mwandishi hakuwahi kuwa Efeso kwa sababu aliandika aliyokuwa amesikia juu ya imani yao (1:15), na hatoi salamu za binafsi kwa washiriki binafsi.
  2. Hata hivyo, Paulo alisema alikuwa amesikia imani ya Filemoni na Filemoni alikuwa ni mmoja wa walioongolewa na Paulo - Flm. 5, 19.
    - A. Paulo hakupeleka salamu za kibinafsi kwa watu binafsi katika nyaraka zake nyingi - 2 Wakorintho, Wagalatia, 1 & 2 Wathesalonike.

#### **2. KITABU HICHO KILIANDIKWA KWA NANI?**

- A. Kimeandikwa kwa “Watakatifu walioko Efeso” Efe. 1:1.
- B. Kanisa la awali liliamini karibu kwa pamoja kuwa waraka huo ulitumwa Efeso.
  1. Ireneaus, Tertullian, Clement wa Alexandria na Origen, wote wanahusisha kama “Waraka kwa Waefeso”.
  2. Yote isipokuwa sehemu tatu tu za maandiko ya awali zina maneno “kule/pale Efeso”.
- C. Wasomi wengine wanapingana, wakiamini ulikuwa ni waraka wa ujumla kwa makanisa yote ya Asia.

1. Wanadai, kwa msingi wa kukosekana sehemu hizo tatu tu za maandiko ya awali “kule/pale Efeso”, kwamba katika nakala za baadaye maneno hayo yalitiwa.
  - A. Nadharia hiyo haina uthibitisho.
  - B. Hata kama ni kweli haiwezi kuleta madhara katika maana.
    1. Na wala haiharibu uvuvio wake.
- D. Kanisa kule Efeso lilianzishwa na Paulo - Mdo. 18:19, 20.
  1. Katika safari yake ya pili ya umisionari Paulo aliwatembelea kwa muda mfupi - Mdo. 18:19 - 21.
  2. Prisila na Akila walibaki Efeso - Mdo. 18:18 - 28.
  3. Katika safari yake Paulo ya tatu ya umisionari walitumia miaka mitatu Efeso - Mdo. 19:1 - 20:1.
    - A. Watu 12 walioujua ubatizo wa Yohana tu walibatizwa - Mdo. 19:1 - 7.
    - B. Paulo alihubiri kwenye masinagogi mpaka upinzani ulipotokea na kumsababisha kuhamia kwenye shule ya Tirano ambako alihubiri kwa muda wa miaka miwili - Mdo. 19:8 - 10.
    - C. Alitenda miujiza mingi akiwa Efeso - Mdo. 19:11, 12.
    - D. Vitabu vya wale waliokuwa wakiendesha mambo ya uchawi vilichomwa kwa moto - Mdo. 19:13 - 20.
- E. Kwa sababu ya machafuko yaliyotokea Efeso, Paulo alilazimika kuondoka - Mdo. 19:23:20:1.
  1. Efeso ulikuwa uwandani maili tatu toka bahari ya Mediterranean (Bahari ya Kati).
  2. Kilikuwa kitovu cha biashara katika jimbo la Asia katika utawala wa Kirumi.
  3. Hekalu la Diana au Artemi lilikuwa ni umaarufu wao mkuu.
    - A. Lilijengwa juu ya jukwaa la ft. 425 kwa ft. 240.
    - B. Lilikuwa na kipimo cha ft. 343 kwa ft. 164.
    - C. Kulikuwa na nguzo zaidi ya 100 zenye urefu kiasi cha ft. 60.
    - D. Sanamu ya Diana, iliyodaiwa kuwa ilianguka toka mbinguni, ilikuwa hapo.
    - E. Illichukuliwa kuwa ni mojawapo ya maajabu saba ya dunia.
  4. Paulo alikuwa na mafanikio sana katika kazi yake hata watu waliacha kuamini Diana - Mdo. 19:23 - 41.
    - A. Wale waliochonga na kuuza sanamu (vinyago) ya Mungu huyo wakawa hawana biashara.
    - B. Vurugu dhidi ya Paulo ikiongozwa na Demetrio mfua fedha (mtengeza vihekalu) ikatokea.
    - C. Baada ya ghasia kuzimwa na karani wa mji, Paulo aliondoka kwenda Makedonia alikokuwa ameazimia awali kwenda - Mdo. 19:21, 22; 40:20:1.

### **3. LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Paulo alikuuwa amefungwa Rumi.
- B. Tarehe za kufungwa huko kwa kawaida hutajwa kama 60 - 62 B. K.

### **4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Haielekei kuwa kiliandikwa kushughulikia tatizo maalum.
- B. Inaelekewa ulikuwa waraka wa mafundisho tu uliopelekwa na Tikiko, ambaye alikuwa anarudi Asia akilipelekea barua kanisa la Kolosai - Efe. 6:21; Kol. 4:7.

### **5. MUHTASARI WA KITABU CHA WAEFESO.**

- A. Salaam - 1:1, 2.
- B. Mpango wa wokovu ambapo mwanadamu huchaguliwa na Mungu, hukombolewa na Kristo, na kuwekwa mhuri na Roho Mtakatifu. - 1:3 - 14.
- C. Sala ya kwanza ya Paulo kwa ajili ya Waefeso - 1:15 - 23.
- D. Waefeso, ambao awali walikuwa wafu katika dhambi, sasa waokolewa kwa neema - 2:1 - 10.

- E. Wayahudi na Mataifa sasa mwili mmoja katika Kristo - 2:11, 12.
- F. Nafasi ya upendeleo ya Paulo kumhubiri Kristo - 3:1 - 13.
- G. Sala ya pili ya Paulo kwa ajili ya Waefeso - 3:14 - 21.
- H. Umoja wa Roho - 4:1 - 16.
- I. Mwenendo mpya katika Kristo - 4:17 - 5:20.
- J. Uhushiano wa Kristo na kanisa unaoneshwa katika uhushiano wa mume na mke - 5:21 - 33.
- K. Wajibu wa watoto na watumwa - 6:19, 20.
- L. Silaha za Mkristo - 6:10 - 18.
- M. Ombi la Paulo kwa maombi ya Waefeso - 6:19, 20.
- N. Hitimisho na Baraka - 6:21-24.

**6. TUJIFUNZAYO TOKA KITABU CHA WAEFESO.**

- A. Wokovu ni kwa neema kwa njia ya imani - Efe. 2:8 - 10.
- B. Waefeso waliokolewa kwa neema walipoitii injili - Efe. 2:8, 9; Mdo. 19:1 - 8.
  - 1. Walisikia - 1:13.
  - 2. Waliamini - 1:13.
  - 3. Walitubu - Mdo. 20:21.
  - 4. Walizikwa katika maji - Mdo. 19:1 - 8; Efe. 4:5.
- C. Kuna kanisa moja tu - Efe. 1:22, 23; 4:4 - 6.
- D. Ili mtu aokolewe yampasa awe katika kanisa - Efe. 4:4; 5:23.
- E. Kanisa ni sehemu ya mpango wa milele wa kusudi la Mungu, na sio wazo la dharura kama wale waaminio vipindi vya miaka elfu - Efe. 3:8-11.
- F. Ili mtu aokolewe yampasa kuishi kwa uaminifu - Efe. 4:17-5:21; 6:1-9.

**MWISHO:**

1. Waefeso kinashughulikia kanisa la Kristo, wakati Wakolosai kinashughulikia Kristo wa kanisa.
2. Timotheo alitumwa Efeso akaonye kuhusu kufundisha neno la Mungu na wala si mafundisho mengine - 1 Tim. 1:3.
3. Mtume Yohana alitumia muda wake wa maisha uliofuata akiwa amekwenda huko Efeso baada ya maisha ya uhamishoni Patmo
4. Ya kwanza katika barua saba zilizotumwa kwenye makanisa ya Asia, ilipelekwa Efeso ili kuwaonya kuhusu tatizo lao la “kuuacha upendo wao wa kwanza” - Ufu. 2:1-7.

## **SOMO LA XIV - WAFILIPI - MAWAZO YA KRISTO**

### **UTANGULIZI:**

1. Waraka wa Waefeso unaliweka kanisa kama mwili wa Kristo, Wakolosai kumweka Kristo kama kichwa cha kanisa, na Wafilipi kuweka mawazo ya Kristo.
2. Wafilipi hakikuandikwa kusahihisha matatizo ya kanisa.
  - A. Ni barua tu iliyoandikwa na mmisionari kwa kanisa alilolianzisha.
  - B. Iliandikwa na mtu aliyekuwa na imani kubwa kwa watoto wake katika imani.
3. Mambo ya kipekee katika Wafilipi.
  - A. Paulo anajitaja mwenyewe mara nyingi zaidi kuliko katika waraka wake mwingine wo wote.
  - B. Usemi, “katika Kristo Yesu” hupatikana mara nane.
  - C. Neno la msingi katika Wafilipi ni furaha ingawa Paulo alikuwa amefungwa gerezani alipouandika waraka huo.
    1. Furaha, furahini, na kufurahi hutokeea mara kumi na tano.
    2. Kutokana na hiyo, tunaona kwamba furaha haitegemei hali ya nje, bali hutoka moyoni.

### **MJADALA:**

1. **NI NANI ALIKIANDIKA KITABU**
  - A. Ushahidi wa ndani na wa nje humwonesha Paulo kuwa ndiye mwandishi.
    1. Alijipambanua mwenyewe, pamoja na Timotheo, kama ndiye mwandishi 1:1.
    2. Mtindo na msamiati ni vya Paulo.
    3. Paulo, pekee, alikuwa na ushirikiano wa karibu na kanisa lililokuwako Filipi.
    4. Polycarp alidondoa kutoka Wafilipi mnamo 140 B.K., na akathibitisha kuwa mwandishi ni Paulo.
    5. Irenaeus (Irene) alinukuu Wafilipi 4:18 mnamo 180 A.D., na akathibitisha kuwa mwandishi ni Paulo.
    6. Tertullian alimnukuu mwandishi wa Wafilipi mnamo 200 A.D. na kuonesha aliamini mwandishi alikuwa Paulo.
  - B. Uandishi wa Paulo haukuhojiwa mpaka miaka ya 1800 na ujio wa mafundisho ya kisasa.
    1. Wengine wanadai kwamba kitabu kimekuwa dhahiri mno kwa alama zinazoonesha kuwa mwandishi ni Paulo, hivyo yaelekea ati huenda waraka huo uliandikwa na mtu aliyeghushi.
    2. Wengine wanadai Paulo anawataja “maaskofu” na “mashemasi” katika mstari, lakini hao hawakuwepo wakati wa kipindi chake.
      - A. Hata hivyo Paulo alichagua wazee wa kanisa wakati wa safari yake ya umisionari (ya kwanza) Mdo. 14:23.
      - B. Kanisa Yerusalemu lilikuwa na wazee wa kanisa hata kabla ya hapo - Mdo. 11:30.
      - C. Maneno “maaskofu” na “wazee” yametumika kwa mbadilishano - Mdo. 20:17, 28.
      - D. Barua mbili zilizoandikwa na Clement wa Rumi mnamo 95 B. K. hutaja wazee wa kanisa na mashemasi.
2. **KILIANDIKWA KWA NANI?**
  - A. Kanisa limetajwa mara mbili kwa jina - Flp. 1:1; 4:15.
  - B. Wakati wa Paulo Filipi palikuwa ni koloni la Kirumi lenye maendeleo.
    1. Palikuwa katika Makedonia katika uwanda kati ya mito Gangites na Strymon.
    2. Katika karne ya nne B.C. dhahabu iligunduliwa katika eneo hilo.
    3. Baba wa Iskanda Mkuu, Filipo wa Makedonia, aliikamata sehemu hiyo, akajenga mji na kuutajia jina kwa kumbukumbu yake.

4. Akatumia dhahabu ya Filipi kugharimia ushindi wake wa Uyunani (Ugiriki).
5. Filipi ilishirikiana na Carthage dhidi ya Rumi katika vita vya Punic.
6. Baada ya kifo cha Julius Kaisari kwa kuuawa, Filipi ulisaidiana na upande wa Brutus na Cassius dhidi ya Octavian Caesar (Kaisari) na Mark Anthony.
7. Vita vya nguvu vilipiganwa mwaka 42 K. K. katika nyanda za Filipi kati ya majeshi haya yanayopingana ambapo Mark na Octavian waliibuka washindi.
8. Kisha Filipi ukawa koloni la Rumi.
  - A. Mashujaa wa jeshi la Rumi walifanya makazi yao hapo.
  - B. Ulitaza mwa na kuonekana kama “Rumi Ndogo”.
  - C. Kilatini kilizungumzwa, na raia wake walipata hifadhi ya sheria ya Rumi.
- C. Kanisa la kule Filipi lilianzishwa wakati wa safari ya pili ya umisionari ya Paulo - Mdo. 16.
  1. Hiyo ilikuwa mara yake ya kwanza kwa Paulo kuhubiri Ulaya.
    - A. Hata hivyo, Ukristo unawenza kuwa ulikwisha ingia sehemu zingine za Ulaya, kama Rumi, kutokana na utawanyiko wa wale walioongoka siku ya Pentekoste - Mdo. 2:10.
  2. Ziara ya Paulo huko Filipi ilikuwa ni matokeo ya maono toka kwa Bwana - Mdo. 16:9, 10.
  3. Hakukuwa na sinagogi Filipi.
    - A. Sheria ya Kiyahudi ilikuwa ni kujenga sinagogi pale palipokuwa angalau na wayahudi wanaume 10.
  4. Lidia mwuzaji wa rangi zambarau kutoka Thiatira, na nyumba yake alikuwa wa kwanza kuitii injili kulingana na mahubiri ya Paulo. - Mdo. 16:14, 15.
  5. Baada ya Paulo na Sila kutoa pepo toka kwa msichana mtumwa, walichukuliwa kupelekwa mahakamani kuhukumiwa.
    - A. Wakapigwa bila kusikilizwa na kutiwa gerezani.
    - B. Tetemeko la ardhi liliwawezesha kuwa huru na mlinzi wa gereza na familia yake wakaongoka - Mdo. 16:25 - 34.
    - C. Paulo alipojitetea kwa ajili ya uraia wake wa Rumi makadhi wakawatoa na kuwashauri waondoke - Mdo. 16:37-39.
  6. Baadaye Paulo alielezea jinsi walivyotendewa kwa aibu (walivyoteswa) - 1 Thes. 2:2.
- D. Paulo aliendelea kudumisha uhusiano wa karibu na kanisa la Filipi.
  1. Yaelekea Luka aliendelea kubaki Filipi hata Paulo na Sila walipokuwa wameondoka - Mdo. 16:40; 20:6.
  2. Paulo alirudi tena Filipi angalau mara mbili - Mdo. 20:3 - 6; 2 Kor. 2:13; 7:5.
  3. Kanisa lilimsaidia Paulo kwa mahitaji kama chakula ingawa walikuwa mafukara - 2 Kor. 11:8, 9; Flp 1:4; 4:10 - 19.

### 3. LINI NA KILIANDIKWA WAPI KITABU?

- A. Kiliandikwa kutoka Rumi wakati Paulo akiwa kifungoni kwa mara ya kwanza.
  1. Kwa kawaida, yakubalika kuwa Paulo alikuwa kifungoni Rumi mara mbili.
    - A. Mara ya kwanza yatajwa katika Mdo. 28:30, 31.
      1. Alikuwa na uhuru wa kutosha kuhubiri na kuandika.
      2. Aliandika Waefeso, Wafilipi, Wakolosai na Filemoni .
      3. Alitegemea kufungu liwa kifungo hicho - Flp. 1:24, 25; 2:19 - 24.
      4. History (historia) yaonesha aliachiliwa, lakini alikamatwa tena wakati wa utesaji wa Nero na akauawa.
  - B. Wakati wa kufungwa kwake kwa mara ya mwisho, aliandika 2 Tim. - 2 Tim. 4:6 - 8, 16, 17.
    1. Anataja kumbukumbu kadhaa zinazoonesha kuwa mfungwa katika kitabu cha Wafilipi kama aoneshavyo katika nyaraka zingine za kifungoni.
      - A. Anahuisha kufungwa kwake angalau mara nne 1:7, 13, 14, 16.

- B. Anazungumzia kuhusu kifo chake, lakini anatarajia kuachiliwa - 1:20 - 26; 2:23, 24.
- C. Anatuma salamu toka kwa watakatifu nyumbani mwa Kaisari - 4:22.
- D. Kuna uwezekano mkubwa kwamba Wafilipi kiliandikwa karibu na mwisho wa kufungwa kwake, ambapo ni wakati wa miaka 60 - 62 B. K.

#### **4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Hakukuwa na adha kama ilivyokuwa kule Korintho au kuyakwepa mafundisho kama kule Galatia.
- B. Barua ziliandikwa kwa marafiki wa mbali wakati mmojawapo alikuwa akielekea huko aliweza kuichukua barua hiyo.
  - 1. Epaafroditu alimletea zawadi Paulo toka kanisa la Filipi - 4:10 - 14, 17, 18.
  - 2. Alitazamiwa kurudi mapema na angeichukua barua toka kwa Paulo.
- C. Makusudi mengi yanajionesha hapa:
  - 1. Kupeleka shukrani kwa sababu ya zawadi.
  - 2. Kuwapatia habari ya hali yake ya kifungoni Rumi.
  - 3. Akiwaku mbusha upendo wake kwa ajili yao.
  - 4. Kuwapa moyo katika imani yao.
  - 5. Kuwaonya kuhusu walimu wapotofu.
  - 6. Kuwaagiza dada wawili, Euodio na Sintike wawe na umoja katika kazi ya Bwana.

#### **5. MUHTASARI WA WAFILIPI**

- A. Kristo maisha yetu - sura ya 1, hasa mstari wa 21.
- B. Kristo mfano wetu - sura ya 2, hasa mstari wa 5.
- C. Kristo tumaini letu - sura ya 3, hasa mstari wa 8.
- D. Kristo nguvu yetu - sura ya 4, hasa mstari wa 13.

#### **6. TUJIFUNZAYO KATIKA KITABU CHA WAFILIPI.**

- A. Mpango wa Mungu katika uongozi wa kanisa kwa kila kusanyiko kuwa na wazee na mashemasi wenye sifa zitakiwazo - Flp. 1:1; Mdo. 14:23; 1 Tim. 3:1 - 13; Tit. 1:5 - 9; 1 Pet. 5:1 - 4.
- B. Kuna sababu kwa Mkristo kufurahi hata katika matatizo - Mdo. 16:25; Flp. 4:4 - 7.
- C. Watu ambaa hawaishi kwa haki au wenye nia mbaya wanaweza kuhubiri ukweli - Flp. 1:15 - 18.
- D. Mtoto wa Mungu ni lazima awe “amejiweka tayari kuitetea injili” - Flp. 1:17; Yd. 3.
- E. Ni faida kwa Mkristo kufa kwa sababu atakuwa na Kristo - Flp. 1:20 - 24.
  - 1. Hata hivyo, apende kuishi muda mrefu wa kutosha ili atumike.
- F. Maisha ya Mkristo yawe kama ipendezavyo injili - Flp. 1:27; Mt. 5:13 - 16.
- G. Wakristo wafanye jitihada kuwa na mawazo ya Kristo - Flp. 2:1 - 11.
- H. Silika ya Kristo yafundishwa katika Flp. 2:5 - 11.
  - 1. Mungu (yaani Uungu wake).
  - 2. Kuwako kabla ya vyote.
  - 3. Kuwa sawa na Mungu kabla ya kuja duniani.
  - 4. Uungu katika mwili wa kibinadamu.
  - 5. Ubinadamu wake.
  - 6. Kifo chake kitakasacho.
  - 7. Utukuzwaji wake.
- I. Wakristo hawapaswi kuhofu, bali wamwamini Mungu kwa mahitaji ya lazima - 4:6, 7.
- J. Mawazo ya Mkristo yajazwe na Fikira safi na kamili. Flp. 4:8; Mt. 12:35 - 37; 15:11, 17 - 20.
- K. Kanisa lina wajibu wa kuwasaidia wamisionari - Flp. 4:10 - 19.

**MWISHO:**

1. Kitabu cha Wafilipi ni kimojawapo kati ya vitabu vinavyopendwa zaidi na kutia moyo zaidi katika nyaraka za Paulo.

## **SOMO LA XV - WAKOLOSAI - UBORA MKUU WA KRISTO**

### **UTANGULIZI:**

1. Waefeso humwinua Kristo kama kichwa cha kanisa wakati Wafilipi huweka mawazo ya Kristo na Wakolosai huweka ubora mkuu wa Kristo.
2. Kristo ameinuliwa juu ya viumbe (uumbaji) vyote.
  - A. Kristo ni jumla ya kila sura na mstari.
  - B. Kitabu hiki kimeitwa kwamba ndicho kinachosimama kama kitovu cha Kristo katika nyaraka za Agano Jipya.
  - C. “Kristo ni yote katika yote” - Kol. 3:11.
3. Kina maeneo ya hatua tatu yanayojumlisha ubora wake Kristo mkuu.
  - A. “...ili awe mtangulizi katika yote” - Kol. 1:18.
  - B. “...katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu katika mwili” - Kol. 2:9.
4. Wakolosai huweka bayana silika ya Yesu Kristo:
  - A. Mungu ni Baba Yake - 1:3.
  - B. Ni Mwana wa Mungu mpendwa - 1:13.
  - C. Ni mfano wa Mungu asiyonekana - 1:15.
  - D. Yeye anatangulia akiwa amehusishwa na viumbe wote - 1:15.
  - E. Yeye ni kabla ya viumbe vyote - 1:17.
  - F. Vitu vyote vimeshikamanishwa na Yeye - 1:17.
  - G. Yeye ni mwanzo - 1:18.
  - H. Amewatangulia wafu - 1:18.
  - I. Ametangulia kwa kila kitu - 1:18.
  - J. Katika Kristo ukamilifu wote unakaa - 1:19.
  - K. Katika Kristo inakaa hekima yote na ufahamu - 2:3.
  - L. Katika Kristo unakaa utimilifu wote wa Mungu - 2:9.
5. Kitabu cha Wakolosai ni kimojawapo katika barua za kifungoni.

### **MJADALA:**

1. **NI NANI ALIKIANDIKA KITABU?**
  - A. Ushahidi wa ndani:
    1. Mwandishi anajitambulisha mwenyewe kwamba ni Paulo mara tatu - Kol. 1:1, 3; 4:18.
    2. Kitabu kinafanana sana na nyaraka zingine zinazofahamika kuwa ziliaandikwa na Paulo.
    3. Mwanawe Paulo katika imani ni mfuasi wa mwandishi - Kol. 1:1.
  - B. Ushahidi wa nje:
    1. Wakolosai, “Luka tabibu mpPENDWA anatumA salamu” 4:14.
    2. Mnamo 210 A.D. Clement wa Iskanderia alinukuu Kolosai 1:28 na kutaja kwamba mhusika wa maandiko hayo alikuwa Paulo.
    3. Mnamo 220 B.K. Origen alinukuu Kol. 2:18, 29 na kutaja kwamba mhusika wa maandiko hayo alikuwa Paulo.
2. **KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**
  - A. Watakatifu waliokuwako Kolosai - Kol. 1:2.
  - B. Mji wa Kolosai ulikuwa ni mmojawapo katika miji mikuu mitatu ya Frigia.
    1. Ulikuwa upo umbali wa maili 12 toka Hierapolis na maili 10 toka Laodikia.

2. Ulikuwa kwenye makutano ya mito miwili Lycus na Maeander.
  3. Ulitelemka umashuhuri wake na kuzidiwa na miji iliyoshirikiana karibu.
  4. Kati ya miaka 223 - 187 BC, Antiocus Mkuu alizihamisha kiasi cha familia 2,000 za Kiyahudi kutoka Mesopotamia na Babeli na kuzipeleka sehemu hiyo.
  5. Jumuia ilikuwa zaidi ya Frigia iliyokuwa na mvuto zaidi wa Kiyunani.
- C. Paulo hakuanzisha kusanyiko (la kanisa) Kolosai.
1. Alikuwa “amesikia” juu ya imani - Kol. 1:4, 9.
  2. Yaelekea Epafra kutoka Kolosai alianzisha kanisa huko Kolosai, pamoja na Hierapolis na Laodikia - Kolosai 4:12, 13.
- A. Yawezekana alikuwa mwongofu wa Paulo, wakati Paulo alipokaa Efeso - Mdo. 19:10.

### **3. LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Paulo alikuwa kifungoni katika awamu ya kwanza huko Rumi - Mdo. 28:30, 31.
- B. Kifungo hicho kimewekwa katika B. K. 60 - 62.
- C. Wakolosai kiliandikwa kuelekea mwishoni mwa wakati huo - mnamo 62 B. K..

### **4. KITABU KILIANDIKWA KWA SABABU GANI?**

- A. Kanisa lilikuwa limevamiwa na maasi Kolosai.
  1. Inaelekea kulikuwa na mchanganyiko wa Falsafa ya Kiyunani, dini za Mashariki na mabaki ya dini ya Kiyahudi - Kol. 2:8 - 23.
    - A. Matokeo ya baadaye ya uasi huo yalihuisha kile kilichoitwa Gnosticism (mtazamo maalum katika imani ya dini).
  2. Wayunani na watu wa Mashariki waliona mwili kama “jela” au kifungo cha nafsi (au roho).
  3. Iliaminiwa kuwa kulikuwa na mzozo kati ya mwili na roho, na kati ya yale ya mwili na ya kiroho.
  4. Mungu ni roho, bali uumbaji ni kitu kilichoundwa au kiwezacho kutengenezwa.
    - A. Imewahi kudaiwa kuwa kwa sababu ya ukweli huo Mungu hakuweza kuumba moja kwa moja, bali viumbe vya kimalaika.
    - B. Kwa hiyo viumbe hivi vya kimalaika vilipaswa kuabudiwa - Kol. 2:18.
- B. Mwandishi alipinga uasi huo kwa kumwinua Kristo.
  1. Kama Mwumbaji wa vitu vyote - 1:16, 17.
  2. Kama Yeye aliyemkomb oa mwanadamu kwa damu yake - 1:14, 20.
  3. Kama katika Yeye wakaa ukamilifu wa uungu katika mwili 2:9.
- C. Zaidi ya hapo alielezea kwamba falsafa na mapokeo ya wanadamu hayana nafasi katika wokovu wa mwanadamu - 2:8.
- D. Sheria ya Musa iligongomewa msalabani - 2:14.
- E. Malaika ni viumbe vilivyoumbwa na havipaswi kuabudiwa.

### **5. MUHTASARI WA WAKOLOSAI.**

- A. Mambo ya utangulizi - 1:1 - 12.
- B. Mambo ya mafundisho - 1:13 - 2:3.
- C. Mambo yenye hoja - 2:4 - 23.
- D. Mambo ya vitendo - 3:1 - 4:6.
- E. Mambo ya kuhitimisha - 4:7 - 18.

### **6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA WAKOLOSAI**

- A. Ufalme umekwisha simikwa - Kol. 1:13.
- B. Ni kwa njia ya damu ya Kristo tu mtu hukombolewa - Kol. 1:14.
- C. Kichwa cha kanisa ni Kristo - 1:18.
- D. Injili ilihubiriwa duniani kote - Kol. 1:6, 23.
- E. Kristo ni mwumbaji wa kila kitu - Kol. 1:16.
- F. Ubatizo unahitaji kuzikwa na kufufuka - Kol. 2:12.
- G. Sheria ya Musa iligongomewa msalabani - Kol. 2:14.
- H. Mwanadamu anapaswa kuwa na mamlaka ya Kristo kwa lo lote alifanyalo Kol. 3:17.
- I. Maandiko ya Agano jipya yalienezwa eneo kubwa mapema sana katika historia ya kanisa - Kol. 4:16.

**MWISHO:**

1. Dini ambayo ina makosa katika nafsi (ya aliyeianzisha), asili yake, kazi na kujipambanua kwake kwa Kristo ni yenye makosa.
  - A. Haihitaji kuendelea kuichunguza zaidi.
2. Kristo ni lazima ainuliwe katika hali zote za maisha ya mtoto wa Mungu na cho chote afanyacho ni lazima kiwe kinaongozwa na Mungu - Kol. 3:14.

## **SOMO LA XVI - 1 WATHESALONIKE - UJIO WA PILI WA KRISTO.**

### **UTANGULIZI:**

1. Waraka wa kwanza kwa kanisa la Thesalonike ulikuwa ni mmojawapo katika vitabu vyatya awali katika Agano Jipyka katika kuandikwa.
  - A. Kwa sababu kiliandikwa mapema hivyo, kinatupatia mtazamo wa kanisa na matatizo yake kiasi cha miaka ishirini hivi baada ya Pentekoste.
2. Kinashughulikia kwa ukubwa zaidi kuhusu ujio wa Pili wa Kristo.

### **MJADALA:**

1. **Ni nani (NANI ALIKIANDIKA KITABU)?**
  - A. Hakuna mashaka makubwa kuhusu ukweli kuwa aliyekiandika kitabu hicho ni Paulo.
  - B. Ushahidi wa ndani unamwonesha Paulo.
    1. Mwandishi anajitaja mwenyewe kuwa ni Paulo - 1 Thes. 1:1; 2:18.
    2. Washirika wa kudumu wa Paulo wanashirikishwa na mwandishi - 1 Thes. 1:1; 3:1, 2.
    3. Mtindo na kujali kwa ajili ya kanisa kunakoonesha na Paulo kunajidhihirisha hapo ndani.
  - C. Ushahidi wa nje.
    1. Mnomo 140 B. K.. Marcion aliupokea kuwa wa Paulo.
    2. Mnomo 170 B. K.. mafundisho ya Muratorian yaliuweka nafasi ya sita kati ya nyaraka za Paulo.
    3. Mnomo 180B. K. Irene (Irenaeus) alikihusisha kitabu hicho.
    4. Clement wa Alexandria alikihusisha kitabu na sifa ya uandishi kumpa Paulo.
2. **KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**
  - A. Mji wa Thesalonike awali uliitwa “Therma” kwa sababu ya majira ya joto katika eneo hilo.
    1. Uko kwenye njia panda itokayo Rumi kwenda Mashariki na njia itokayo mto Danube kwenda bahari ya Aegean.
    2. Shemeji wa Alexander Mkuu, Cassander, alijengwa Therma mwaka 315 K. K. na kuutajia jina la mkewe.
    3. Mwaka 168 K.K. Thesalonike ulishindwa na kuwekwa chini ya Rumi na kufanywa mmoja kati ya miji mikuu ya majimbo 4 ambayo Makedonia ilikuwa imegawanywa.
    4. Baadaye ulifanywa kuwa mji mikuu wa Makedonia yote.
    5. Ulijumuisha kimsingi Wayunani, Warumi na Wayahudi.
  - B. Kanisa lilianzishwa na Paulo na Sila wakati wa safari ya pili ya Paulo ya umisionari - Mdo. 17:1-10.
    1. Paulo na Sila waliondoka mji wa Filipi baada ya kupigwa na kufungwa.
    2. Kwa sababu hakukuwa na sinagogi huko walipitia miji ya Amphipolisi na Appollonia - Mdo. 17:1.
    3. Kisha alifika Thesalonike na kuhojiana kwa muda wa siku tatu ndani ya sinagogi.
      - A. Alihubiri kifo na kufufuka kwa Kristo - Mdo. 17:3.
      - B. Wengi wa Wayunani waliomcha Mungu na wanawake wenye vyeo waliamini - Mdo. 17:4.
    4. Kundi lilichochewa dhidi ya kanisa na Wayahudi na mashitaka kuleta dhidi yao.
    5. Paulo na Sila wakaondolew a wakati wa usiku ili kuokoa maisha yao - Mdo. 17:10.
3. **LINI NA WAPI KITABU HICHO KILIANDIKWA?**
  - A. Upinzani ulikuwa umechochewa dhidi ya Paulo na wachachezi wakiwa ni Wayahudi kutoka Thesalonike waliokuja Beroya - Mdo. 17:13 - 15.

1. Paulo alisindikizw a na ndugu kwenda baharini ambako aliabiri kwenda Athene.
  2. Sila na Timotheo walibaki nyuma kwa muda mfupi.
  3. Paulo akahubiri Athene na kisha kwenda zake Korintho - Mdo. 17:16 - 18:4.
  4. Kujali kwa Paulo kwa ajili ya kanisa kule Thesalonike kulituli zwa wakati Sila na Timotheo walipoungana naye na kumletea taarifa nzuri ya uimara wao - Mdo. 18:5.
  5. Huo ndio wakati Paulo alipoandika 1 Thesalonike.
- B. Paulo alikuwa Korintho 51 B. K. na 52 B. K.
1. Baadaye katika kukaa kwake akaletwa mbele ya Galio, liwali wa himaya ya Rumi. - Mdo. 18:12.
  2. Kuna maandishi yaliyopatikana huko Delphi mwaka 1909, yakimtaja Galio na tarehe ya uliwali wake Korintho.
  3. Kwa hiyo, tunaweza kutaja tarehe ya kitabu kuwa ni mnamo 51 B. K. au 52 B. K. kwa kuwa kilikuwa kimeandikwa kutoka Korintho.

#### 4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?

- A. Paulo alitaka kuwafariji Wathesalonike Wakristo katika mateso yao - 1:1 - 10; 3:1-13.
- B. Alijitetea dhidi ya wale waliohoji huduma yake na dhamiri/nia yake - 2:1 - 20.
- C. Maagizo yaliyotolewa kuhusu maisha ya utauwa na maonyo kuukimbia uasherati - 4:1 - 12.
- D. Masahihisho yalifanywa kuhusu kutoelewa kwao juu ya ujio wa pili wa Kristo - 4:13 - 15:11.

#### 5. MUHTASARI WA 1 THESALONIKE (Wathesalonike wa I)

- A. Sifa toka kwa Paulo kwa Wakristo - Sura ya 1
- B. Jibu la Paulo kwa washitaki wake akionesha kazi zake - Sura ya 2.
- C. Shauku yake kwa kanisa na mateso yake - Sura ya 3.
- D. Ombi la Paulo kuukimbia uasherati na kwamba waishi maisha ya utauwa - 4:1-12.
- E. Mafundisho yake ujio wa pili wa Kristo - 4:13 - 5:11.
- F. Maombi ya mwisho na maonyo - 5:12 - 28.

#### 6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA 1 WATHESALONIKE

- A. Wakristo wawaige Wakristo wa Thesalonike katika kazi, upendo na uvumilivu - 1 Thes. 1:3; Gal. 5:6; Yak. 2:14 - 20.
- B. Kanisa la Thesalonike liliweka akilini mambo ya huduma ya misheni - 1:8.
- C. Wakristo wa Thesalonike walikuwa wametubu kwa nia ya kweli - 1:9.
- D. Wakristo wanahitaji kuweka kielelezo kilichowekwa na Paulo kushughulikia mambo ya mafanikio, waongofu wapya na ndugu kwa ujumla - 2:3-12.
- E. Mafundisho ya usafi wa mambo ya unyumba yahitajika leo - 4:1-8.
- F. Wakristo wanahitaji kupendana wao kwa wao - 4:9, 10.
- G. Mafundisho ya ujio wa pili:
  1. Litahusu ujio binafsi, wa kuonekana na kusikika - 4:16.
  2. Mafundisho ya "Mpasuko" (Rapture) sio ya kweli maana Wakristo watakuwa daima na Bwana - 4:17.
  3. Tukio hilo litatokea bila kutazamia.
  4. Vema kuwa tayari wakati wote - 5:6 - 11.
  5. Wito wa kuomba pasipo kukoma - 5:17.
  6. Mwanadamu sio tu wa kufa, bali ujumla wake ni mwili, nafsi na roho - 5:23.

#### MWISHO:

1. Wathesalonike wa I ni mojawapo katika maandiko ya awali ya Agano Jipya.
2. Ujio wa mara ya pili umetajwa katika kila sura ya kitabu hicho.
  - A. Kumetajwa mara 618 katika Agano Jipya.
3. Kina mafundisho ya ujio wa mara ya pili mengi zaidi ya vitabu vingine vyta Agano Jipya.

## **SOMO LA XVII - 2 WATHESALONIKE - MATUKIO YANAYOTANGULIA SIKU YA BWANA.**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu kiliandikwa punde baada ya 1 Wathesalonike.
2. Yaelekea Wakristo Wathesalonike bado hawakuwa wanaelewa ujio wa pili.
  - A. Labda wengine walidhania ulikuwa wa karibuni 2 Thes. 2:1, 2.
    1. Hiyo ilisababisha (kupelekea) wengine kuacha kufanya kazi - 2 Thes. 3:6-12.
3. Kanisa lilikuwa bado linaendelea na maudhi (kuudhiwa) makubwa.
4. Akaamua kusahihisha mafundisho mapotofu waliyopewa (kukanganywa kuelewa) kuhusu ujio wa pili na kuwapa moyo waimarike.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIANDIKA KITABU?**

- A. Ushahidi wa ndani unaonesha aliyeandika ni Paulo.
  1. Mara mbili mwandishi ajitaja kuwa ni Paulo - 2 Thes. 1:1; 3:17.
  2. Msamiati na mtindo vinaonesha ni vya Paulo.
  3. Wengine wanadai ni habari ya kughushi
    - A. Wanadai kwamba kwa vile yafanana sana na 1 Thesalonike lazima iwe ni ya kughushi.
    - B. Wengine wanadai kwa vile Waraka huo ni mkali zaidi kuliko ule wa kwanza, basi ni wa kughushi.
      1. Hata hivyo, hakuna uthibitisho katika hayo yote mawili.
- B. Ushahidi wa nje umhusishao Paulo ni mkubwa.
  1. Ametajwa katika mafundisho ya Didache mnamo 100 B. K.
  2. Mnamo 110 A.D. Ignatius aonekana kuhusisha mafundisho hayo.
  3. Pia Justin Martyr na Polycarp walihusisha katika mafundisho hayo katikati ya karne ya pili.
  4. Mnamo 180 A.D. Irene (Irenaeus) anahuisha mafundisho ya kitabu hicho kwa kumhusisha Paulo kama mwandishi.
  5. Clement wa Alexandria na Tertullian wote walinukuu 2 Wathesalonike, huyo Tertullian akimhusisha Paulo kuwa ndiye mwandishi.

#### **2. KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**

- A. Kimeandikwa na Paulo na wenzake Sila na Timotheo kwa kanisa la Thesalonike - 2 Thes. 1:1.
- B. Kanisa lilian zishwa na Paulo na Sila wakati wa safari yake ya pili ya umisionari - Mdo. 17:1-10.
  1. Mji wa Thesalonike uliitwa hapo kwanza "Therma" kwa sababu ya nyakati za joto eneo hilo.
    - A. Ulikuwa penye makutano ya njia kuu itokayo Rumi kwenda Mashariki na njia ilikatiza toka mto Danube kwenda bahari ya Aegean.
    - B. Shemeji wa Alexander Mkuu, Cassander, aliujenga upya Thema mwaka 315 B.C. na kuutajia kwa jila la mkewe.
    - C. Mwaka 168, Thesalonike ulishindwa katika vita kwa Rumi na kufanya mji mkuu mmojawapo katika majimbo manne ambayo Makedonia ilikuwa imegawanywa.
    - D. Baadaye ulifanywa kuwa mji mkuu wa nchi nzima ya Makedonia.
    - E. Uliwajumuisha kimsingi Wayunani, Warumi na Wayahudi.

#### **3. KITABU KILIANDIKWA LINI NA WAPI?**

- A. Paulo alikuwa bado Korintho alikoandika 1 Wathesalonike - Mdo. 18:1, 5.  
 1. 2 Wathesalonike kiliandikwa punde baadaye.

**4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Maudhi dhidi ya kanisa yalikuwa yamefikia hali mbaya zaidi hivyo Paulo aliandika kuwapa moyo - 2 Thes. 1:4 - 12.  
 B. Mafundisho yake kuhusu ujio wa pili ama hayakuelewaka au yalipotoshwa.  
 1. Inawezekana walipokea barua iliyoghushiwa ikidaiwa kutoka kwa Paulo, ambayo ilisababisha kutoyaelewa mafundisho yake - 2 Thes. 2:1, 2.  
 2. Wengi walikuwa wanatazamia ujio wa mara ya pili kutokea dakika yo yote - 2 Thes. 2:3.  
 3. Aliwahakikishia kwamba kuanguka na kufunuliwa yule mwenye uasi (mwenye ukengeufu) hakuna budi kutokea kwanza - 2 Thes. 2:3, 4.  
 C. Wengine waliacha kufanya kazi kwa kudhani Bwana alikuwa anakuja punde - 2 Thes. 3:6-12.

**5. MUHTASARI WA 2 THESALONIKE.**

- A. Salamu, kutakiana hali na shukurani kwa sababu ya imani yao - 1:1-3.  
 B. Kuwasihii kujipa moyo na kuwa imara katika mateso - 1:4-12.  
 C. Kuanguka na ujio wa yule asi ukitabiriwa - 2:1-12.  
 D. Shukurani zaidi na kupeana moyo kwa uimara wao - 2:13-17.  
 E. Ombi la Paulo kuomba kwa niaba yake - 3:1-5.  
 F. Nidhamu juu ya waishio bila utaratibu yaamuriwa - 3:6-15.  
 G. Kufunga - 3:16-18.

**6. MAFUNZO TUYAPATAYO TOKA 2 WATHESALONIKE .**

- A. Wale wasiomjua Mungu na wasioitii injili wamepotea 2 Thes. 1:7-9; Mk. 16:16; Tit. 1:2.  
 B. Kazi imeamuriwa na Mungu - Mwa. 2:15; Efe. 4:28; 2 Thes. 3:8 - 12.  
 C. Nidhamu ya kanisa yapaswa kutendwa - 2 Thes. 3:6, 12 - 15.  
 D. Kukengeuka na kufunuliwa kwa yule asi (mtu wa dhambi) ni lazima kutokee kabla ya ujio wa pili wa Kristo.  
 1. Yaliyoandikwa kuhusu yule mtu/nafsi ya dhambi:  
 A. Hujikweza juu ya cho chote kitajwacho Mungu na kukaa ndani ya hekalu lake - 2:4.  
 B. Ataendelea hadi ujio wa pili - 2:8.  
 C. Anaaminiwa kwa sababu ya nguvu ya shetani ishara zake na uongo wake - 2:9.  
 D. Huwadanganya watu wasioupenda ukweli - 2:10-12.  
 2. Mawazo kuhusu “nafsi/ mtu huyo”.  
 A. Shetani.  
 B. Myahudi asiyé mwaminifu.  
 C. Taifa la Wayahudi.  
 D. Mfalme wa himaya ya Warumi.  
 E. Himaya ya Warumi.  
 F. Upapa au Papa wa Rumi.  
 G. Hitler, Mussolini, Stalin au kiongozi mwingine wa kisiasa.  
 H. “Mpinga Kristo” ajaye.  
 I. Makao ya Mason (Masonic Lodge).  
 J. Kuinuka kwa Eukemeni (Ecumenical Movement).  
 K. Msimamo usiojali sheria au utauwa.  
 3. Wazo linaloshikiliwa na wengi ni Upapa.  
 A. “Kile kinachozuia” ni himaya ya Kirumi ambayo ilizuia Papa kuinuka wakati wa himaya hiyo.

- B. Ujio wa upotofu ni maasi makubwa ya kanisa yaliyopelekea kuja kwa Kanisa la Rumi.
- C. Mtu wa kuasi angekaa katika "Hekalu la Mungu".
  - 1. Yaani kanisa - 2 Thes. 2:4.
- D. Mtu wa kuasi angempinga Mungu na kujiinua mwenyewe.
  - 1. Imekuwa ni kweli Papa wamejiinua na kukalia viti vya enzi na majina ya Mungu wamejibandika.
- E. Mtu wa kuasi angedanganya na ishara za uongo.
- F. Mtu wa kuasi angeendelea hadi ujio wa Mara ya Pili.

**MWISHO:**

- 1. Kitabu kinahusisha mojawapo ya mafundisho yaliyo ya wazi zaidi juu ya ujio wa pili.
- 2. Kinapinga mawazo yaliyoshikiliwa kwamba Agano Jipya lilifundisha kwamba Yesu Kristo angekuja wakati wa uhai wa mitume.

## **SOMO LA XVIII - 1 TIMOTHEO - MISINGI YA VITENDO KWA WAHUBIRI**

### **UTANGULIZI:**

1. Nyaraka za 1 Timotheo na 2 Timotheo na Tito hutajwa kwamba ni “Nyaraka za
  - A. Jina la vitabu hivyo hutokea kutokana na mkanganyo wa neno, “mchungaji”
  - B. “Mchungaji” ni neno litokalo katika mchunga mifugo.
  - C. Wazee wa Kanisa, sio wahubiri, ndio wachunga kundi - Mdo. 20:28; Efe. 4:11; 1 Pet. 5:1 - 4.
  - D. Watu wa madhehebu kwa makosa huwataja wahubiri wao ni “Wachungaji”.
  - E. Hiyo ndiyo iliyopelekea madhehebu kuzitaja nyaraka hizo, “Nyaraka za Uchungaji”.
2. Vema zaidi kuziita Nyaraka za Uinjilisti kwa sababu zinashughulikia kazi ya mwinjilisti.

### **MJADALA:**

1. **NANI ALIANDIKA KITABU?**
  - A. Ushahidi wa ndani una nguvu ukimtaja Paulo.
    1. Waraka unadai mwandishi ni Paulo - 1 Tim. 1:1.
    2. Kumbukumbu nyingi zinazomtaja Paulo na Timotheo zinaonesha Paulo ndiye mwandishi.
  - B. Ushahidi wa nje unaelekeza kwa Paulo.
    1. Mnamo 200 A.D. Clement wa Alexandria alitangaza uliandikwa na Paulo.
    2. Tertullian, aliyeishi karibu wakati huo huo alinukuu toka kitabu hicho na kutaja kuwa mwandishi ni Paulo.
    3. 1 Timotheo, 2 Timotheo na Tito viliorodheshwa katika vile vitabu vyta Paula (nyaraka) katika kumbukumbu za Muratorian (A.D. 170) na katika tafsiri za zamani za Kilatini na Syriac.
  - C. Wenye msimamo huria wa kisasa wanakana kuwa Paulo ndiye mwandishi.
    1. Wanadai kwamba 1 Timotheo, 2 Timotheo na Tito haviwezi kuingia katika maelezo ya taabu ya Paulo ambayo imenukuliwa katika kitabu cha Matendo.
      - A. Ushahidi imara wa kihistoria kwamba Paulo aliachiliwa kutoka kifungo cha Rumi baada ya miaka miwili.
      - B. Alikamatwa na kuuawa baadaye kidogo, kipindi hicho kingeweza kutumika kufanya hivyo.
    2. Wanadai kwamba maneno yaliyomo katika nyaraka hizo hayamo katika zile nyingine zilizoandikwa na Paulo.
      - A. Wanashindwa kuliangalia jambo hilo, kwamba mahali na muda hurekebisha mtindo na msamiati.
      - B. Hizi zilikuwa nyaraka za vitendo kwa mhubiri mwingine, aliyekuwa mwana katika imani.
        1. Si maelekezo ya kidini (au Kanuni).
      - C. Alikuwa ni mtu mwenye elimu akiwa na uwezo wa kutumia msamiati mpana aliokuwa nao.
    3. Wanadai kwamba 1 Timotheo, 2 Timotheo na Tito lazima viwe viliandikwa na mtu mwingine kwa sababu vinawakilisha kanisa lililokuwa limeendelea, ambalo lilikuwa halijatokea.
      - A. Yaelekeea hawa watu hawaelewi kwamba kanisa ni chombo cha Mungu kilichojengwa kwa mpango ulioundwa na Yeye mwenyewe.
      - B. Kanisa la Yerusalemu lilikuwa na wazee wake lenyewe - Mdo. 11:30.
      - C. Paulo aliwachagua wazee wa kanisa katika makanisa aliyoaanzisha katika safari yake ya kwanza ya umisionari - Mdo. 14:23.
  2. **KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**
    - A. Kwa Timotheo, mwana wa Paulo katika imani - 1 Tim. 1:2.
    - B. Mengi yamefunuliwa kuhusu Timotheo.
      1. Mwenyeji wa Listra - Mdo. 16:1.

2. Babaye alikuwa Myunani - Mdo. 16:1 - 3.
3. Mamaye alikuwa Myahudi - Mdo. 16:1.
4. Alifundishwa Maandiko na mama yake na bibi yake katika miaka ya mwanzoni (katika umri) - 2 Tim. 1:5; 3:14,15.
5. Alichaguliwa na Paulo katika safari ya pili ya Paulo ya umisionari kuwa mmisionari - Mdo. 16:1 - 3.
6. Alipewa kipawa cha miujiza na Paulo - 2 Tim. 1:6.
7. Unabii ulizungumza juu yake - 1 Tim. 1:18.
8. Alitazamwa kuwa ni "kijana" lakini Warumi walimwona kila mtu mwenye umri kati ya miaka 18 na 40 kuwa ni kijana - 1 Tim. 4:12.
9. Alionekana kuwa na matatizo ya tumbo pamoja na matatizo mengine ya afya - 1 Tim. 5:23.
10. Alifungwa kwa sababu ya kuwa Mkristo - Ebr. 13:23.

### **3. KITABU KILIANDIKWA LINI NA WAPI?**

- A. Kitabu cha Matendo kilihitimishwa na kufungwa kwa Paulo Rumi - Mdo. 28.
  1. Kufungwa kulidumu miaka miwili - Mdo. 28:30, 31.
  2. Paulo aliandika "Nyaraka za Kifungoni" wakati huo wa kufungwa - Efe. 4:1; 6:20; Flp. 1:13; Kol. 4:3, 10; Flm1, 9, 10, 22.
  3. Paulo alionesha matarajio yake kuwa angeruhusiwa - Flp. 1:25; Flm. 22.
  4. Katika 2 Tim. hapaoneshi tumaini la kuachiwa bali kifo - 2 Tim. 4:6 - 8.
  5. Paulo alipanga kuitembelea Rumi katika safari yake kwenda Hispania - Rum. 15:24.

### **MWISHO:**

1. A. Kulikuwa na nyakati mbili za ufungwaji (mtume).
  - B. Paulo aliachiliwa huru baada ya kifungo cha kwanza.
  - C. Alikwenda Hispania kama alivyopanga.
  - D. Baadaye alifungwa tena.
  - E. Aliandika 2 Timotheo muda mfupi kabla ya kifo chake.
2. 1 Timotheo huenda kiliandikwa wakati Paulo alipokuwa akitembelea makanisa aliyoyaanzisha kabla ya kufungwa kwake kwa kwanza.
  - A. Mahali ulipoandikwa waraka huo, hakuna uhakika.
  - B. Yawezekana uliandikwa Makedonia.
3. Tarehe yakuandikwa, yawezekana sana B.K. 64 au 65.
  - A. Aliachiliwa toka kifungo cha kwanza B.K. 61 & 62.
  - B. Yawezekana alitumia miaka miwili Hispania na mwaka mwagine akiyatemebelea makanisa kabla ya kufungwa tena.

### **4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Matatizo ya mafundisho yalikuwa yanababisha matatizo katika kanisa.
  1. Timotheo alibaki Efeso ili aweze "kuwaonya baadhi yao wasifundishe mafundisho mengine" - 1 Tim. 1:3
- B. Matatizo yalikuwa ni mchanganyiko wa mafundisho ya dini ya Kiyahudi na falsafa ya Kiyunani.
  1. Mabishano juu ya vizazi na nasaba - 1:4.
  2. Wengine walitamani wawe walimu wa Sheria - 1:5 - 10.
  3. Wengine walitaka kuweka sheria mahali ambapo Mungu hakuweka sheria hiyo - 4:1 - 5.
- C. Timotheo aliamuriwa kwa maagizo maalum juu ya namna ya kuenenda katika kanisa - 1 Tim. 3:14, 15.
  1. Wajibu wa wanaume na wanawake umeainishwa - Sura ya Pili.

2. Sifa za wazee wa kanisa na mashemasi - Sura ya 3.
  3. Timotheo alielekezwa jinsi ya kuenenda yeye mwenyewe.
  4. Taratibu kuhusu wajane zilitolewa - 5:1 - 16.
5. **MUHTASARI WA 1 TIMOTHEO.**
- A. Ukiukaji wa mafundisho ni lazima ushughulikiwe - Sura ya 1.
  - B. Wajibu wa wanaume na wanawake - Sura ya 2.
  - C. Sifa za Wazee wa kanisa na mashemasi - Sura ya 3.
  - D. Wajibu na mwenendo wa mtumishi mwema - Sura ya 4.
  - E. Msimamo wa vitendo kwa ajili ya kazi ya kanisa - Sura aya 5.
    1. Sifa za wajane ambao wangeandikishwa - mist. 1 - 16.
    2. Mwenendo mbele za wazee wa kanisa na wengineo umejadiliwa - mist. 17 - 25.
  - F. Msimamo wa vitendo kwa ajili ya watu wa Mungu watolewa - Sura ya 6.
    1. Maonyo kwa watumishi - mist. 1 - 5.
    2. Maonyo kwa matajiri - mist. 6 - 19.
    3. Maonyo ya kufungia kwa Timotheo - mist. 20 na 21.
6. **MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA 1 TIMOTHEO.**
- A. Kanisa litaendelea kusumbuliwa na walimu wapotofu - Mdo. 20:26 - 32; 1 Tim. 1:3 - 11; 4:1 - 5.
  - B. Watu wamepewa wajibu wa uongozi katika kazi za jumuia na ibada ya kanisa - 1 Tim. 2:1 - 15.
  - C. Wanawake wawe na mavazi ya staha na wajifunze wakiwa kimya.
  - D. Wazee wenye sifa na mashemasi wenye sifa wanahitajika - 1 Tim. 3.
  - E. Ni vibaya kufunga pale ambapo Mungu amefungua na kufunga pale ambapo amefunga - 1 Tim. 4:1 - 5.
  - F. Wazee na waangaliwe (watunzwe) na watoto wao - 1 Tim. 5:16.
  - G. Wazee watumikao kikamilifu wasaidiwe na kanisa - 1 Tim. 5:17, 18.
  - H. Utajiri wa dunia hauna thamani - 1 Tim. 6:5 - 19.

**MWISHO:**

1. Sehemu mbali mbali za kazi za kanisa yapasa zishughulikiwe na wale ambao Mungu amekusudia wafanye hivyo.

## SOMO LA XIX - 2 TIMOTHEO - WARAKA WA MWISHO WA PAULO

### **UTANGULIZI:**

1. Nyaraka za 1 Timotheo, 2 Timotheo na Tito kwa kawaida zinaitwa, “Nyaraka za Uchungaji”
  - A. Sio sahihi kwa sababu vitabu hivyo viliandikwa kwa wahubiri badala ya wazee wa kanisa, ambao ndio wachungaji.
  - B. Ni sahihi zaidi kuvitaja “Nyaraka za Uinjilisti”.

### **MJADALA:**

#### 1. NANI ALIKIANDIKA KITABU HICHO?

- A. Kwa ujumla imekubaliwa kuwa kiliandikwa na Paulo.
  1. Kiliandikwa na mtu yule yule kama 1 Timotheo, na Tito.
- B. Ushahidi wa ndani unaonesha kuwa mwandishi ni Paulo.
  1. Mwandishi anadai kuwa ni mtume Paulo - 2 Tim. 1:1.
  2. Kumbukumbu nyingi za watu na sehemu zilizomhusisha Paulo zaonesha kuwa yeze ndiye mwandishi.
- C. Ushahidi wa nje una nguvu ukimhusisha Paulo.
  1. Amehusishwa Paulo na Ireneaus (Irene) na Clement wa Alexandria.
  2. Waraka huo umeorodheshwa katika nyaraka za Paulo kwenye mafundisho ya Muratorian na tafsiri za zamani za Kilatini na Syriac.

#### 2. KITABU HICHO ALIANDIKIWA NANI?

- A. Kwa “Timotheo mwanangu mpewda 2 Tim. 1:2.
- B. Yaonekana kwamba Timotheo alikuwa ni sahibu wa karibu zaidi na mpewda zaidi wa Paulo.
  1. Timotheo alikuwa mwenyeji wa Listra - Mdo. 16:1 - 3.
  2. Baba alikuwa Myunani na Mama alikuwa Myahudi Mdo. 16:1 - 3.
  3. Mama na bibi yake walikuwa waumini waliomfundisha Timotheo Maandiko toka mwanzoni mwa maisha yake - 2 Tim. 1:5; 3:14, 15.
  4. Kulikuwa na maisha ya ujirani sana na Paulo hata katika sehemu ya mwisho ya maisha yake Paulo.

#### 3. LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA?

- A. 2 Timotheo kiliandikwa wakati Paulo akiwa Rumi.
  1. Alikuwa kifungoni - 1:7, 8, 16, 17.
  2. Alikuwa amekwisha tokeo mbele za Kaisari - 4:6.
  3. Alikuwa akisubiri hukumu yake kutolewa.
  4. Alikuwa akitazamia kufa karibuni kwa sababu ya imani yake - 4:6 - 8.
- B. Kulikuwa na vifungo vya Paulo viwili kule Rumi.
  1. Cha kwanza ni cha miaka miwili - Mdo. 28.
    - A. Akiwa huko aliandika Waefeso, Wafilipi, Wakolosai na Filemoni.
    - B. Alitazamia kuachi wa huru - Wafilipi 1:25; Filemoni 22.
    - C. Aliachiwa kwa kipindi na akahubiri Hispania - Rum. 15:24.
    - D. Yasemekana baadaye alizuru Asia na Uyunani na kisha akakamatwa wakati wa utawala wa Nero na kuteswa.
- C. Wakati wa kifungo chake cha pili huko Rumi aliandika 2 Timotheo.

1. Nero alijuua Juni 8, 68 B. K.
2. Kwa hiyo, 2 Timotheo yamkini kiliandikwa mwishoni mwa 67 B.K. au mapema 68 B. K., muda mfupi kabla Paulo hajauawa.

**4. KWA NINI KITABU HICHO KILIANDIKWA ?**

- A. Paulo alikuwa tayari amezeeka na akiwa amejitoa mhanga katika mambo mengi kwa ajili ya Kristo.
  1. Alikuwa karibu kufariki kwa sababu ya imani yake.
  2. Wengi wa wale waliokuwa marafiki zake walikuwa wamemwacha - 4:10 - 12.
  3. Timotheo alikuwa mpendwa wake mkuu - 1:2.
  4. Alipenda amwone Timotheo mara moja tena kabla hajafa.
- B. Kanisa lilikuwa katika matatizo kwa muda huo na Paulo alifahamu hilo.
  1. Walimu wengi wa uongo walikuwa wanaingia katika kanisa na hali kuendelea kuwa mbaya - 1:15; 2:16-18; 3:1-9, 13.
  2. Timotheo alihitaji kujandaa kwa ajili ya mateso ambayo yalikuwa yanakuja.
    - A. Paulo alimpa moyo Timotheo asimwonee haya yeye au Bwana - 1:8, 12.
    - B. Alimpa moyo Timotheo kuvumilia mateso (au mambo magumu) kama askari mwema. 2:3.
    - C. Paulo alitahadharisha kwamba wote ambao wangeishi maisha ya utauwa wangepata mateso. 3:12.
- C. Ilikuwa muhimu kwa Timotheo kumsaidia huduma Paulo katika mahitaji ya kawaida.
  1. Timotheo alihitajiwa ampelekee Paulo koti, vitabu (na vya ngozi) ambavyo alikuwa ameviacha Troa, na alikuwa anavihit aji - 4:13.
  2. Paulo alimtaka Timotheo afike kabla ya majira ya baridi 4:21.

**5. MUHTASARI WA 2 TIMOTHEO:**

- A. Salaamu na kujuliana hali - 1:1 - 3.
- B. Ombi la kuwa imara na kustahimili - 1:4 - 2:13.
- C. Maelekezo kuhusu tabia ya kibinagsi - 2:14 - 26.
- D. Onyo kuhusu ujio wa ukengeufu - 3:1 - 9.
- E. Mafunzo ya awali ya Timotheo - 3:10 - 17.
- F. Kumpa moyo Timotheo kuhubiri Neno kwa sababu nyakati mbaya zilikuwa zinakuja - 4:1 - 8.
- G. Maagizo ya binafsi na salaamu 4:9 - 22.

**6. TUJIFUNZAYO TOKA 2 TIMOTHEO:**

- A. Umuhimu wa mafunzo ya awali nyumbani - 1:5; 3:14, 15.
- B. Onesforo alivyoonesha mfano mzuri pasipo woga wala haya. - 1:16-18.
- C. Umuhimu wa kuwataja walimu wa uongo ili wengine watahadharishwe - 1:15; 2:17, 18.
- D. Umuhimu wa kulitumia Neno kwa halali - 2:15.
- E. Wakristo wanaweza kutazamia kuteseka kwa ajili ya imani yao - 3:12; Mdo. 14:22; Lk. 6:26.
- F. Maandiko ni uvuvio wa Mungu na yanatosha kwamba ni ufunuo wa Mapenzi ya Mungu - 3:15-17.
- G. Umuhimu na ulazima wa kuendelea kudumu kuhubiri Neno - 4:1-5.
- H. Tumaini lililowekwa tayari kwa Wakristo waaminifu waupendao ujio wa Bwana - 4:6-8.

**MWISHO:**

1. Kitabu hicho ni cha mwisho katika nyaraka za Paulo za uvuvio.
2. Uliandikwa kwa rafiki yake na mtenda kazi mwenzake.

3. Kuwapa moyo Wakristo kutenda kazi katika hali yo yote.
4. Wakristo waaminifu wanaweza kupambana na kifo kwa furaha kama alivyofanya Paulo - 4: 6 - 8.

## **SOMO LA XX - TITO - KULIWEKA KANISA KATIKA UTARATIBU**

### **UTANGULIZI:**

1. Kama ilivyofah amika awali, 1 na 2 Timotheo na Tito vimekuwa vikitajwa kuwa (kama) "Nyarakaka za Uchungaji".
2. Ni sahihi zaidi kuziita Nyarakaka za Uinjilisti kwa sababu ziliandikwa kwa wainjilisti.
3. Kufuatana na muda zilipoandikwa zilikuwa ni za mwisho kuandikwa na Paulo.
4. Ni nyarakaka za utendaji wa kusudi la pande tatu:
  - A. Kutoa maelekezo juu ya muundo, kazi na ibada ya kanisa lilipo.
  - B. Kuwapa maelekezo na kuwatia moyo wahubiri.
  - C. Kuwaonya watu juu ya walimu wapotofu na uasi ambaa ulikuwa unakuja.

### **MJADALA:**

1. Nani alikiandika kitabu hicho?
  - A. 1 na 2 Timotheo na Tito huhesabika kuwa ni kitu cha pamoja.
    1. Paulo ndiye mwandishi wa vyote vitatu.
    2. Mambo yanaonesha Paulo ndiye mwandishi wa 1 na 2 na vivyo hivyo kwa Tito.
  - B. Paulo anadai kuwa ndiye mwandishi - 1:1
    1. Kimeandikwa katika mtindo ule ule kama nyarakaka nyingine za Paulo.
    2. Hutaja watu, mahali na matukio ambayo yanakubaliana na jinsi tumjuavyo Paulo katika kumbukumbu nyingine za Agano Jipy.
2. **KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**
  - A. "...Tito mwanangu, hasa katika imani tuishirikiyo," 1:4.
  - B. Mengi yanaweza kufahamika kuhusu Tito kutoka kumbukumbu ndani ya Agano Jipy.
    1. Katika kitabu cha Matendo hajatajwa kwa jina.
      - A. Hata hivyo, kutoka katika Wagalatia tunaona alisafiri na Paulo na Barnaba kwenda kwenye mkutano wa Yerusalem kujadili suala la tohara - Gal. 2:1, Mdo. 15.
    2. Alikuwa Myunani ambaye kwa namna fulani aliingizwa katika shauri la mambo ya tohara - Gal. 2:3 - 5.
    3. Alikuwa mwana wa Paulo katika imani - Tit. 1:4.
    4. Anaweza kuwa alitoka Antiokia ya Shamu kwa sababu Paulo alimchukua kwenda Yerusalem kutokea Antiokia ya huko - Mdo. 15:2; Gal. 2:1.
    5. Alikuwa ni rafiki wa karibu na mmisionari mwenzake Paulo.
    6. Anatajwa kwa jina angalau mara 9 katika 1 Kor. na 2 Korintho.
    7. Paulo alimtuma Korintho kupanga utaratibu wa makusanyo kwa ajili ya maskini - 2 Kor. 8:16, 17; 12:18.
    8. Anaweza kuwa ndiye aliyebeba barua ya Paulo ya kwanza kuipeleka Korintho - 2 Kor. 7:12 - 16.
    9. Ndiye aliyeichukua barua ya 2 Kor. 12:17 - 21.
    10. Aliongozana na Paulo katika safari ya umisionari kwenda Krete na kubaki huko kukamilisha kazi - 1:5; 3:12.
    11. Alipokutana na Paulo Nikapoli, Artema au Tikiko alitumwa kuchukua nafasi yake - 3:12.
    12. Alikuwa na Paulo wakati wa kifungo chake cha mwisho na alitumwa Dalmatia - 4:10.
  3. **LINI NA WAPI KITABU HICHO KILIANDIKWA ?**

- A. Kama ilivyotajwa awali kulikuwa na kufungwa kwa Paulo nyakati mbili huko Rumi.
  - 1. Paulo aliachiliwa huru baada ya miaka miwili kutoka kile cha kwanza - Mdo. 28:30, 31; Flp. 1:25; Flm. 22.
  - 2. Baada ya hapo alihubiri Hispania, akatembelea makanisa ya Asia na Uyunani, alifanya kazi Krete na akakamatwa tena wakati wa mateso kipindi cha utawala wa Nero.
- B. Waraka waweza kuwa uliandikwa wakati wa kati ya vifungo hivyo viwili.
  - 1. Kwa hiyo, ni kipindi kile kile kama 1 Timotheo na 2 Timotheo.
  - 2. Yawezekana mnamo 66 au 67 B.K..
- C. Yawezekana kiliandikwa Nikapoli, mji wa bandari ya bahari ya Adriatic kiasi cha maili 150 kaskazini magharibi mwa Korintho katika Uyunani - 3:12.

#### **4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA ?**

- A. Paulo na Tito walikuwa wamefanya kazi mionganoni mwa makanisa ya Krete.
  - 1. Krete kilikuwa ni kisiwa upande wa mashariki mwa bahari ya kati Mediterranean Sea).
    - A. Hakutajwi jambo la uanzishwaji wa makanisa huko.
    - B. Yawezekana yalianzishwa na Wayahudi walioongoka wakati wa Pentekoste Yerusalem - Mdo. 2:7-11.
- B. Makanisa ya Krete yanaonekana yalikuwa yakiyumba.
  - 1. Yalikosa uongozi - 1:5.
  - 2. Walimu wa uongo walikuwa wakivuruga kanisa - 1:9-16.
  - 3. Yaonekana kwamba wenyeji wa Krete walielekea kuyumba, wasioaminika, hali iliyochukuliwa na kuingizwa kanisani na kusababisha matatizo ya kanisa.

#### **5. MUHTASARI WA KITABU CHA TITO.**

- A. Salaam - 1:1 - 4.
- B. Habari ihusuyo kuchaguliwa na sifa za wazee wa kanisa - 1:5-9.
- C. Maelezo kuhusu walimu wa uongo na mafundisho yao - 1:10-16.
- D. Mambo yahusuyo mafundisho yenyeye uzima 2:1-15.
  - 1. Maelekezo kwa watu wanaume wazee - 2:1, 2.
  - 2. Maelekezo kwa wanawake wazee - 2:3-5.
  - 3. Maelekezo kwa vijana wanaume - 2:6-8.
  - 4. Maelekezo kwa watumwa - 2:9, 10.
  - 5. Sababu ya kuishi maisha ya haki ni neema ya Mungu - 2:11.
- E. Taratibu saba za maisha ya haki - 3:1, 2.
- F. Hali saba zinazojipambanua kwa wasioongoka 3:3.
- G. Wokovu kwa njia ya neema - 3:4 - 8.
- H. Kuwashughulikia waasi - 3:9-11.
- I. Maagizo ya mwisho - 3:12-15.

#### **6. MASOMO TUJIFUNZAYO KATIKA KITABU HICHO.**

- A. Kusudi la Mungu ni kwamba makanisa yaongozwe na watu wenye sifa (wazee wa kanisa wenye sifa) - 1:5-9; 1 Tim. 3:1-7; Mdo. 14:23.
- B. Ni lazima kwamba wazee wa kanisa wawe tayari kuwajibu walimu wapotoshaji - 1:9-11.
- C. Watu wawe ni mfano (kielelezo) kwa maisha wanayoishi - 2:1, 2.
- D. Wajibu wa wanawake wazee ni wa pande mbili:
  - 1. Kuwa kielelezo - 2:3.

2. Kuwafundisha wanawake vijana kuhudu familia zao - 2:4, 5.
- E. Mkristo, aliyeokolewa na neema ya Mungu akatae tamaa ya dunia - 2:11, 12.
- F. Walimu wa uongo waonywe na kukataliwa - 3:10, 11; Rum.16:17.

**MWISHO :**

1. Tunajifunza mengi kuhusu siku za mwisho za maisha ya Paulo kutoka katika mafundisho ya kitabu cha Tito na nyaraka zake kwa Timotheo.

## SOMO LA XXI - FILEMONI - BARUA YA KIBINAFSI TOKA KWA MTUME.

### **UTANGULIZI:**

1. Waraka huu ndio mfupi kuliko nyaraka zake zote.
2. Ndio pekee wa kibinafsi katika nyaraka zake ulihifadhiwa.
3. Filemoni (aliyeandikiwa) alikuwa Mkristo na alimiliki mtumwa.
  - A. Unashughulikia suala la mtumwa wake aliyetorok, Onesmo, aliyeongolewa na Paulo na alikuwa anarejeshwa kwa Filemoni.
    1. Histori yakadiria kwamba kulikuwa na watumwa 60,000,000 katika himaya ya Kirumi kipindi cha karine ya kwanza.
    2. Mtu aliweza kuwa mtumwa katika moja ya njia tatu:
      - A. Kuzaliwa kwa wazazi amba walikuwa watumwa.
      - B. Kukamatwa vitani.
      - C. Kuuzwa utumwani kwa sababu ya kuwiwa (deni).
  - B. Warumi waliomiliki watumwa walikuwa na mamlaka ya uhai na kifo juu ya watumwa wao.
4. Waraka huo (Filemoni) ni mmojawapo kati ya nyaraka za “Paulo za kifungoni”.
  - A. Ziliandikwa katika kipindi cha kufungwa kwake kwa mara ya kwanza kule Rumi. - Mdo. 28:30, 31.
  - B. Hizi ni: Waefeso, Wafili pi, Wakolosai na Filemoni.
5. Waraka huu umeitwa, “umahiri wa uadilifu na maombezi ya Kikristo”.

### **MJADALA:**

1. **NANI ALIANDIKA KITABU HICHO?**
  - A. Mwandishi anajitaja mwenyewe mara tatu kama ni Paulo - 1, 9, 19.
    1. Akiwa amefungwa Rumi. - 1, 20, 22.
    2. Washiriki wa mwandishi ni: Timotheo, Epafra, Marko, Aristako, Dema na Luka wote wanajulikana walikuwa washiriki wa Paulo - 1, 23, 24.
  - B. Ushahidi wa nje unamwonesha Paulo
    1. Waandishi kama Tertullian na Origen walionesha kwamba Paulo aliandika Waraka kwa Filemoni.
    2. Ulitokea kati ya nyaraka za Paulo na katika mafundisho ya Marcion, Muratorian na yale ya Kilatini cha zamani na tafsiri za zamani za Syriac.
2. **KITABU HICHO ALIANDIKIWA NANI?**
  - A. Aliandikiwa Filemoni.
    1. Ameelezwa kama mtendakazi mwenzaki na Paulo aliyependwa naye - mst. 1.
    2. Aliongoka kwa Kristo kwa njia ya Paulo - mst. 19.
    3. Mkazi wa Kolosai - Kol. 4:7-18.
    4. Yamkini alikuwa mtu tajiri.
      - A. Alimiliki watumwa.
      - B. Kanisa lilikutana nyumbani mwake - mst. 2.
  - B. Pia aliandikiwa Afia, Arkipo na kanisa - mst. 2.
    1. Afia anasadikiwa kuwa alikuwa mke wa Filemoni.
    2. Arkipo anasadikiwa alikuwa mwanawawe Filemoni - Kol. 4:17.
3. **LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA ?**

- A. Kiliandikwa Rumi wakati Paulo akiwa kifungoni Mdo. 28:30, 31; Kol. 4:7 - 18; Flm. 1, 9, 10, 22 - 24.
- B. Yamkini Tikiko ndiye aliyechukua waraka huu kwa sababu ndiye aliyebeba waraka kwa kanisa la Kолосаі - Kol. 4:7-9.
- C. Hilo lingeweza kuweka tarehe ya kuandikwa waraka huo kuwa 62 B. K.. Wakati huo huo na Kitabu cha Kолосаі kilipoandikwa.

#### **4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Onesmo alikuwa ametoroka toka kwa mmiliki wake - Filemoni.
  - 1. Onesmo - maana yake "Faida".
  - 2. Alimfanya kosa bwana wake, labda kwa kuiba toka kwa bwana wake - mst. 18.
  - 3. Alisafiri kwenda Rumi.
  - 4. Akaja kukutana na Paulo na akaongoka - mst. 10.
- B. Onesmo alikuwa anarudishwa kwa bwana wake Filemoni kwa njia ya Paulo.
  - 1. Paulo alipenda Onesmo acae naye, lakini kwa ruhusa ya Filemoni - mst. 11 - 14.
  - 2. Paulo alijua kuwa Filemoni alikuwa na haki kisheria kumwadhibu Onesmo.
    - A. Kwa hiyo akawa anamwombea kwa niaba yake.
      - 1. Badala ya kutoa amri, jambo ambalo angeweza kulifanya badala yake akawa anaomba kwa Filemoni - mst. 8-10.
    - B. Kwa maoni ya Paulo ilikuwa ni bahati kubwa kwamba Onesmo alitoroka na kuweza kuwa Mkristo - mst. 15,16.
      - 1. Kwa yeye kufanya hivyo kulileta matokeo ya kuwa Mkristo ambaye alipaswa achukuliwe hivyo badala ya kufanywa mtumwa (kuwa katika hali ya utumwa).
  - C. Filemoni anaombwa na Paulo amtendee Onesmo kama ambavyo angemtendea yeye Paulo.
  - D. Paulo alionesha kwamba kama Onesmo alifanya makosa Paulo alikuwa tayari kulipa mst. 18, 19.

#### **5. MUHTASARI WA WARAKA KWA FILEMONI.**

- A. Salaam - mist. 1 - 3.
- B. Asante na shukrani kwa Filemoni - 4 - 7.
- C. Ombi la Paulo kwa niaba ya Onesmo - 8 - 21.
- D. Maelezo ya Paulo kuamini angeachiwa huru karibuni mst. 22.
- E. Washiriki wa Paulo wanatuma salaamu mist. 22 - 25.

#### **6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA KITABU CHA FILEMONI.**

- A. Paulo aliendelea kuhubiri injili hata alipokuwa kifungoni - Mdo. 28:30, 31; Flm. 10, 11.
- B. Ukristo unaweka tofauti hali ya maisha ya mtu.
  - 1. Onesmo sasa alikuwa na faida ingawa awali hakuwa na faida - mst. 11.
- C. Kurejesha kilichopotea au kilichoibwa panapokuwa na toba ya kweli kunahitajika.
  - 1. Filemoni alikose wa na Onesmo alipoamua kukimbia.
  - 2. Ilikuwa sasa vema kurudi na kuyatengeneza makosa yasiwepo tena (Mt. 3:8).
- D. Uweza wa Mungu huwafanya wawili - mtenda dhambi na mhubiri wakutane pamoja - mst. 10.
- E. Injili ilihusika na kuondolewa kwa utumwa japo taratibu.
  - 1. Halikufanyika jambo hilo kwa vita au amri, bali kwa kufundisha.
  - 2. Matumizi ya "Sheria ya Dhahabu" yaliwezesha kuondoka kwa utumwa (yangewezesha hivyo) - Mt. 7:12.
  - 3. Kwa mvuto wa Ukristo wengi wa waanzilishi wa taifa la Marekani (USA), kama George Washington na Thomas Jefferson waliwaachia huru watumwa.

- F. Kwamba kwa sababu mtu ni Mkristo hakuna maana ya kwamba vizingiti nya kijamii vimeondolewa.
  - 1. Mtumwa alikuwa bado anakuwa chini ya bwana wake - 1 Kor. 7:20 - 23.
- G. Utumwa ulirekebishwa na Ukristo mpaka misingi yake ilipouondoa - Efe. 6:5 - 9; Kol.3:22 - 4:1.

**MWISHO:**

- 1. Paulo ameoneshwa kuwa mtu wa adili, mwerevu katika kuyaendea mambo nyeti, mwanadiplomasia.
  - A. Jambo ambalo angeweza kulifanya amri kama mtume alichagua kushawishi kwa hiari.
- 2. Hajajulikana kama Filemoni alifuata au la mashauri ya Paulo.

## **SOMO LA XXII - WAEBRANIA - NENO LA MWISHO LA MUNGU**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu cha Waebrania huchukuliwa kuwa ni kimojawapo kati ya vitabu vigumu vya Agano Jipyा.
2. Ili kuufahamu mpango wa ukombozi mtu anahitaji kuwa na ufahamu wa kitabu hiki.
3. Agano la Kale na Jipyा yamefungamanishwa na kitabu hiki:
  - A. Kuonesha kwamba Agano la Kale mahali pake pamechukuliwa na Agano Jipyा.
  - B. Kuonesha kwamba msamaha mkamilifu wa dhambi na ukombozi haukuwezekana chini ya Agano la Kale.
  - C. Kuonesha kwamba Yesu ndiye neno la mwisho kwa mwanadamu.
    1. Akikataliwa hayuko mwingine wala hapawezi kuwa na wokovu pasipo Yeye.
4. Kitabu hicho ni kitabu cha imani.
  - A. Kimeandikwa kuimarisha imani ya Wakristo dhaifu.
  - B. Kinajumuisha “Ukumbi wa Sifa za Mashujaa wa Imani - Sura ya 11.
5. Kinategemea ufahamu wa Agano la Kale zaidi kuliko kitabu kingine cho chote cha Agano Jipyा ili kukielewa.

### **MJADALA:**

1. **NANI ALIKIANDIKA KITABU HICHO?**
  - A. Hakijumuishi jina la mwandishi
  - B. Kupambanua mwandishi kumekuwa ni mdahalo wa muda mrefu.
    1. Waandishi wengi wamekisiwa kuhusika:
      - A. Clement wa Rumi.
      - B. Barnaba.
      - C. Sila.
      - D. Prisila au Akila.
      - E. Yohana au Marko.
      - F. Luka.
      - G. Apolo.
      - H. Paulo.
    2. Walio wengi wamekubali kuwa mwandishi wa kitabu hicho ni Paulo.
      - A. Waandishi wa kale waliompokea Paulo kuwa ndiye mwandishi:
        1. Pantaenus, rais wa shule ya Biblia iliyokuwako Alexandria, Misri mnamo 180 B. K.
        2. Clement wa Alexandria, aliyemfuatia Pantaenus kama rais wa shule ya Biblia ya Alexandria, alisema Paulo aliandika kitabu hicho na Luka akakitafsiri katika Kiyunani.
        3. Origen, aliyemfuata Clement kama mkuu wa Shule ya Biblia alimwandikia Africanus na kuelezea, "...tulikusudia kuandika maelezo yanayojitegemea kuonesha kwamba waraka huo ni wa Paulo"
        4. Katika mwaka wa 269 Baraza la Antioquia lilipeleka barua ambayo ilisema mtume yule yule aliyeandika kwa Wakorintho aliandika pia Waraka kwa Waebrania.
        5. Eusebius, anayechukuliwa kuwa ni "Baba wa historia ya kanisa" aliandika mnamo karne ya nne kwamba Paulo aliandika waraka huo na ama Luka au Clement wa Alexandria alitafsiri katika Kiyunani.
        6. Kuanzia kipindi cha Jerome katika karne ya nne hadi Matengenezo ya Waprotestanti katika karne ya 16, hakuna aliyehoji kuwa mwandishi ni Paulo.

3. Hoja kubwa dhidi ya Paulo kuwa ndiye mwandishi ni kwamba Kiyunani kilichotumika ni tofauti na kile kinachopatikana katika nyaraka zake nyingine.
  - A. Hilo linaweza kujibowi kwa kufikiria kama Kitabu cha Waebrania kiliandikwa na Paulo kwa Kiebrania, kisha mtu mwingine akatafsiri katika Kiyunani, kutakuwa na tofauti ya wazi katika lugha.
  - B. Ni muhimu izingatiwe kwamba wasikilizaji wapelekewa huduma, muda na hali husika vyote vinaathiri lugha anayoitumia mwandishi.
  - C. Ushahidi wa ndani unaonekana angalau kwangu, kuwa una nguvu zaidi kwa upande wa kwamba ni Paulo (mwandishi).
    1. Mtazamo wa mantiki ile ile inayotumika katika nyaraka zake nyingine unajionyesha hapa pia.
    2. Mshirika wa karibu sana na Paulo, Timotheo, ametajwa - Ebr. 13:23.
    3. Uliandikwa huko Italia karibu wakati ule Paulo alipoachiliwa toka kifungo chake cha kwanza - Mdo. 28:30, 31; Ebr. 13:24.
  - D. Ingezingatiwa pia kwamba uamuzi kuhusu mwandishi sio suala la ushirika.

## 2. KITABU HICHO KILIANDIKWA KWA NANI?

- A. Maoni mengi yametolewa kuhusu awali ulikuwa unapelekwa wapi.
  1. Wakristo wa Kiyahudi ko kote kule.
  2. Wakristo wa Kiyahudi wa Uyunani, Hispania au Italia.
  3. Wakristo wa Kiyahudi wa Palestina.
    - A. Mtazamo huo unaweza kuwa sahihi kwa sababu zifuatazo.
      1. Jina la somo, "KWA WAEBRANIA" lilikuwa limehusishwa katika Waraka huo mapema.
        - A. Jina "Waebrania" lilikuwa la kawaida kwa Wayahudi walioishi Palestina.
        - B. Wengine wote walitajwa tu Wayahudi.
    - B. "Wakristo" wa mwanzoni wengi wao wanakubali uliandikwa kwa Wayahudi wa Palestina.
    - C. Ushahidi wa ndani una nguvu kuonesha kuandikwa Wakristo Wayahudi wa Palestina.
      1. Wapokeaji walikuwa wazoefu wa hekalu la Kiyahudi (katika shughuli za ibada) na taratibu na matoleo.
      2. Matatizo yaliyokuwa yakishughulikiwa yanaendana zaidi na hali ya Wakristo wa Kiyahudi katika Palestina wakati wa kipindi kilichotangulia kuanguka kwa Yerusalem mwaka 70 B. K.
      3. Kumbukumbu zilizotangulia maanguko ya Yerusalem zinaonesha wale walioandikiwa waraka walikuwa wakazi wa Yerusalem.

## 3. ULIANDIKWA LINI NA WAPI?

- A. Yaonesha kwamba wale waliopokea waraka huo walikuwa Wakristo kwa muda wa kutosha.
  1. Hiyo ingeonesha kuwa uliandikwa miaka kadhaa baada ya kuanza kwa kanisa.
- B. Kwa kuwa unashughulikia ujio wa maangamizi ya Yerusalem, ni lazima uwe uliandikwa kabla ya B. K. 70.
  1. Ulipokuwa unaandikwa hekalu lilikuwa lingalipo na matoleo yalikuwa yakiendelea kutolewa - 8:4; 10:11.
  2. Kumbukumbu zilitaja kuhudu uharibifu ulipokuwa unaujia mji - 10:24, 25.
- C. Paulo alikuwa kifungoni Rumi mwaka 62 A.D. lakini alikuwa akitazamia kufunguliwa punde - Flp. 1:21 -26; 2:24.
  1. Ebr. 13:24 panaonesha Paulo alikuwa ametoka kufunguliwa kifungoni.

2. Kwa hiyo, yaelekea wazi zaidi waraka huo uliandikwa wakati wa kumalizia kifungo chake yaani 63 B.K.
- D. Kama ilivyotajwa huko nyuma, uliandikwa Italia, Mdo. 28:30, 31; Ebr. 13:24.
4. **KWA NINI KITABU HICHO KILIANDIKWA ?**
- A. Kulikuwa na hatari Wayahudi waliokuwa Wakristo walikuwa wako katika kuelekea kuacha Ukristo na kurudi kwenye dini ya Kiyahudi.
  - B. Walikuwa wakitiwa moyo kudumu katika uaminifu na mwandishi akiwathibitishia hilo kwa kuonesha jinsi ubora kwa Kristo ulivyokuwa ukizidi ule wa taratibu za Musa.
  - C. Maneno makuu katika kitabu cha Waebrania:
    - 1. Bora Zaidi.
      - A. Hutokeea mara 13.
      - 1. Huonesha kwamba Ukristo.
        - A. Unao ubora zaidi wa kuhani na ukuhani.
        - B. Unayo matoleo bora zaidi.
        - C. Una agano bora zaidi kwa msingi wa ahadi bora zaidi.
        - D. Unatoa mapumziko na nchi bora zaidi.
      - 2. Imani.
      - A. Hutokeea mara 32.
      - 3. Mara moja tu.
      - A. Hutokeea mara 12.
      - 4. Milele.
      - A. Hutokeea mara 5.
5. **MUHTASARI WA KITABU CHA WAEBRANIA**
- A. Neno la mwisho la Mungu kwa mwanadamu lilikuwa kwa njia ya Kristo, 1:1-3.
  - B. Kristo ni bora kuliko malaika, 1:4-2:18.
  - C. Kristo ni bora kuliko Musa, 3:1-6.
  - D. Kristo anatoa mapumziko mema zaidi kuliko Yoshua aliyoyatoa Kanaani, 3:7-4:13.
  - E. Kristo ni kuhani mkuu bora zaidi kuliko Haruni na wafuasi wake, 4:14-8:5.
  - F. Kristo alianzisha agano bora zaidi kwa msingi wa ahadi bora zaidi kuliko ile iliyofanywa na Waisraeli , 8:6-10:39.
  - G. Kusihi kwa ajili ya uaminifu, 11:1-40.
  - H. Kusihi kwa ajili ya uimara.
  - I. Wosia wa kufungia, 13:1-25.
6. **MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA WAEBRANIA.**
- A. Ni kwa njia ya Kristo tu wokovu wapatikana - 9:28.
  - B. Mwanadamu hafungwi na Agano la Kale leo, bali anaishi chini ya Agano Jipy, 7:12, 22; 8:6-13; 10:9; 12:24.
  - C. Kuna kuhani mwenye rehema na uaminifu anayeyaelewa majaribu ya mwanadamu na anatoa neema wakati wa uhitaji, 4:14-16.
  - D. Imani iokoayo ni imani ya utii, 5:8, 9; 11:4, 7 - 10, 17.
  - E. Mahudhurio ya kawaida katika ibada ni ya lazima ili kuendeleza uaminifu, 10:25.
  - F. Mwanadamu afapo haibaki tena nafsi ya kutufuta wokovu, 9:27-28.
  - G. Ni kwa njia ya Kristo tu Mungu anaongea na mwanadamu leo - 1:1, 2.

- H. Kristo ni Mwana na Mungu - 1:8.
- I. Mkristo aweza kuanguka toka katika Neema na kupotea milele - 4:1, 11; 6:1 - 9; 10:26-31.
- J. Wakristo ni lazima wakue na kuweza kufundisha wengine , 5:12-6:9.
- K. Karama za miujiza zilitolewa kwa kusudi la kulithibitisha neno la Mungu - 12:22-28.
- L. Wakristo ni wenyewe wa Ufalme usioweza kutetemeshwa - 12:22-28.
- M. Ndoa yatoka kwa Mungu na yapaswa ielekezwe kwa sheria za Mungu - 13:4.
- N. Yesu habadiliki na hivyo twaweza kuzitegemea ahadi zake - 13:8.

**MWISHO:**

1. Katika kitabu hiki inaweza kuonekana wazi kwamba ni kwa njia ya damu ya Kristo tu mwanadamu anaweza kuondolewa dhambi - 10:4; 9:22-28.
2. Huthibitisha kwamba wale tu wanaotii ndio watakaokolewa - 5:8, 9.

**SOMO LA XXIII - YAKOBO - WARAKA WA KUTUMIA AKILI YA KAWAIDA**  
(Common Sense)

**UTANGULIZI:**

1. Misingi ya Ukristo wa vitendo imesisitizwa katika kitabu hiki.
  - A. Kitabu cha Yakobo kimetajwa kuwa ni “waraka wa kutumia akili ya kawaida”.
  - B. Pia kimetajwa kuwa ni “kitabu cha Methali za Agano Jipyä”.
2. Ni kitabu cha kwanza katika vitabu saba vinavyojulikana kama nyaraka za wote.
  - A. Hizi hazikuandikwa kwenye makanisa maalum au watu maalum.
  - B. Hizi ni: Yakobo, 1, 2 Petro, 1, 2, 3 Yohana na Yuda.
3. Kitabu cha Yakobo kimetajwa kwamba ndicho cha Kiyahudi kuliko vyote katika Agano Jipyä.
4. Katika namna nyingi kinafanana na Mafundisho ya Mlimani (Hotuba ya Bwana Yesu Mlimani).

**MJADALA:**

1. **NANI ALIKIANDIKA KITABU HICHO?**

- A. Watu muhimu watatu katika Agano Jipyä wanatajwa kwa jina la Yakobo.
  1. Mwana wa Zebedayo na ndugu wa Yohana ambaye alikuwa mmoja wa mitume wa awali Mt. 4:21; Lk. 5:10.
  2. Mwana wa Alfayo, ambaye pia alikuwa mmoja wa mitume wa awali - Mt. 10:3; Mk. 3:18; Lk. 6:15; Mdo. 1:13.
  3. Mwana wa Mariamu na Yusufu, mdogo wake (kwa mama) Bwana Yesu - Mt. 13:55; Mk. 6:3; Gal. 1:18, 19.
- B. Yakobo, mwana wa Zebedayo na nduguye Yohana, aliamuriwa kuuawa na Herode Agripa I miaka michache baada ya kanisa kuanza - Mdo. 12:1, 2.
  1. Hajawa kawaida kuamini kuwa huyu Yakobo ndiye mwandishi kwa sababu yaonekana alifariki kabla ya kitabu kuandikwa.
- C. Kuhusu Yakobo mwana wa Alfayo, habari zake zafahamika kidogo tu.
  1. Mwandishi wa kitabu kinacho taja jina lake anaonekana alikuwa akijulikana sana.
  2. Kwa sababu huyu Yakobo amekuwa hajulikani, ni wachache sana waliowahi kufikiria angekuwa ndiye mwandishi.
- D. Ni Yakobo mwana wa Mariamu na Yusufu, ambaye anasadikika kuwa alikiandika kitabu hicho.
  1. Alikuwa ni mmojawapo wa ndugu wa kimwili wanne wa Yesu - Mt. 13:55.
  2. Yeye pamoja na ndugu wengine, hawakumwamini Yesu hadi alipofufuka - Yn. 7:1-5.
  3. Bwana alimtokea baada ya kufufuka kwake - 1 Kor. 15:7.
  4. Yeye, pamoja na ndugu wengine na mamaye Yesu, Mariamu, walikutanika Yerusalem baada ya Yesu kupaa mbinguni, Mdo. 1:14.
  5. Akawa kiongozi wa kanisa Yerusalem lilipoanzishwa - Mdo. 15:13; Gal. 2:9.
  6. Mawazo ya aina mbili hutolewa kuhusu kifo chake katika maandiko ya awali.
    - A. Josephus anadai Yakobo alipigwa kwa mawe kwa amri ya kuhani mkuu.
    - B. Eusebius anadai Yakobo alitupwa chini kutoka mnara wa hekalu na kupigwa hadi kufa kwa virungu.

2. **KITABU ALIANDIKIWA NANI?**

- A. “Kabila kumi na mbili waliotawanyika” - 1:1.
  1. Usemi “kabila kumi na mbili” lilikuwa ni jina la Israeli.

2. Wayahudi walikuwa wametawanyika duniani kote kwa sababu ya utumwa na masuala ya biashara.
- B. Kumbukumbu inafanywa kwa Wakristo ambao ni “Israeli ya Mungu” Gal. 6:16.
1. Wengi wao walitawanyika kwa sababu ya mateso.

### 3. LINI NA WAPI KITABU HICHO KILIANDIKWA ?

- A. Yakobo ni kimojawapo katika vitabu vya awali kabisa katika Agano Jipyä kuandikwa.
1. Josephus anaonesha Yakobo aliuawa mnamo 62 au 63 B. K.
  2. Kwa kuwa Yakobo hahusishi kumbukumbu ya Wakristo wa Mataifa yaelekeea kitabu kiliandikwa kabla ya mkutano wa Yerusalem kujadili suala la tohara - Mdo. 15.  
A. Hilo lingeweka muda wa kuandikwa kitabu kabla ya 48 B.K.
  3. Kumbukumbu za “jina zuri mliloitwa” zinaonesha kitabu kiliandikwa baada ya 40 B.K. wakati jina Mkristo lilipotolewa - Mdo. 11:26; Yak. 2:7.
  4. Hitimisho kwa hiyo ni kuwa kitabu hicho kiliandikwa kati ya 40 B.K. na 48 B.K.
- B. Kutaja Palestina mara nyingi hivyo kwaonesha Yakobo alikuwa akiandika kutokea huko.
1. Kumbukumbu zinazotaja “Mvua za mwanzo na za mwisho” zitokeavyo Palestina - 5:7.
  2. Kumbukumbu za hali ya joto (katika upepo) zilijulikana kama “simoon” na ziliku wa za kawaida katika Palestina, 1:11.
  3. Kumbukumbu zinazotaja maji matamu na maji machungu ni chemchemi zipatikanazo Palestina, 3:11.
  4. Yaelekeea waraka huu uliandikwa Yerusalem kwa sababu Yakobo aliishi huko.

### 3. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA ?

- A. Kwa sababu ya mateso na Wakristo kutotendewa ipasavyo walihitaji uvumiliu, 1:12-15; 2:6-7; 5:1-11.
- B. Kulikuwa na haja ya kufundisha kuhusu masuala ya upendeleo, ambao Wakristo walionekana kuwa na kosa, 2:1-10.
- C. Kulikuwa na haja ya kusahihisha uelewa wao wa imani, 1:22-27; 2:14-26.
- D. Kulikuwa na haja ya kusahihisha tabia yao kuhusu mawazo yao ya kidunia, husuda na tamaa - 3:13 - 4:12.

### 4. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA KITABU CHA YAKOBO

- A. Sala inayopungukiwa imani haitajibiwa - 1:6.
- B. Chanzo cha dhambi ni tamaa ya mwanadamu - 1:13 - 16.
- C. Mkristo amezaliwa kwa Roho Mtakatifu kwa njia ya Neno - 1:18.
- D. Mkristo lazima ajifunze kudhibiti ulimi wake - 1:26, 3:1 - 12.
- E. Kuonesha upendeleo ni dhambi - 2:1 - 10.
- F. Imani iokoayo ni imani yenye matendo - 2:14 - 26.
- G. Maisha ya hapa duniani ni mafupi na yapasa yamshirikishe Mungu katika yote - 4:13 - 16.
- H. Sala itokayo katika maisha ya uaminifu ina nguvu - 5:13 - 18.

### **MWISHO:**

1. Yakobo anajieleza mwenyewe kuwa ni mtumishi wa Yesu 1:1.
  - A. Hilo linavuka nasaba ya kimwili wapendayo wengi kuwa nayo.
  - B. Yakobo anafahamu kwamba uhusiano wa kiroho kati ya Mungu na mwanadamu ni muhimu kupita vyote - Mk. 3:31-35; Lk. 11:27, 28

## **SOMO LA XXIV - 1 PETRO - WITO KUTUMIKA KATIKATI YA MATESO**

### **UTANGULIZI:**

1. Nyaraka mbili ziliandikwa na Mtume Petro.
2. Ni mionganoni mwa Nyaraka saba za Wote kwa sababu hazikuandikwa kwenye kusanyiko maalum wala kwa watu binafsi.
3. Maandiko ya Petro yanaaheshimika sana na kukubalika kwa mapana.
4. Waraka wake wa kwanza ni waraka wa kutiana moyo na kusihiana ukiwa umeandikwa kwa Wakristo waliokuwa wanateswa kwa ajili ya imani yao katika Kristo.

### **MJADALA:**

#### 1. **NANI ALIANDIKA KITABU HICHO?**

- A. “Petro mtume wa Yesu Kristo” - 1:1.
- B. Mpaka nyakati za kisasa uandishi wake haukuhojiwa.
  1. Waandishi wa awali kama Clement wa Rumi Polycarp, Papias, Irenaeus, Tertullian, Origen na Eusebius, wote wanaonesha imani yao kuwa Petro aliandika kitabu hicho.
  2. 2 Petro huthibitisha uhalali wa 1 Pet. - 2 Pet. 3:1.
  3. Yaliyo ndani ni sifa ya kile tukifahamucho kuhusu tabia ya Petro.
- C. Petro alikuwa ni mmoja wa watu waliokuwa mashuhuri zaidi katika kanisa la awali.
  1. Anajielez a mwenyewe kama ni mtume.
    - A. Si kama Papa inavyodaiwa na kanisa Katoliki.
  2. Jina la babaye alikuwa Yona na kakaye alikuwa Andrea, aliyekuwa pia mtume - Mt. 16:17; Yn. 1:40 - 42.
  3. Alioa - Mk. 1:29 - 31; 1 Kor. 9:5.
  4. Alikuwa na watoto kwa sababu alitumika kama mzee wa kanisa katika kanisa - 1 Pet. 5:1; 1 Tim. 3:4, 5; Tit. 1:6.
  5. Yeye na Andrea walitoka Bethsaida lakini yawezekana waliishi Kapernaumu - Yn. 1:44; Mt. 8:5, 14, 15.
  6. Yeye na Andrea walikuwa wavuvi wa samaki ambaو walikuwa washirika na Yakobo, Yohana na Zebedayo - Mt. 4:18; Lk. 5:1-11.
  7. Yeye na Andrea walikuwa ni wanafunzi wa kwanza wa Yohana Mbatizaji - Yn. 1:35 - 40.
  8. Alikuwa ni Andrea aliyemleta Petro kwa Yesu - Yn. 1:40 - 42.
  9. Jina la kupewa lilikuwa Simoni - Mt. 4:18.
  10. Jina Petro, kutoka Kiyunani “Petros”, lilimaanisha jiwe dogo.
  11. Kwa Kiaramu petros ni Kefa - Yn. 1:42.
  12. Alikuwa jasiri, mwenye maamuzi ya haraka aliyekuwa kiongozi wa watu, lakini wakati mwingine alikuwa dhaifu na mwenye kurudi nyuma.
    - A. Daima anaonekana wa kwanza katika orodha ya mitume, Mt. 10:2-4; Lk. 6:12-16; Mdo. 1:13.
    - B. Alimkana Yesu mara tatu, kisha akatubu kwa machozi ya uchungu, Lk. 22:31-34; 54-62.
    - C. Alipewa nafasi tatu kuthibitisha upendo wake kwa Bwana (aliyemhoji ni Yesu) - Yn. 21:15-17.
  13. Alipata bahati ya kuwa mionganoni mwa “sehemu ya ndani” ya mitume - Mk. 5:35 - 43; Mt. 17:1-8; 26:36-46.
  14. Yesu alimtokea mara baada ya kufufuka kwake - 1 Kor. 15:53.
  15. Alipewa “funguo za ufalme” kuzitumia siku ya Pentekoste na nyumbani kwa Kornelio kuruhusu wote Wayahudi na Wamataifa kuingia katika ufalme - Mt. 16:19; Mdo. 2 na 10.
- D. Je, Petro alikuwa Papa wa kwanza?

1. Wakatoliki wanadai kwamba yeche ni mwamba ambaye juu yake kanisa limejengwa - Mt. 16:18.
  - A. Usemi wa Yesu ni utengenezaji wa maneno.
    1. Anasema, "Wewe ndiwe Petro (Petros, jiwe dogo) na juu ya mwamba huu (Petra, mwala, mwamba), nitalijenga kanisa langu," Mt. 16:18; 1 Kor. 3:11.
    - B. Mamlaka ya kufunga na kufungua walipewa mitume wote na sio Petro peke yake.
  2. Mapapa wanakatazwa kuoa, lakini Petro alikuwa ni mtu aliyeoa - 1 Kor. 9:5.
  3. Paulo aliweza kumkemea Petro, lakini Mapapa husemekana kuwa hawakosei (hawaanguki) katika masuala ya mafundisho na kanisa.
  4. Petro alidai kuwa ni mtume na mtumishi wa Yesu - 2 Pet. 1:1.
    - A. Kama alikuwa ni Papa wa kwanza, kwa nini hakudai kuwa alikuwa na wadhifa huo?
  5. Tofauti na Mapapa wa leo, Petro alikataa kutukuzwa kwa heshima maalum - Mdo. 10:25, 26.

## 2. KITABU WALIANDIKIWA NANI?

- A. Kimeandikwa kwa "wateule wa Utawanyiko, wakao hali ya ugeni katika Ponto, Galatia, Kapadokia, Asia na Bithinia," 1:1.
  1. Yote yalikuwa majimbo katika himaya ya Kirumi ndani ya Asia Ndogo.
  2. Anaweza kuwa alitumika katika maeneo hayo pamoja na kuanzisha baadhi ya makanisa.
  3. Baadhi ya makanisa yanaweza kuwa yalianzishwa na Wayahudi walioongoka siku ya Pentekoste - Mdo. 2:9.
- B. Watu wa kwanza kupokea nyaraka zake walikuwa ni Waongofu wa Mataifa.
  1. Usemi wa "...tamaa za kwanza katika Ujinga wenu" ungeonesha wazo hilo - 1:14, 18.
  2. Hawa hawakuwa watu wa Mungu, wala hawakuwa wamepokea rehema nyakati zilizopita - 2:10.
  3. Anatumia jina lake la Kiyunani badala ya jina lake la Kiaramu - 1:1.
  4. Walikuwa, "wametenda mapenzi ya Mataifa wakati uliopita - 4:2 - 4.

## 3. WARAKA ULIANDIKWA LINI NA WAPI?

- A. Uliandikwa Babeli - 5:13.
  1. Wengine wametoa wazo kuwa Babeli ni mfano tu kwa ama Rumi au Yerusalem.
    - A. Hata hivyo, hakuna ushahidi kwa kuhitimisha hivyo.
  2. Wengine wamefikiria unatajwa mji mdogo katika Misri wenye jina hilo.
  3. Yaonekana ni vema zaidi kulitumia jina hilo kwa ajili ya Babeli iliyo juu ya Frati (Euphrates).
- B. Yaelekea uliandikwa kipindi cha mateso makubwa.
  1. Yaonekana kuelekeana na mateso ya Nero - 64 - 67 B.K..
  2. Wengi wanafikiria ni mwaka 65 B.K.

## 4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?

- A. Kiliandikwa kuwaimarisha na kuwapa moyo Wakristo waliokuwa wakiteswa kwa sababu ya imani yao, 1:6-7; 4:14-19.
- B. Maneno mawili, au namna ya maneno hayo, yanasaidia kuelezea kwa nini waraka uliandikwa.
  1. Namna moja ya kuteseka au mateso hutajwa mara 15.
  2. Neno tumaini limeonekana mara nne.

## 5. MUHTASARI WA 1 PETRO.

- A. Urithi na tumaini la waumini - sura ya 1.
- B. Neema ya uvumiliyu katika kustahimili - sura ya 2.

- C. Maelezo ya hulka ya Mkristo wa kweli - sura ya 3 na 4.
- D. Wosia wa kufungia - sura ya 5.

**6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA 1 PETRO.**

- A. Kuna urithi umewekwa Mbinguni kwa ajili ya Wakristo - 1:3 - 5.
- B. Imani ya Mkristo inajaribiwa na kuwa na nguvu zaidi kwa njia ya mateso, 1:6, 7; 4:14 - 19.
- C. Wakristo ni lazima wawe watakatifu kama Mungu alivyo mtakatifu, 1:14-16.
- D. Wakristo ni watu walioteuliwa (baada ya kutii Injili) na Mungu, 2:4-10.
- E. Wakristo wawaheshimu viongozi wao na kutii sheria za nchi - 2:13 - 17.
- F. Kielelezo cha Mkristo katika mateso, pamoja na wengine wote, ni Kristo - 2:19 - 25.
- G. Mume asiyeamini anaweza kuongoka katika kuingia kwa Kristo kutokana na mfano mzuri kuwekwa na mkewe, 3:1-6.
- H. Ubatizo ni wa lazima katika wokovu, 3:18-22.
- I. Wazee wa kanisa ni wachungaji na sio, "Madikteta," 5:1-4.
- K. Adui mkuu wa Mkristo ni Shetani, 5:6-9.

**MWISHO:**

1. Watenda dhambi wanaweza kutakatisha mioyo yao kwa kuitii kweli - 1:22, 23.
2. Maisha ni ya kitambo kifupi tu - 1:24, 25.
3. Waraka huu ni waraka wa tumaini.
  - A. Bila kujali kunatokea nini katika maisha, Mkristo ana tumaini jema zaidi la maisha mema zaidi baada ya haya ya sasa.

**SOMO LA XXV - 2 PETRO - WITO KWENYE UFAHAMU KATIKATI YA  
MAFUNDISHO YA UPOTOFU.**

**UTANGULIZI:**

1. Petro alikuwa kwa kiasi fulani kitimtimu na kiongozi mwenye msukumo kwa watu.
  - A. Yesu alipowauliza wanafunzi wake kama wangeondoka alikuwa ni Petro aliyejibu, "Twende kwa nani?" Yn. 6:67, 68.
  - B. Alikuwa ni Petro aliyejibu katika swal la Yesu kuhusu watu walinena kuwa Yeye alikuwa nani - Mt. 16:13-16.
  - C. Petro alisema asingemkosea Yesu - Mk. 14:29, 30.
  - D. Petro ndiye aliyetao hotuba ya kwanza kwa Wayahudi siku ile ya Pentekoste na Wamataifa katika nyumba ya Kornelio, Mdo. 2 na Mdo. 10.
2. Yesu alitabiri kuhusu kifo cha Petro - Yn 21:18.
3. Mapokeo yanaonesha kwamba Petro alisulibishwa kwa sababu ya imani yake.
4. Kabla ya kifo chake aliandika nyaraka mbili kuhusu mateso wakati wa dhiki/masumbuko (1 Petro), na walimu wapotofu (2 Petro).

**MJADALA:**

1. **NANI ALIANDIKA KITABU HICHO?**
  - A. Waraka unadhihirisha kwa nguvu kabisa kwamba mwandishi alikuwa mtume Paulo.
    1. Hudai kuwa mwandishi ni yeze - 1:1.
    2. Huweka kumbukumbu kwa 1 Pet. 3:1.
    3. Mwandishi alikuwa shahidi wa utukufu wa Yesu - 1:16.
    4. Mwandishi alikuwepo pale mlimani wakati wa kubadilika sura - Mt. 1:17, 18; 17:1 - 9.
    5. Mwandishi anajishirikisha katika mitume - 3:2.
  - B. Hata katika sura ya ushahidi huo wa ndani, mashaka mengi yamewekwa dhidi ya uhalali wa 2 Petro kuliko kitabu kingine cho chote katika Agano Jipy.
    1. Wanaohoji wanadai usingekuwa umeandikwa na Petro, kwa sababu mwandishi anajitaja kuwa ni Simoni Petro badala ya Petro - 1:1.
      - A. Kisichozingatiwa ni kwamba Simoni lilikuwa ni jina lake la Kiebrania ambapo Bwana alimtajia jina la Petro, Yn. 1:40 - 42.
    2. Wanaohoji pia wanadai 2 Petro usingeandikwa na Petro kwa sababu mwandishi anahuisha utabiri wa kifo chake katika Yn. 21:18, na Yohana hakikuwa kimeandikwa mpaka muda mrefu kupita baada ya Petro kufariki, 1:13, 14.
      - A. Yesu alitabiri kifo cha Petro kwa Petro mwenyewe.
        1. Ilikuwa sio lazima kwa yeze kusubiri mpaka Yohana aandike juu ya jambo hilo ili kulijua.
        - B. Kwa kupata ukweli mwandishi aliufahamu utabiri kwaonesha Petro alikuwa ndiye mwandishi.
      3. Wanaohoji wanadai kumbukumbu za kubadilika kwa sura ziliongezwa ili ionekane kuwa Petro aliandika waraka huo, 1:17, 18.
        - A. Ni dhahiri, kugeuka kwa sura kwaonesha Petro kuwa ndiye mwandishi, akiwa pamoja na Yakobo na Yohana kuthibitisha tukio, Mt. 17:1-9.
        - B. Huu ni ushahidi imara dhidi ya wanaohoji.
      4. Wanaohoji wanadai kumbukumbu za maandiko ya Paulo yakiwa ni Maandiko (3:15, 16) yalikuwa yemeandikwa katika karne ya pili kwa maana nyaraka za Paulo zilikuwa hazijasambazwa mpaka wakati huo, na kabla ya hapo hazikujulikana kuwa Maandiko Matakatifu.

- A. Hilo ni kusahau ukweli kwamba Paulo anadai uvuvio kwa ajili ya nyaraka zake wakati ule ule zilipoandikwa , 1 Kor. 2:10, 11; 14:37; 1 Thes. 2:13.
- B. Kuna ushahidi kwamba maandiko ya Paulo yalisambazwa mionganoni mwa makanisa wakati wa maisha yake, 1 Kor. 1:2; Kol. 4:16.
- C. Clement wa Rumi katika nyaraka zake mbili kwa kanisa lililokuwa Korintho mnamo 95 au 96  
B.K. alinukuu kwa upana sana maandiko ya Paulo.
  - 1. Kama maandiko ya Paulo hayakuwa yameenea angeweza kufanya hivyo?
- 5. Wanaohoji wanadai kumbukumbu katika 1 Pet. 3:1 ni jaribio la kulifanya lililoghushiwa lione kane jema.
  - A. Dai hilo halina utetezi.
- 6. Wanaohoji wanadai kuwa, “mababa” wa 2 Pet. 3:4 wanahu shisha kizazi cha kwanza cha Wakristo waliokuwa wamekuwa.
  - A. Kwa hiyo, waraka utakuwa ni lazima uliandikwa muda mwangi baadaye.
  - B. Ifahamike kwamba wengi wa Wakristo wa awali walikuwa wamekuwa wakti waraka unaandikwa.
  - C. Pia yawezekana usemi “mababa” uwe na kumbukumbu ya mababa wa Agano la Kale na manabii.
- 7. Wanaohoji wanadai kwamba mwandishi aliazima toka kwa Yuda na, wanadhani, Petro asingeweza kufanya hivyo, 2:1-19; Yuda 1:4-20.
  - A. Inakubaliwa kwamba 2 Petro na Yuda ujumbe wake una lugha ya namna ya kufanana kwa sababu walikuwa wanashughulikia suala linalolingana.
    - 1. Vile vile ifahamike kama “uazimaji” ulifanyika, isingeweze kana kuwa kinyume chake?
      - A. Labda Yuda aliazima kwa Petro?
      - B. Linalohitaji kuangaliwa ni kwamba wote wawili walikuwa wakiandika kwa uwezo wa uvuvio.
        - 1. Kama mambo hayo hayo yalitumiwa na mwinge, hilo lillifanyika kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu, Isa. 2:1-4; Mik. 4:1-4.
  - 8. Wanaohoji wanadai mtindo wa uandikaji katika Kiyunani unatofautiana, hivyo kuonesha waandishi tofauti.
    - A. Inasahaulika ukweli kuwa kuna kufanana kwingi kuliko kutofanana.
    - B. Pia kwa sababu ya ukweli kwamba, nyaraka zinashughulikia masuala tofauti, mtu angetazamia tofauti za mtindo na msamiati.

## 2. WARAKA ULIANDIKWA KWA NANI?

- A. Uliandikwa kwa Wakristo wale wale waliopokea Waraka wa kwanza - 3:1.
- B. Yaonekana punde baada ya kupeleka Waraka wake wa kwanza, akawa amepata taarifa ya mambo mengine ambayo yalihitaji ayashughulikie.

## 3. LINI NA WAPI WARAKA (KITABU) ULIANDIKWA ?

- A. Sio rahisi kuamua lini na wapi waraka huo uliandikwa?
- B. Yamkinika zaidi uliandikwa mara baada ya ule wa kwanza.
  - 1. Yawezekana karibu na mwisho wa mateso chini ya Nero - B.K. 64 - 67.
- C. Petro yawezekana bado alikuwa Babeli - 1 Pet. 5:13.

## 4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA ?

- A. Uliandikwa ili kuwaonya watu dhidi ya mafundisho mapotofu yaliyokuwa yanaenea kanisani.
  - 1. Petro alisisitiza kwamba usalama wa pekee wa kuepuka mafundisho mapotofu ulikuwa ni kulijua Neno.

- A. Neno kuu katika 2 Petro ni ufahamu.
  - 1. Limetumika mara saba.
- B. Petro anabainisha hali/sifa za mwalimu mpotofu na mafundisho yake.
  - 1. Kumkana Yesu kuwa ni Kristo na Mwana wa Mungu - 2:1; Mt. 16:16.
  - 2. Kutumia utauwa kama njia ya kupatia faida ya binafsi - 2:3, 14 - 16.
  - 3. Kukosa heshima katika mamlaka, ama ya Mungu au mwanadamu - 2:10 - 12.
  - 4. Maisha ya ufisadi - 2:13, 14.
  - 5. Kukana suala la ujio wa mara ya pili, kiyama na kuteketea kwa dunia - 3:1 - 17.

**5. MUHTASARI WA 2 PETRO.**

- A. Maonyo kwa ajili ya kukua kiroho - sura ya 1.
- B. Hatari za mafundisho na hatma ya walimu wapotofu - sura ya 2.
- C. Kuja kwa mara ya Pili na mwisho wa dunia - sura ya 3.

**6. SOMO TUJIFUNZALO KUTOKA 2 PETRO.**

- A. Mungu ametoa Neno lake kitu kitakiwacho ili kuokolewa - 1:3; 2 Tim. 3:16,17.
- B. Anayetaka kuokolewa ni lazima aongeze baraka za Kikristo katika maisha yake - 1:5 - 11.
- C. Ushuhuda wa manabii waliovuviva na mashahidi waliooana wanamthibitishia Yesu - 1:16 - 21.
- D. Walimu wapotofu daima wamekuwepo na daima watakuwepo - 2:1 - 19.
- E. Yawezekana mtoto wa Mungu kuanguka toka katika neema - 2:20 - 22; 3:17.
- F. Kuja kwa mara ya Pili kwa Yesu kutakuwa ghafula na pasipokuategemea - 3:9, 10.
- G. Hapatakuwepo mahali pa ufalme wa kidunia (kwa mujibu wa mafundisho ya vipindi vyta miaka elfu (premillennialism) kwa sababu dunia itakuwa imeteketea - 3:10 - 12.
- H. Tumaini la muda ujao kwa Mkristo liko mbinguni - 3:13; Yn. 14:1 - 3.
- I. Mungu anawapenda watu wote na anataka wote waokolewe - 3:9.
- J. Kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na mwisho wa dunia kunaleta sababu yenyeye nguvu kwa nini Wakristo wajishughulishe na kumtumikia Mungu, 3:11, 14.
- K. Anayeyatumia vibaya maneno ya Mungu atapotea - 3:16.
- L. Ni lazima kwa Wakristo kuendelea kukua katika neema na ufahamu - 3:18.

**MWISHO:**

1. Habari ya 2 Petro yahitajika leo kama ilivyohitajika katika karne ya kwanza kwa sababu ya idadi ya walimu wapotofu duniani.
2. Njia pekee ya usalama dhidi ya upotofu wa upotoshaji wa mwalimu wa uongo ni kuwa na ufahamu makini wa Maandiko.

## **SOMO LA XXVI - 1 YOHANA - WARAKA WA UPENDO TOKA KWA MTUME WA UPENDO.**

### **UTANGULIZI:**

1. Waraka wa 1, 2 na 3 wa Yohana ni mionganini mwa vitabu vya mwisho vya Agano Jipywa kuandikwa.
  - A. Kutokana na vitabu hivyo tunapata undani wa kanisa na hali yake karibu na mwisho wa karne ya kwanza.
2. Vitabu hivi daima hutajwa kuwa ni “Nyarakaza upendo”.
  - A. Hata hivyo, vinashughulikia kimsingi walimu wapotofu waitwao waongo na wapinga Kristo.
3. Vyote vitatu viliandikwa na Yohana aliye kwishaitwa “mtume wa upendo”.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIKIANDIKA KITABU?**

- A. Kutoka nyakati za mwanzo kabisa, waraka huu umefikiriwa kuwa uliandikwa na Yohana ingawa haujumuishi jina lake.
1. Papias na Polycarp, wanafunzi wa Yohana walimpa sifa Yohana kuwa ndiye mwandishi wa kitabu hicho.
  2. Mnamo 170 A.D. kumbukumbu za Muratorian Canon zilionesha Yohana kuwa mwandishi.
  3. Tafsiri za zamani za Syriac na Kilatini, ambazo ni mbili kati ya tafsiri za zamani sana, zilimchukulia Yohana kuwa ndiye mwandishi.
  4. Wakati wa karne ya 2, ya 3 na ya 4 waandishi mashuhuri walimchukulia Yohana kuwa ndiye mwandishi.
    - A. Tertullian.
    - B. Irenaeus (Irene).
    - C. Clement (wa Alexandria).
    - D. Origen.
- B. Katika mitume, Yohana alikuwa mmojawapo wa wale waliojulikana kuliko wengine wote.
1. Mwana wa Zebedayo na Salome na ndugu wa Yakobo - Mt. 4:21; 27:55, 56.
  2. Mvubi wa samaki ambaye familia yake ilikuwa shirika na Andrea na Petro , Lk. 5:7-10.
  3. Mmojawapo wa watu wa kwanza kuwa mwanafunzi wa Yesu - Mt. 4:21, 22; Lk. 6:13-16.
  4. Alikuwa mmojawapo wa sehemu ya ndani ya mitume, Mk. 5:35-42; Mt. 17:1-9; 26:36, 37
  5. Alipewa jina la “mwana wa ngurumo” pamoja na nduguye Yakobo - Mk. 3:17; Lk. 9:51 - 56.
  6. Alijitaja mwenyewe kuwa “mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda” - Yn. 20:2; 21:20,24.
  7. Alifanya kazi kwa ukaribu zaidi na Petro - Yn. 20:1-10; Mdo. 3, 4, 8.
  8. Aliandika vitabu vitano katika Agano Jipywa.
  9. Anafikiriwa kuwa ndiye mtume pekee aliye fariki kifo cha kawaida.

#### **2. KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**

- A. Kinatambulika kuwa ni kitabu (waraka) kwa wote, si waraka kwa mtu maalum.
- B. Waandishi mbalimbali wa awali, kama Irene na Clement wa Alexandria, wanaonesha kwamba aliitumia sehemu ya mwisho ya maisha yake Efeso.
1. Makanisa mengi (makusanyiko) yalianzishwa eneo lile na Paulo.
  2. Kitabu cha Ufunuo, ambacho kiliandikwa na Yohana kilitumwa (katika anuani) kwenda kwenye “makanisa saba ya Asia.”
  3. Usemi ambaao ameatumia mara nyingi kwa wasomaji “watoto wadogo” waweza kuonesha walikuwa ni waongofu wake.

4. Wale aliowaandikia yawezekana sana walikuwa ni Mataifa kwa maana mara nyingi aliwaonya kuhusu ibada ya sanamu.

### 3. KITABU KILIANDIKWA LINI NA WAPI?

- A. "...kanisa katika Efeso .... Yohana akibakia kwa kudumu huko mpaka wakati wa Trajan ..." Irene.
  - 1. Yasemekana alihamia Efeso baada ya kifo cha Mariamu mama wa Yesu, na kuteketea kwa Yerusalem, Yn. 19:25-27.
  - 2. Akiwa aliishi mpaka wakati wa Trajan (98 - 117 B.K.) kungemfanya awe alikuwa na miaka yapata 100 alipofariki.
- B. 1 Yohana kinaonekana kiliandikwa na mtu mzee - 1 Yoh. 2:1, 12 - 14.
  - 1. Hayatajwi mateso, ambayo yameoneshwa katika utawala wa Domitian ulioanza mnamo 94 B.K. yalikuwa hayajaanza bado.
  - 2. Kwa kawaida waraka huo hufikiriwa uliandikwa kati ya 85 - 90 B.K. Tarehe ya mwisho ikiwa yenye uwezekano zaidi.

### 4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?

- A. Wengi walikuwa wanapotoshwa na walimu wa uongo ambaو walikuwa wamelivamia kanisa.
  - 1. Waraka uliandikwa kupinga mafundisho ya walimu hao.
  - 2. Pia uliandikwa kuimarisha imani ya Wakristo.
- B. Upotofu wa msingi katika mafundisho ulikuja katika kumkana Kristo kuwa alikuja katika mwili - 1:1, 2; 2:22, 23; 4:1-3.
  - 1. Msimamo wa Gnosticism (hali ya kuwa na ufahamu wa pekee maalum ambaو wengine hawana)
    - A. Neno hilo latokana na gnostic, ambalo latokana na gnosko, maana yake - najua, na gnosis, maana yake - ujuzi.
  - 2. Madai yao yalikuwa walikuwa na ufahamu bora ambaو Wakristo wa kawaida hawakuwa nao.
  - 3. Neno kujua (-jua) limetumika mara 27 katika kupinga mafundisho haya mapotofu.
- C. Imani ya msingi ya "Gnostics" ilikuwa kwamba vitu vya mwili, vitu vinavyoonekana na vitu vya kidunia vilikuwa viovu.
  - 1. Kwa sababu dunia ni kiumbe cha kimwili walidai kuwa isingewezeekana kuwa kilumbwa na Mungu, bali na mungu mdogo, kwa sababu ya uovu uliomo.
  - 2. Walifundisha kwamba kama mwili ni mwovu, Yesu asingalizaliwa kutoka kwa mwanamke.
  - 3. Baadhi ya watu fulani wa Gnostics walitajwa kama Docetics (kutokana na Kiyunani dokeo maana yake uonaji wa kufikiria tu) kwa sababu walifundisha kwamba Kristo alikuwa nafsi ya kiroho aliyeonekana kwa kufikiria alikuwa na mwili wa nyama.
  - 4. Bado wengine walifundisha kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida tu.
    - A. Walifundisha kwamba ukamilifu wa kiroho, yaani Kristo, ulikuja juu ya Yesu wakati wa ubatizo wake.
    - B. Kufuatia kusulibiwa wanassema kwamba Kristo alimwacha haraka Yesu na kuondoka.
- D. Kitabu cha 1 Yohana ni kitabu cha mtazamo wa pande mbili:
  - 1. Kweli dhidi ya kosa.
  - 2. Nuru dhidi ya giza.
  - 3. Upendo dhidi ya chuki.
  - 4. Uzima dhidi ya mauti.
- E. Yohana pia anasisitiza wazo dhahiri la ushirika.
  - 1. Ushirika kwa misingi ya ufahamu sahihi - 1:3.
  - 2. Kwa kuenenda katika nuru ushirika na Mungu huthibitika.

**5. MUHTASARI WA 1 YOHANA.**

- A. Yohana alithibitisha ujio wa Kristo katika mwili - 1:1 - 4.
- B. Ili mtu awe na ushirika na Mungu ni lazima aenende katika nuru - 1:5 - 2:17.
- C. Onyo dhidi ya wapinga Kristo - 2:18 - 29.
- D. Wakristo hawaendelei kuishi katika dhambi - 3:1 - 10.
- E. Maana ya upendo wa kweli - 3:11 - 24.
- F. Walimu wapotofu wajaribiwe - 4:1 - 6.
- G. Mafundisho ya nyongeza katika upendo wa kweli 4:7 - 5:3.
- H. Maisha ya milele yako kwa Yesu - 5:4 - 13.
- I. Haja ya sala na msamaha - 5:14 - 21.

**6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA 1 YOHANA.**

- A. Ili kuokolewa mtu ni lazima aukubali ukweli kuhusu hali kamili ya Kristo, 1:1-4; 2:18-24; 4:1-3; 5:5-13.
- B. Kama mtu anaendelea katika dhambi hawezu kuwa na ushirika na Mungu - 1:6, 7; 2:4, 5; 3:8 - 10.
- C. Wale wenye ushirika na Mungu wana ushirika na wengine wenye ushirika wa jinsi hiyo na Mungu, 1:3, 5-7.
  - 1. Wale wasio na ushirika na Mungu hawana ushirika na wenye imani.
- D. Msamaha wa dhambi kwa damu ya Kristo una masharti, hata kwa Wakristo - 1:7 - 10; Mdo. 8:22.
- E. Wakristo wasiweke tumaini lao katika dunia (na mambo yake) - 2:15 - 17.
- F. Ye yote anayekana kuwa Yesu alikuja katika mwili ni mpinga Kristo - 2:18 - 23; 4:1 - 3.
- G. Njia pekee kwenda Mbunguni ni Yesu - 2:1, 2; 5:5, 11, 12, 20.
- H. Maisha ya milele si jambo la kuwa nalo sasa bali ni jambo litalajiwalo na ahadi - 2:25; Tit. 1:2; Rum. 8:24, 25.
- I. Kuwa mtoto wa Mungu ni kupata tuzo iliyoo kuu kuliko zote - 3:1 - 3; 4:9, 10; 5:11, 12, 14.
- J. Dhambi hairithiwi, bali ni tendo dhahiri la kutomtii Mungu - 3 :4; 5:17; Eze. 18:20.
- K. Upendo hujidhihirisha wenyewe katika vitendo - 3:16 - 18; 4:20, 21; 5:2.
- L. Mtu ampendaye kwa kweli Mungu atashika amri zake - 2:3, 6; 3:7-22; 5:2, 3.
- M. Dhambi zote zasameheka isipokuwa isiyo kiriwa, 1:9; 5:14- 17.
- N. Ibada ya sanamu ni makosa, bila kujali ina kuja kwa mtazamo gani - 5:21.

**MWISHO:**

1. Kumpenda Mungu na ndugu kwawezekana wakati huo huo dhambi na mafundisho mapotofu yanapingwa.
2. Elimu haimhakikishii mtu kuwa yuko upande wa Mungu (msimamo ulioko kwa Mungu).
  - A. Hata wenye elimu wanawez a kuwa wajinga katika Neno Lake.

## **SOMO LA XXVII - 2 YOHANA - BARUA KWA MKRISTO MWANAMKE**

### **UTANGULIZI:**

1. 2 Yohana na 3 Yohana ndivyo vitabu vifupi kuliko vyote katika Agano Jipy.
  - A. Katika tafsiri ya Kiingereza, 3 Yohana kina mstari mmoja zaidi ya 2 Yohana.
  - B. Katika Kiyunani, 3 Yohana kina mstari mmoja pungufu kuliko 2 Yohana.
2. Zote mbili ni barua za binafsi zinazotupatia undani wa uhusiano wa binafsi na matatizo mionganoni mwa Wakristo wa awali.
3. Zote mbili zinachukuliwa kuwa ni nyaraka kwa wote kwa sababu hazikuandikwa kwa ajili ya makanisa maalum.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIKIANDIKA KITABU?**

- A. Mwandishi anatajwa tu “mzee” mst. 1.
  1. Neno mzee yaelekea lilitumika hapo kwa masuala ya umri wa mwandikaji kuliko suala la mzee wa kanisa.
- B. Waraka unaonesha ushuhuda kuwa uliandikwa na mtu yule yule kama ule wa 1 Yohana.
  1. Msamiati karibu unafanana.
  2. Somo kuu ni mmoja.
- C. Waandishi wa awali kama Clement wa Alexandria, Dionysius na Cyprian walimchukulia Yohana kuwa ndiye mwandishi.

#### **2. KITABU KILIANDIKWA KWA NANI?**

- A. Anuani yasema, “kwa mama mteule na watoto wake” - mst. 1.
- B. Maoni ya aina mbili kuu kuhusu huyu “mama mteule” alikuwa nani.
  1. Kumbukumbu yaelekea katika kanisa.
  2. Kumbukumbu yaelekea kwa mwanamke maalum.
    - A. Bila kujali aliyeandikiwa ni nani, ujumbe ni mmoja.

#### **3. LINI NA WAPI KITABU HICHO KILIANDIKWA?**

- A. Sababu tatu kwa kukiandika kitabu hicho:
  1. Kumjulisha aliyeandikiwa (au walioandikiwa) kuwa Yohana aliwaona wanawe wakitembea katika kweli, mst. 4
  2. Kumpa moyo aendelee kutembea katika upendo - mist. 5, 6.
  3. Kutahadharisha juu ya walimu wa uongo - mst. 7 - 11.
- B. Kuna mabishano ya kutosha yanayozingira usemi, “mafundisho ya Kristo” katika mstari wa 9.
  1. Wenye msimamo huria hututaka tuuelewe kuwa maana yake ipo tu kuhusisha mafundisho ya Uungu wa Kristo.
  2. Wengine husema yana maana mafundisho ambayo Kristo binafsi alifundisha na kwa njia ya wale waliovuviwa.
    - A. Kujumuishwa katika hayo ingekuwa uungu wa Kristo.
    - B. Pia mafundisho yahusuyo mpango wa wokovu, kanisa, ibada yake na maisha ya Kikristo.
    - C. Wenye msimamo huria hutaka walete mkanganyo katika Agano Jipy juu ya mafundisho yake kuhusu wokovu, kanisa na mambo mengine.

- C. Usemi, “mafundisho ya Kristo” unahusisha mafundisho ambayo Kristo alifundisha.
1. Katika 2 Yohana zipo semi zingine zinazofanana na huu.
    - A. “Kuenenda katika kweli” kumaanisha kufuata kweli iliyofunuliwa - mst. 4; Yn. 17:17.
    - B. “Kuenenda kwa kufuata amri zake” kwa kumbukumbu zaidi ya kuamini katika Uungu wa Kristo, mst. 6; Ebr. 5:8, 9; 11:6.
    - C. “Kuenenda katika upendo” kuonesha haja ya kushika amri za Mungu, mst. 6; Yn. 14:15.
    - D. “Kiri kwamba Yesu Kristo alikuja katika mwili hilo lathibitisha zaidi ya Uungu Wake - mst. 7; Lk. 6:46.
  2. Matumizi ya semi zinazofanana, zaonesha kwamba “mafundisho ya Kristo” panahusisha mafundisho yote ya Kristo, siyo yale tu yahusuyo uungu Wake.
    - A. Usemi, “mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo” unaonesha mambo waliyofundisha na sio tu kuwako kwake, Mt. 16:12.
    - B. Usemi, “mafundisho ya mitume” wahusisha mafundisho yao, sio tu ukweli kwamba walichaguliwa kuwa mitume, Mdo. 2:42.
    - C. Wakati mitume waliposhutumiwa kuwa “walijaza Yerusalem kwa mafundisho yao” shutuma hiyo ilihusisha kile kilichofundishwa, Mdo. 5:28, 42.
    - D. Usemi, “Mafundisho ya Balaam” unahusisha mambo aliyofundisha badala ya imani ya kuwako kwake, Ufu. 2:14.
    - E. Neno “mafundisho” humaanisha mafunzo yote ayatoayo mtu au kikundi.
      1. Sio tu kufundisha kuwa yamekuwako.
  3. Hata kama usemi huo ulihuisha tu uungu wa Yesu, ukweli huo ungedai kwamba mwanadamu afanye yote amwamuruyo, Lk. 6:46; Ebr. 5:8, 9; Mt. 7:21-23.

##### **5. MUHTASARI WA 2 YOHANA.**

- A. Shukurani za mwandishi kwa “mama mteule” na “watoto wake,” mst. 1 - 4.
- B. Kuwapa moyo kuonesha upendo wao kwa Mungu kwa kushika amri zake, mst. 5, 6.
- C. Onyo kwa wale wasioleta mafundisho ya Kristo - mist. 7 - 11.

##### **6. MASOMO TUJIFUNZAYO KUTOKA 2 YOHANA.**

- A. Amri, mafundisho na ukweli, vyote ni muhimu.
  1. Neno Amri limetumika mara tatu.
  2. Neno mafundisho limetumika mara mbili.
  3. Neno kweli limetumika mara tatu.
- B. Upendo ni muhimu.
  1. “Mama mteule” na “watoto” wake walipendwa “katika kweli” - mst. 1
  2. Kusihu “kupendana wao kwa wao” - mst. 5.
  3. Wakati mtu anaenenda katika amri za Mungu anaonesha upendo wake kwa Mungu - mst. 6.
  4. Upendo na kweli huenda bega kwa bega.
    - A. Haviko katika kutofautiana.
- C. Hatari za wadanganyaji, mist. 7 - 11.
  1. Anayeshindwa kutumia mafundisho ya Mungu hana Mungu.
  2. Walimu wa uongo wasitiwe moyo na Wakristo.
  3. Anaye wapa moyo walimu wa uongo ni mwenye hatia sawa tu na walimu wa uongo.

## **SOMO LA XXVIII - 3 YOHANA - VIONGOZI WATATU KATIKA KANISA LA AWALI .**

### **UTANGULIZI:**

1. Waraka huu unatoa habari juu ya viongozi watatu wa kanisa la awali.
  - A. Gayo alienenda katika kweli na kuwasa idia wamisionari.
  - B. Diotrefo alitaka kuwa wa kwanza katika kanisa.
    1. Ama alitaka kulitawala au kuliharibu kanisa.
  - C. Demetrio alikuwa mpole, mtumishi mwadilifu wa kanisa aliyejewa na taarifa nzuri toka kwa watu wote.
2. 3 Yohana ni waraka (kitabu) mfupi katika Agano Jipyä kuliko vitabu vyote vya Agano Jipyä katika lugha ya Kiyunani, bali katika lugha ya Kiingereza ni cha pili katika vitabu vifupi kupita vyote katika Agano Jipyä.
3. Maneno makuu matatu yapatikana kitabuni:
  - A. Ukweli linapatikana mara 5
  - B. Upendo linapatikana mara moja.
  - C. Mpendwa linapatikana mara tatu.
4. Kuna masomo mawili kwa Wakristo leo yanayopatikana katika kitabu hicho:
  - A. Wale wanaokwenda katika shughuli za injili wastahili kusaidiwa.
  - B. Ukarimu ni sifa ya Mkristo.

### **MJADALA:**

1. **NANI ALIKIANDIKA KITABU?**
  - A. Mwandishi anajitaja mwenyewe kuwa “mzee” - mst. 1
    1. Yamkini zaidi ni suala la umri na sio mzee wa kanisa.
  - B. Ufananaji wa lugha, mtindo na somo kwenye 1 Yohana na 2 Yohana kunaonesha kitabu hiki kiliandikwa na mwandi shi mmoja - Yohana.
2. **KITABU ALIANDIKIWA NANI?**
  - A. Gayo - mst.1.
  - B. Wengi wametajwa Gayo katika Agano Jipyä.
    1. Gayo wa Makedonia - Mdo. 19:29.
    2. Gayo wa Debe - Mdo. 20:4.
    3. Gayo wa Korintho - 1 Kor. 1:14; Rum. 16:23.
    4. Ni hali isiyowezekan a kusema ni Gayo yupi aliandikiwa kitabu hicho.
3. **LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA?**
  - A. Kiliandikwa mnamo wakati mmoja na yawezekana mahali pamoja pale pale kilipoandikwa 1 Yohana na 2 Yohana.
  - B. Kwa hiyo, kiliandikwa Efeso mnamo 90 B.K.
4. **KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**
  - A. Yohana alikuwa amepokea taarifa ya uaminifu wa Gayo - mst. 3 - 7.
    1. Alienenda katika kweli.
    2. Alionesha ukarimu kwa wote ndugu na wageni.
      - A. Neno mgeni limetumiwa mara nyingi kumaanisha ndugu waliokuwa katika safari.

- B. Alikwisha ambiwa matendo ya Diotrefe - mist. 9 - 11.
  - 1. Alipenda kuwa wa kwanza.
  - 2. Alimsengenya Yohana.
  - 3. Alikataa kuwasaidia ndugu waliokuwa wahitaji.
  - 4. Aliwafukuza ndugu waliowasaidia wahitaji.
- C. Yohana alihitaji kumsifia Demetrio kwa msimamo wake kwa ajili ya njia ya Kristo.

5. **MUHTASARI WA 3 YOHANA.**

- A. Sifa za Gayo - mist 1 - 8.
- B. Sifa za Diotrefe - mist. 9 - 11.
- C. Sifa za Demetrio - mist. 12 - 14.

6. **MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA 3 YOHANA.**

- A. Baraka za katika vitu zina umuhimu hafifu kuliko mafanikio ya kiroho kama vile afya ya kimwili ilivyo hafifu kuliko afya ya kiroho - mst.2; Mt. 16:26.
- B. Uaminifu wa watoto wa mtu, uwe wa kimwili au wa kiroho (katika hao watoto) ni kiini kikuu kupita vyote katika furaha, mst. 4.
- C. Wakristo wana wajibu wa kuwasaidia wahitaji, mst. 5, 6; Gal. 6:10; Yak. 1:27.
- D. Wamisionari waaminifu wanastahili msaada wa kujitolea mhanga toka kwa ndugu, mist. 6-8; Flp. 1:3-5; 4:10-17.
- E. Kile mtu anachosaidia kiwe kizuri au kibaya, kinageuka kuwa ndicho ashirikicho, 2 Yoh 9 - 11, 3 Yoh 8.
- F. Kuwa na utawala wa mtu mmoja katika kanisa ni kinyume cha muundo wa Agano Jipy - Mdo. 14:23; Flp. 1:1; Mt. 20:20-28.
- G. Watu wafanyao mema wastahili kusifiwa wakati wale watendao mabaya inapasa kuwafichua.

**MWISHO:**

- 1. Katika kitabu hiki tunaona haja ya ukarimu - Ebr. 13:2.
- 2. Twaona matatizo ya kanisa sio jambo jipy katika kizazi chetu.

## **SOMO LA XXIX - YUDA - KUISHINDANIA IMANI**

### **UTANGULIZI:**

1. Kitabu kimejaa maonyo dhidi ya wale ambao wangehatarish a usalama na amani ya kanisa.
2. Walimu wa uongo wameitwa: si watauwa, wafisadi, wasio amini, watafutaji makosa, wanafiki, wadanganyifu, wenye shauku za kimwili, wanung'unikaji.
3. Walimu wapotofu waliolinganishwa na Kaini, Balaamu, Kora, Sodoma na Gomora na malaika walioanguka.
4. Kila kitu kimewekwa katika makundi matatu:
  - A. Wasomaji walitajwa kuwa "walioitwa, waliohifadhiwa na waliopendwa - mst.1.
  - B. Aliyoyataka kwao ilikuwa ni "rehema, amani na upendo" - mst.2.
  - C. Aliwakumbusha wasomaji wake matukio matatu ya hukumu ya Mungu "Waisraeli jangwani, malaika walioanguka na Sodoma na Gomora" - mist. 5 - 7.
  - D. Kuhusu walimu wapotofu alisema wanaunajisi mwili kudharau uongozi na kunenea maovu mambo ya heshima," mst. 8.
  - E. Akaonesha kwamba walimu wapotofu walifuata mfano wa Kaini, Balaamu na Kora - mst. 11.
  - F. Aliwataja walimu wapotofu kama "wenye kunung'unika, wenye kulalamika, waendao kwa tamaa zao" - mst. 16.
  - G. Pia alisema walimu wapotofu ni "waleta matengano, wa mambo ya dunia hii tu na hawana Roho" - mst. 19.
5. Kitabu kinafundisha mtu kuwa wa dini tu hakutoshi.
  - A. Mtu anapaswa kuwa katika hali sahihi mbele za Mungu ili ampendeze Mungu.

### **MJADALA:**

1. **NANI ALIKIANDIKA KITABU?**
  - A. Yuda nduguye Yakobo - mst. 1.
    1. Kuna majina Yuda (kwa Kiingereza Jude Judas) sehemu kadhaa za Agano Jipy, pamoja na mitume wawili, Lk. 6:13-16.
    2. Ni mmojawapo wa ndugu wa Bwana - Mt. 13:55, 56; Mk. 6:3; Gal. 1:19.
    3. Yeye pamoja na ndugu zake hawakumwamini Yesu mpaka baada ya ufufuo - Yn. 7:1 - 5; Mdo. 1:14.
    4. Labda hakuwa mashuhuri kama Yakobo, lakini Yuda alikuwa ni mwinjilisti mchangamfu katika karne ya kwanza, 1 Kor. 9:5.
  - B. Ushahidi wa historia unaonesha nduguye Yakobo ndiye aliye kiandika kitabu hiki.
    1. Kumbukumbu zinapatikana katika MURATORIAN CANON ambazo ziliandikwa mwaka 170 B. K.
    2. Tertullian, mnamo 200, aliuhusisha waraka huo kuwa wa Yuda.
    3. Clement wa Alexandria mnamo 210 B.K. alimtaja Yuda.
  - C. Uvuvio wa waraka huo umehojiwa katika maeneo mawili.
    1. Imedaiwa kuwa Yuda amenukuu mengi kutoka kwenye Kitabu cha Henoko (Enoch) na "Assumption of Moses" (Makisio ya Musa), vitabu ambavyo vyote havikuwa vimevuvuviwa - mist. 9, 14.
      - A. Paulo alinukuu kutoka kwa washairi wa kidunia, lakini hilo halioneshi kuwa walihalalisha yote waliyoyasema, Mdo. 17:28; Tit. 1:12,13.
    - B. Kitabu cha Henoko (Enoch) kilipatikana mwaka 1774 katika nakala ya Biblia ya Kushi (Ethiopian Bible).
      1. Kwa mara ya kwanza ilitafsiriwa katika Kiingereza mwaka 1821.
      2. Hakiwezi kufuatiliwa nyuma zaidi ya karne ya 3.
      3. Nini kusema kuwa Yuda hakuujua unabii wa Enoch (Henoko) kwa uvuvio?

4. Nini kusema kitabu cha Henoko kisingekuwa ni nukuu ya kitabu cha Yuda kwa sababu historia ya kitabu hicho cha Henoko haifikiit kitabu cha Yuda?
- C. Kwa mujibu wa nukuu ya Yuda kuhusu Mikaeli na mashindano yake na shetani, Yuda anaweza kuwa alifahamu hilo kwa uvuvio, na mwandishi wa baadaye akamnukuu Yuda.
2. Wanaohoji hudai waraka wa Yuda ni wa kuazima toka kwa Petro kwa sababu ya sehemu nyingi kufanana.
  - A. Kwa hiyo?
    1. Wote walikuwa ni waandishi waliovuviwa, wenyewe uvuvio wa huyo huyo Roho Mtakatifu.
    - B. “Kuazima” kutoka mwandishi mwingine aliyeuvuviwa hakupinga kufanyika hilo kwa Uvuvio.
    - C. Ni dhahiri yawezekana kwamba Roho Mtakatifu alifunua ujumbe wa namna moja moja kwa waandishi wote wawili kwa sababu walikuwa wakipamban a na jambo/hali ya namna moja, Isa. 2:1-4; Mika 4:1-4.

## 2. KITABU ALIANDIKIWA NANI?

- A. “...Walioitwa/waliopend wa na Mungu Baba,” mst. 1.
- B. Hakuna kinachoonesha kama hawa walikuwa Wayahudi au Wamataifa.
  1. Hakuna mazingira ya kijiografia yaoneshayo.
  2. Linashughulikiwa jambo la aina moja (tatizo moja) katika kanisa zima - walimu wapotofu.

## 3. LINI NA WAPI KITABU KILIANDIKWA?

- A. Haioneshi Yuda alikuwa wapi alipokiandika kitabu hicho.
  1. Labda Palestina, lakini hilo haliwezi kufahamika dhahiri.
- B. Kiliandikwa sehemu ya pili ya kipindi cha karne ya kwanza kwa sababu kinashughulikia tatizo lililokuwa limeenea zaidi wakati huo.

## 4. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA.

- A. Lengo lilikuwa kuandika kuhusu wokovu wa kawaida - mst. 3.
  1. Hata hivyo, tatizo lilizuka katika kanisa ambalo lisabisha abadili mpango wake.
- B. Anaandika kulipa moyo kanisa, “kuishindania imani” - mst.3.
  1. Neno “kushindania” humaanisha kuijingiza katika pambano kama mshindanaji.
    - A. Linatokana na neno la Kiyunani ambalo huleta neno la Kiingereza “agonize” (kuwa na uchungu mwingi).
  2. Usemi “imani” unahusisha injili - Mdo. 6:7; Flp. 1:27; Gal. 1:23; Efe. 4:5, 13.
  3. Neno “mara moja” laonesha wazo la mara moja kwa hali zote, 1 Pet. 3:18; Ebr. 9:12, 27; 10:10.
    - A. Wazo ni kuwa Neno la Mungu limekwisha funuliwa, limethibitishwa na kuandikwa mara moja kwa utmilifu.
      1. Hilo linashughulikia wazo la usfunuo wa baadaye.

## 5. MUHTASARI WA KITABU CHA YUDA.

- A. Salaam na sababu za kuandika - mist. 1 - 3.
- B. Mfano wa walimu wapotofu na watu waovu - mist. 4 - 7.
- C. Maelezo juu ya walimu wapotofu na uovu wao - mist. 8 - 16.
- D. Utabiri wa mtume juu ya walimu wapotofu - mist. 17 - 19.
- E. Namna ya kuwashughulikia waliopotoshwa na walimu wa uongo - mist. 20 - 23.
- F. Baraka - mist. 24, 25.

**6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA KITABU CHA YUDA.**

- A. Kuna imani moja tu sio nyingi mst. 3; Efe. 4:5.
- B. Mtu anapaswa awe mwanadini kihalali na sio kuwa mwanadini tu, ili ampendeze Mungu - mst. 3; Efe. 4:4-6; Mt. 7:21-23.
- C. Kuna mwongozo wa kweli uitwao “imani” au “injili” ambao wapaswa kutumika ili kuzijaribu imani, maoni na matendo ya mtu, Mdo. 17:11; Gal. 1:6-12.
- D. Daima kuna hatari ya walimu wa uongo wawaong ozao waaminifu katika upotofu, mst. 4; Mt. 7:13-23; Mdo. 20:29-31; 1 Tim. 4:1-5.
- E. Walimu wa uongo huonekana wapole, safi, adilifu, wanyenyekemu, wenye upendo, watulivu, wema ili kuwandanganya kiurahisi zaidi walio wepesi wa kudanganyika, mst. 4; Mt. 7:15; Rum. 16:17, 18; 2 Kor. 11:13-15.

**MWISHO.**

1. Walimu wapotofu daima watakuwepo.
2. Ni muhimu daima waaminifu wawe tayari kuishindania imani - 2 Pet. 3:15; Yuda 3.

## **SOMO LA XXX - UFUNUO - MSIBA NA SHANGWE.**

### **UTANGULIZI:**

1. Ufunuo kitabu ambacho kimeachiliwa zaidi kuliko vyote, kinachokang anya zaidi kuliko vyote na hata hivyo kinajadiliwa, katika Biblia nzima.
2. Kuna pande mbili zenye upeo kuhusu kitabu cha Ufunuo.
  - A. Kukigeuza na kukipotosha ili kufikia uamuzi wa kutisha na kushangaza katika unabii uhusuo mwisho wa vitu vyote.
  - B. Kukipuza kabisa kwa kuhofia yale yanayoweza kufahamika, kwa kuamini kwamba kwanza mwanadamu hakukusudiwa akielewe kitabu hicho.
3. Ufunuo ni ufunuo wa Yesu Kristo - 1:1.
  - A. Neno “ufunuo” latoka katika neno la Kiyunani “apokalupsis” maana yake “kufunua, kufumbua.”
  - B. Wale wasomao, kusikia na kuvitunza vitu vya kitabu hicho watabarikiwa - 1:3.
4. Kinafunua shangwe ya mwisho dhidi ya uovu, kweli dhidi ya makosa, wateswao juu ya watesaji na Kristo dhidi ya Shetani.
5. Neno kuu la Ufunuo ni ushindi.
  - A. Ujumbe wake ni Wakristo hatimaye watashangilia ushindi dhidi ya ulimwengu.

### **MJADALA:**

#### **1. NANI ALIANDIKA KITABU HICHO?**

- A. Madai kuwa kiliandikwa na Yohana - 1:1, 4 , 9; 22:8.
  1. Wazo liliwahi kutolewa kwamba kiliandikwa na mwandishi aliyekuwa mzee wa kanisa Efeso aliyeitwa Yohana.
  2. Wengine walitoa wazo kwamba mwandishi alikuwa Yohana Marko.
- B. Wanahistoria wa awali kushuhudia uandishi kuwa ni wa Yohana Mtume katika kitabu hicho.
  1. Justin Martiyr - B.K 110 - 165.
  2. Irene (Irenaeus) - B.K. 120 - 202.
  3. Clement wa Alexandria - A.D. 153 - 217.
  4. Tertullian - A.D. 145 - 220.
  5. Origen - A.D. 185 - 254
  6. Hippolytus - A.D. 170 - 236.
- C. Uandishi wa Yohana unakanwa kwa sababu ya lugha iliyotumika.
  1. Kiyunani cha Ufunuo kimetumika kuwa tofauti sana kulinganisaha na 1 Yohana, 2 Yohana, 3 Yohana.
  2. Ifahamike kwamba vitabu vingine alivyoviandika viliandikwa katika wakati wa starehe, ambapo Ufunuo kiliandikwa katika hali ya msisimko mkubwa kwa jinsi maono yalivyokuwa yakijifunua mbele zake.
  3. Ifahamike pia kwamba kuna miliganisho mingi inayoonekana katika vitabu hivi.
    - A. Kristo anatajwa kuwa ni “Neno,” Yn. 1:1; 1 Yoh. 1:1; Ufu. 19:13.
    - B. Maneno kushinda, kupata ushindi yanapatikana katika Yn. 16:33; mara kadhaa katika 1 Yoh na Ufunuo.
- D. Waandishi wa awali wanashuhudia kwamba Yohana aliondoka Yerusalemu muda mfupi kabla haujaangamizwa na akaja Efeso ambako aliutumia muda wa maisha yake uliobaki.

#### **2. NANI ALIANDIKIWA KITABU HICHO?**

- A. Anuani ni kwa "makanisa saba ya Asia" - 1:4; sura ya 2 na 3.
  - 1. Haya ni makanisa yaliyoanzishwa na Paulo - Mdo. sura ya 19,20.
  - 2. Yaonekana dhahiri (zaidi) yaliandikiwa makanisa yote kila mahali.
- B. Asia Ndogo ilikuwa ni ngome ya Ukristo katika robo ya mwisho ya karne ya kwanza.

### **3. KWA NINI KITABU KILIANDIKWA?**

- A. Makanisa yaliingia katika mateso makali mno yaliyowapata tangu kuwanza kwa Kanisa.
  - 1. Yesu alikuwa ametabiri kwamba ulimwengu ungewachukia wanafunzi wake - Yn. 15:18 - 20.
  - 2. Paulo alionya pia kuhusu mateso kwa sababu ya Neno la Mungu - Mdo. 14:22; 2 Tim. 3:10 - 12.
- B. Yohana alikuwa uhamishoni Patmo - 1:9.
  - 1. Patmo ni kisiwa cha mwamba, maili 24 nje ya pwani ya Asia Ndogo na maili 70 kusini magharibi mwa Efeso.
  - 2. Eneo lake lilikuwa kiasi cha maili 50 za mraba.
  - 3. Wafungwa wa kisiasa walipelekwa kufanya kazi kwenye machimbo ya chumvi.
- C. Ufunuo kiliandikwa kuwapa moyo Wakristo waliokuwa katika mateso, akiwaonesha kuwa Mungu alikuwa katika kiti chake cha Enzi, na wangeshinda mateso.
- D. Kitabu kiliandikwa katika lugha ya mfano 1:1.
  - 1. Mifano hiyo ingeeleweka kwa Wakristo.
    - A. Lakini isingeelweka kwa watesaji wa Kirumi.
- E. Kitabu hicho kiko katika aina ya maandiko yajulikanayo kwa Kiingereza kama "Apocalyptic".
  - 1. Lugha ya Apocalyptic ni:
    - A. Mifano (methali) ya hali ya juu.
    - B. Ilitumika kipindi cha mateso.
  - 2. Ilitumika sehemu kidogo katika Agano la Kale kwenye vitabu Ezekiel, Danieli na Zekaria.
  - 3. Ilivuma sana kipindi kati ya 200 K.K. na 200 B.K.

### **4. KITABU KILIANDIKWA LINI NA WAPI?**

- A. Yadaiwa kiliandikwa na Yohana akiwa uhamishoni Patmo - 1:9 - 11; 10:4; 14:13; 19:9; 21:5.
- B. Tarehe tofauti zimekisiwa:
  - 1. 64 - 68 A.D. wakati wa utawala wa Nero.
  - 2. 69 - 79 A.D. wakati wa utawala wa Vespasian.
  - 3. 81 - 96 A.D. wakati wa utawala wa Domitian.
- C. Kipindi cha Nero kilikubalika zaidi katika karne ya 19.
  - 1. Mateso ya kwanza ya Kirumi yalikuja wakati wa utawala wa Nero ambaye alilaumu kuhusu kuungua kwa moto mji wa Rumi akiwasngizia Wakristo.
  - 2. Hakuna ushahidi kuwa mateso hayo yalikuwa ya kote duniani.
    - A. Wala hakuna ushahidi kwamba yalikuwako kwa sababu za kidini.
  - 3. Ushahidi wa ndani uliokaririwa kwa ajili ya kipindi hicho:
    - A. Kutajwa kwa makabila kumi na mawili ya Israeli kwa kuwa rekodi zote za makabila ziliharibiwa wakati wa kuteketezwa kwa Yerusalem.
    - B. Katika sura ya 11:1 Yohana anaambiwa alipime hekalu, hali inayoonesha ni tukio la kabla ya 70 A.D.
      - 1. Kwa sababu ya hali ya lugha ya mfano hatuwezi kuchukulia kuwa ni makabila au hekalu, kama lugha ya kawaida.
    - C. Imekwisha semwa kuwa mnyama wa 13:18 ni Nero kwa maana Neron Kaisar katika Kiebrania ina tarakimu yenye kulingana na 666.

1. Ambalo halizingatiwi hapo ni kwamba kwa nini Yohana angetumia Kiebrania wakati anawaandikia watu wanaoongea Kiyunani?
2. Vile vile kuhitimisha hivyo inabidi herufi moja ya Kiebrania iachwe.
3. Wengine wametumia lugha nyingine na kupata Euranthas, Lateinos na Titan katika Kilatini au Kiyunani.
4. Hapa vile vile ni muhimu kukumbuka kuwa kitabu hiki kimeandikwa katika lugha ya mifano.
5. Tarakimu 6 imepungua 1 kwa iliyokamili 7.
  - A. Kwa hiyo ni mfano au ishara ya maafa.
  - B. Kuizidisha mara tatu ni ukamilifu wa kushindwa.
- D. Kipindi cha Vespasian kimeshikiliwa na wanazuoni wachache.
  1. Hakuna msaada wa ushahidi wa nje juu ya maoni hayo.
  2. Aya moja tu inaweza kusemwa kusaidia juu ya muda huo, 17:9-11.
    - A. Tunaona wafalme saba wanatajwa.
      1. Watano wameanguka, mmoja yupo na mmoja anakuja.
      - B. Imedhaniwa kuwa wafalme hao ni wafalme wa Rumi kuanzia: Agusto akifuatiwa na Tiberio, Caligula, Klaudio na Nero.
        1. Hao ndio watano walioanguka.
      - C. Mmoja aliyekuwako angekuwa ni Vespasian aliyekuwa mtawala wakati huo.
      - D. Yule ambaye hakuwa amekuja angekuwa ni Tito ambaye alitawala miaka miwili tu, 79-81 A.D.
      - E. Mnyama ambaye ni wa nane angekuwa ni Domitian.
    3. Matatizo ya makisio hayo ni :
      - A. Wafalme watatu wanarukwa - Galba, Otho na Vitellius - ambao walitawala kwa muda mfupi kati ya Nero na Vespasian.
      - B. Hakuna ushahidi wa historia kwamba Vespasian aliwatesa Wakristo.
  - E. Tarehe zinazokubaliwa zaidi ni wakati wa utawala wa Domitian.
    1. Irene alisema iliandikwa na Yohana karibu na mwisho wa utawala wa Domitian.
    2. Domitian alikuwa ni mfalme wa kwanza wa Kirumi aliyeanzisha rasmi mateso kwa Wakristo katika hali ya ujumla.
      - A. Kwa kukagua jinsi watu wanavyomtii na himaya ya Kirumi, watu walilazimika kufanya matoleo kwenye sanamu yake.
      - B. Ingawa Nero alipokea kuabudiwa kama mungu, hali ya uungu aliisubirisha mpaka kipindi cha baada ya kifo.
        1. Domitian alidai aabudiwe kama mungu wakati akiwa hai.
  - F. Hivyo, tunahitimisha kwamba Ufunuo kiliandikwa na Yohana kisiwani Patmo mnamo 95 B.K au 96 B.K.

## **5. MUHTASARI WA KITABU CHA UFUNUO.**

- A. Makanisa saba ya Asia - sura ya 1 - 3.
- B. Muhuri saba - sura ya 4 - 7.
- C. Baragumu saba za hukumu - sura ya 8 - 11.
- D. Mwanamke na mwanaye wateswa na joka na wasaidizi wake - sura ya 12 - 14.
- E. Vitasa saba vya ghadhabu - sura ya 15, 16.
- F. Anguko la kahaba mkuu na mnyama - sura ya 17 - 19.
- G. Hukumu, mbingu mpya na nchi mpya - sura ya 20 - 22.

## **6. MASOMO TUJIFUNZAYO TOKA KITABU CHA UFUNUO.**

- A. Mitazamo minne ya kitabu cha Ufunuo.
1. Mtazamo wa wakati ujao: Hushikilia kwamba sura zote kuanzia 4 - 22 huelezea matukio yatakayotokea baadaye, lakini yatakuja punde na kupita.
    - A. Mawazo ya vipindi vya miaka elfu moja (Pre millenialism).
    - B. Kosa lake ni kuchukua lugha ya mfano na kuifanya ni ya kawaida.
    - C. Kwa msimamo huo kitabu cha Ufunuo kisingeleta faraja yo yote kwa Wakristo wa karne ya kwanza walioteswa.
  2. Mtazamo wa maendelezo ya mtazamo wa Kihistoria - hushikilia kwamba sura ya 4 - 22 ni maeleo juu ya historia ya kanisa kuanzia mwanzo wak hadi mwisho wake.
    - A. Msimamo ambao wakati mmoja ulishikwa sana na Waprotestanti.
    - B. Unahitaji kupindua pindua ukweli wa historia.
    - C. Hushughulikia zaidi historia ya kanisa katika Ulaya Magharibi.
    - D. Pia hutoa nafuu kidogo sana kwa Wakristo wa karne ya kwanza.
  3. Mtazamo uitwao Preterist - Kushikilia kwamba kitabu chote cha Ufunuo ni mambo ambayo yalitimia katika karne za kwanza, mbili au tatu za Ukristo.
    - A. Mtazamo huo una uhusiano mdogo sana kwa sasa.
    - B. Jambo kuu zaidi ni kwamba hufundisha kuwa Ufunuo kilikuwa na ujumbe kwa Wakristo wa karne ya kwanza.
    - C. Vile vile kwa usahihi husisitiza mazingira ya historia.
    - D. Udhafu wa mtazamo huo ni kuwa hauna ujumbe kwa ajili ya leo.
  4. Mtazamo wa Falsafa ya Historia - Hushughulikia misingi ya Ufunuo.
    - A. Hukifanya kitabu kiwe cha kufaa kwa nyakati zote.
    - B. Hauhusishi kukisia au kutotumia ipasavyo mifano au kupindua pindua ukweli wa historia.
    - C. Ni wa ujumla mno na hautoi msisitizo wa kutosha kwenye mazingira ya historia.
- B. Mtazamo wa tano ni ule uitwao Mtazamo wa Mazingira ya Historia.
1. Husisitiza umuhimu wa Mazingira ya Historia.
  2. Husisitiza misingi ya kitabu.
  3. Hushughulika na ukweli na misingi na kuepuka makisio yanayopatikana katika mitazamo mingine.
- C. Kitabu chafundisha kuwa Mungu anafahamu yatokeayo kanisani, 1:12, 13, 20.
- D. Makanisa yale ambayo hayana uaminifu na matunda, vinara vyake vitaondolewa, 2:5.
- E. Mungu hataruhusu mafundisho ya upotofu katika kanisa Lake - 2:2, 9, 14, 15; 3:9.
- F. "Kuitunza nyumba" kwa ajili ya Bwana hakutampendeza yeye - 3:1, 2, 14 - 16.
- G. Ufalme ulikuwepo katika karne ya I kwa sababu Yohana alikuwa ndani yake - 1:9; 1 Kor. 15:24 - 26.
- H. Mungu yuko katika kiti chake cha Enzi na Anadhibiti bila kujali ulimwenguni kunatokea nini (Mungu haathiriki na mipango ya watu duniani) - 4:1 - 11.
- I. Kupokea taji ya uzima mtu anapaswa awe mwaminifu hata kufa - 2:10.
- J. Kazi zitendwazo na Wakristo sio za bure, bali zawafuata ng'ambo ya kaburi - 14:13; 1 Kor. 15:58.
- K. Siku Kuu yaja wakati watu wote watahukumiwa - 20:11 - 15.
- L. Kusema uongo kutamfanya mtu awe nje ya mbinguni - 21:8, 27.
- M. Jehanum ni mahali halisi na pamewekwa kwa wasiotenda haki - 20:15; 21:8.
- N. Mtu hastahili kuongeza wala kupunguza kutoka katika Neno la Mungu - 22:18, 19.

### **MWISHO:**

1. Tuwe waangalifu, kutoingiza na kushikilia mawazo ambayo hayawiani katika kitabu hiki (na kuyageuza ni mafundisho).
2. Ujumbe muhimu ni kwamba, Mungu ni mdhibiti na watoto Wake ni zaidi ya washindi.





